ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao Cha Kwanza - Tarehe 11 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA MHESHIMIWA SPIKA WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KUHUSU KIFO CHA RAIS MSTAAFU WA AFRIKA KUSINI, MAREHEMU MZEE NELSON MANDELA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa naomba niwakaribisheni sana katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Baraza la Wawakilishi lililoanza leo. Mwenyezi Mungu akitujaalia kuwa sote ni wazima na kuhudhuria shughuli zetu kuanzia leo hii siku ya tarehe 11/12/2013.

Waheshimiwa Wajumbe taarifa ya Spika kwa leo inahusu kifo cha Rais Mstaafu wa Afrika ya Kusini, Marehemu Mzee Nelson Mandela.

Waheshimiwa Wajumbe, nakumbuka kwamba hivi karibuni ulitokea msiba mzito wa kuondokewa na kiongozi wetu humu, Kiongozi wa Afrika ya Kusini ambaye alikuwa ameugua kwa muda mrefu. Nimeona kwamba ni muhimu kwa kiongozi mkubwa kama huyu wa Afrika na sio tu katika Afrika na si tu kwa ajili ya Afrika ya Kusini, lakini ni kiongozi wa Dunia nzima akitambuliwa, basi tusianze shughuli zetu kabla ya kumkumbuka.

Katika kumkumbuka inabidi angalau kwa kifupi tuelezee juu ya harakati na umuhimu wake katika uongozi wake kwa nchi ya Afrika ya Kusini.Lakini pia, katika uongozi wake huo ndani yake kuna mafunzo makubwa ambayo hata sisi viongozi wa nchi nyengine katika nchi zetu za Kiafrika na hata duniani kote, kuna mambo ya kujifunza kutoka kwake kutokana na harakati za uongozi wake nchini Afrika ya Kusini na duniani kote.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuanza shughuli za Mkutano wetu huu wa kumi na nne wa Baraza la Wawakilishi, nimeona nitoe taarifa hii katika kuungana na wenzetu wa Afrika ya Kusini na wengine wengi duniani katika msiba mkubwa ambao umelipata taifa la Afrika ya Kusini, Bara la Afrika na duniani kote kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa kwanza wa Afrika ya Kusini mwenye asili ya Kiafrika Mzee Nelson Mandela, ambaye pia ni Rais wa kwanza wa Afrika ya Kusini aliyechaguliwa kwa demokrasia halisi.

Umuhimu wa kumkumbuka kiongozi huyu kutokana na ujasiri wake na namna harakati za ukombozi wa Afrika ya Kusini kutokana na utawala wa kibaguzi ulioota mizizi nchini humo. Historia inaonyesha kuwa jitihada hizo zilikuwa ni ngumu sana na ziliwezekana baada ya Mzee Nelson Mandela kujitoa muhanga katika harakati hizo.

Lakini cha zaidi ni namna ambavyo alifanikiwa kuondosha ubaguzi na ukabila na akaendelea kuwaunganisha Waafrika wa Kusini waliokuwa kwenye matabaka na kujenga misingi ya demokrasia ya kweli. Hatua hizi zinamfanya marehemu Mzee Nelson Mandela kuwa ni mwanaharakati wa kupigiwa mfano duniani.

Mzee Nelson Mandela alizaliwa tarehe 18 Julai, 1918 huko kijijini kwao Qunu, nchini Afrika Kusini. Harakati za kuwakomboa wananchi dhidi ya udhalimu wa wazungu wachache alizianza mapema ambapo akiwa katika Chuo Kikuu cha *Fort Hare* nchini Afrika Kusini alishiriki katika maandamano ya wanafunzi na mwaka 1940 alifukuzwa katika chuo hicho kutokana na kushiriki kwake katika maandamano hayo.

Maandamano hayo yaliyokuwa na lengo la kupinga ubaguzi waliokuwa wakifanyiwa wananchi wa Afrika ya Kusini. Baada ya kufukuzwa katika chuo hicho, Mzee Nelson Mandela aliendelea na masomo na kuhitimu Shahada ya Kwanza ya Sanaa *(B.A)* mwaka 1941, ambapo alikuwa akisoma kwa njia ya mawasiliano *(by correspondence)*. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha *Witwatersrand* akichukua Shahada ya Sheria.

Waheshimiwa Wajumbe, harakati za kisiasa za Mzee Nelson Mandela zinahusisha juhudi kubwa zilizochukuliwa na viongozi wenzake katika kuanzisha Umoja wa Vijana wa Chama cha *ANC* mwaka 1944 na mwaka 1948, alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu Taifa wa Umoja wa Vijana wa chama hicho. Kiongozi huyu alishiriki katika matukio mbali mbali ya kupinga amri zilizotolewa katika Utawala wa Ubaguzi wa rangi ili kushindikiza kuondolewa kwa ubaguzi wa rangi nchini humo na kutokana na kushiriki kwake katika harakati hizo, Mzee Nelson Mandela alikutana na misukosuko

kadhaa ikiwemo kufungwa, kuzuiwa kushiriki katika siasa na mikusanyiko mbali mbali nchini humo.

Kiongozi huyu shupavu alikamatwa mwaka 1956 akiwa na wenzake ambapo walishtakiwa kwa kosa la uhaini na mwaka 1961 waliachiwa huru ambapo Mzee Nelson Mandela alikuwa mshtakiwa, lakini pia, alitekeleza jukumu la kuwatetea wenzake kama mwanasheria baada ya wakili aliyekuwa akiwatetea kujiondoa katika jukumu hilo.

Mzee Nelson Mandela na viongozi wenzake walikubaliana juu ya umuhimu wa kupinga ubaguzi na kuleta haki kwa njia ya kuendesha mapambano kutokana na nguvu waliyokuwa wakiitumia watawala wachache wa Kizungu. Kundi la *Umkhonto we Sizwe* lilianzishwa na Mzee Nelson Mandela kuwa Kamanda wake mkuu wa kwanza. Kutokana na harakati mbali mbali zilizoendeshwa na Mzee Nelson Mandela na wenzake katika kupinga udhalimu wa serikali ya Wazungu wachache iliyoendesha ubaguzi wa rangi, serikali hiyo iliwafungulia kesi maarufu ya *Rivonia* viongozi hao mwaka 1963, ambapo pamoja na mashtaka mengine, viongozi hao walifunguliwa mashtaka ya kupanga kuiangusha serikali ya wazungu wachache.

Viongozi hao walihukumiwa kifungo cha maisha jela mwaka 1964. Katika kesi hiyo, Mzee Nelson Mandela alihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 27 jela, lakini baadaye aliachiwa huru kutoka gerezani tarehe 2 Febuari, 1990 kutokana na vuguvugu kubwa la kampeni ya kuachiwa huru kwake ndani na nje ya Afrika Kusini.

Mwaka 1994, Mzee Nelson Mandela alichaguliwa na wananchi wa Afrika Kusini kuwa Rais wa nchi hiyo na kumaliza kabisa Utawala wa Wazungu wachache. Mzee Nelson Mandela anakumbukwa kwa maneno yake yenye msisimko na ushujaa wa hali ya juu ambayo ninayanukuu kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili;

> ‘Nimesimamia misingi ya demokrasia na jamii iliyo huru ambayo watu wote wanaishi katika amani na kupata fursa sawa; ni misingi ambayo natarajia kuishi nayo na kuona ikifanikiwa. Lakini itakapobidi, ni misingi ambayo nipo tayari kufa kwa ajili ya kuitetea’

Hayo ni maneno ya Mzee Nelson Mandela kwa tafsiri isiyorasmi ya Kiswahili ambayo yeye aliyatumia kwa lugha ya Kiingereza.

Waheshimwa Wajumbe, tuna mengi sana ya kujifunza kutoka kwa shujaa huyu kwa uzalendo na ubinadamu uliooneshwa na Mzee Mandela, ila kwa wakati naomba tumuombee dua na kabla ya kusimama nataka kuongeza jambo moja muhimu sana.

Kwamba pamoja na harakati zote ambazo Mzee Nelson Mandela alikuwa nazo ameendesha katika kuondoa Utawala wa Ubaguzi wa rangi katika nchi ya Afrika ya Kusini, lakini ni mtu ambaye hakuonesha wala hakuwa na nia ya kulipiza kisasi kwa vitendo ambavyo yeye mwenyewe walikuwa amefanyiwa.

Kukaa kwake jela na kuteswa sana pamoja na matatizo mengi ambayo alipata, lakini bado alikuwa na nia ile ile kuwaunganisha Wananchi wa Afrika ya Kusini kubakia kitu kimoja kama wananchi wamoja. Jambo hili limewezesha wananchi wa nchi hiyo weupe na weusi kuishi kwa amani na utulivu kuweza kuendesha nchi yao kwa amani na utulivu. Kwa mnasaba huo, basi na kwa sababu ya msiba huo mkubwa, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe sasa tusimame kwa muda wa dakika moja ili tumkumbuke kiongozi huyu wa Afrika na Duniani kote kwa ushujaa.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walisimama kwa muda wa dakika moja)

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha hati Mezani naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kukutana hapa katika kikao hichi kitukufu na kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu, Mwenyezi Mungu atuwezeshe kufanya hivyo kwa amani na utulivu mkubwa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba sasa kuwasilisha mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 23 Ogasti, 2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny/Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, Vijana, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, naomba kuwasilisha Hati Mezani ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa jamii, kuhusu Mswada wa Sheria wa kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo mengine hanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 5

Kuenziwa kwa Askari Waliouwawa Dafur

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny.Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza :-
Kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kutuleta hapa tukiwa hai na tukiwa tunatumia pumzi zake, huu ni uwezo wake mkubwa.

Vile vile, kabla ya kujibiwa swali la Nam. 5, nataka nitoe pole kwa Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kifiwa na mama yake mzazi kilichotokea Kitongoji Pemba.

Hivi karibuni Tanzania imepata pigo kubwa baada ya kuuliwa kwa askari wake waliokuwa katika ulinzi wa amani wa *UN* huko Dafur, kwa bahati mbaya sana miongoni mwa askari waliofariki ni kutoka upande wa Zanzibar.

(a) Ni kwa kiasi gani familia za askari hao kwa upande wa Zanzibar zilishirikishwa kuanzia hatua ya mapokezi ya maiti hao, kuwatambua na hatimae kuwazika.

(b) Kwa kuwa kadhia ya Askari wetu hao iliwafikia pale walipokuwa wakifanya kazi ya umoja wa Mataifa huko Dafur. Je, Umoja wa Mataifa umeshiriki kiasi gani katika kuzihudumia Serikali pamoja na familia za marehemu wapiganaji hao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu :-

Mhe. Spika, nami kabla ya kujibu swali naomba nitoe mkono wa pole kwa mwenzetu Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa kufiliwa na mama yake. Aidha nitoe mkono wa pole kwa ndugu yangu Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kufiliwa na mama yake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 5, naomba nitangulize maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli mnamo tarehe 13 Julai 2013, askari saba wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakiwa kwenye ulinzi wa Amani, Dafur nchini Sudan waliuawa baada ya kushambuliwa na kikundi ambacho hakikuweza kufahamika. Miongoni mwa askari waliofariki walikuwamo askari waliotoka Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 5 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mara baada ya kutokea vifo hivyo, Mkuu wa Majeshi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliwajuilisha rasmi wafiwa wote. Alifanya mawasiliano na kusaidia na familia ya marehemu kufahamu maeneo ambapo misiba ingefanyika ili kusaidia huduma za chakula, ujenzi wa mahema, usafiri na huduma nyengine muhimu kwa wafiwa.

b) Mhe. Spika, kufuatia msiba huu, Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania liliandaa utaratibu wa kurejesha nchini miili ya marehemu ambayo ilipokelewa tarehe 20/7/2013. Familia za marehemu ambazo hazikuwa na wenyeji mjini Dar-es-Salaam zilizigharamiwa huduma za Hoteli wakati wakisubiri mapokezi na kuagwa marehemu hao. Kadhalika Umoja wa Mataifa ulitoa Dola za Kimarekani elfu sabiini (*USD* 70,000/-) kwa kila familia iliyofiwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema Peponi roho za marehemu *AMIN*.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kuna malalamiko mengi ya askari hasa kwa wale wanaotumikia vyombo vya Muungano waliokuwepo hapa Zanzibar juu ya viinua vyao mgongo, pencheni zao na hata wale wangine ambao walipatwa na maafa kama hayo ya kufariki.

Kwa kuwa wengi wa askari hawa ambao wale waliostaafu na wengine ambao tayari wameshatangulia mbele ya haki kwa matatizo kama hayo, wengine wengi familia zao hazina uwezo wa kuweza kufatilia matatizo yao hasa katika suala hilo la viinua mgongo na pencheni. Kwa kuwa wizara yako inajishughulisha na mambo hayo yanayohusiana na forodha. Na kwa kuwa wengi hawana elimu ya kwamba wafuatilie wapi.

Je, wizara yako imeandaa utaratibu gani hasa na imetoa elimu gani kwa wenzetu hawa wastaafu juu ya namna ya kufuatilia viinua mgongo katika Wizara yako hiyo ambayo ni kiunganishi baina ya serikali hii na Serikali ya Muungano.

Mhe. Spika: Nafikiri Mheshimiwa suala hili ungeliandikia karatasi ili uliulize liwe ni swali la msingi. Tunachokizungumzia hapa ni askari waliokufa huko Dafur. litafutie utaratibu wa kuliuliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwa kuwa matukio ya Askari wetu wa jeshi la Wananchi wa Tanzania kupoteza maisha yamekuwa yakijirudia baada ya askari mwengine kukabiliana na Kikundi cha M23.

Je, serikali ina mpango gani wa kuepusha maafa kama hayo yasiweze kutokea, ingawa ni askari ni wajibu wake kupigana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, sikulipata sawa sawa namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa sababu ya tatizo la eko azungumze tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kuwa matukio ya askari wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania yamekuwa yakijirudia kutokana na vifo. Hivi karibuni askari wetu mmoja katika kukabiliana na kikundi ya M23 alipoteza maisha.

Je, serikali ina mpango gani wa kuepusha maafa kama hayo yasiweze kutokea pamoja na kwamba askari ni wajibu wake kupigana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania siku zote inachukua kila hatua kuhakikisha kwamba askari wetu wanapewa mafunzo ya kutosha katika kukabiliana na uwadui.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba jeshi letu lina uwezo mkubwa katika kukabiliana na maadui ndani na nje ya nchi yetu. Lakini katika jitihada hizi hutokea bahati mbaya. Nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hutokea bahati mbaya na askari wetu kwa kiwango kikubwa wanajihami na wanao uwezo huo na wana mafunzo ya kutosha ya kupambana na adui yeyote yule. Tuendelee kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya na nzuri ya kulitumikia taifa hili.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili ya nyongeza.
Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mbali na askari hawa, waliofariki kutokana na shambulio la waasi kule Dafur kuna mwanajeshi mmoja kutoka katika kikosi cha Ali Khamis *Camp* ambaye alipotea katika mazingira yasiyoeleweka. Na kwa kuwa familia ya marehemu kijana huyu wametaka kujua juu ya kijana wao alipo na kwa kuwa askari wenzake wengi wamesharudi na yeye haeleweki, lakini hadi sasa hawajapata majibu yeyote kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano.

a) Namuuliza Mhe. Waziri, je, serikali inafahamu kuhusu jambo hili.

b) Serikali inaiambia nini familia ya kijana huyo ambaye amepotea katika mazingira ya kutatanisha na hadi leo hii hawajapata majibu yeyote juu ya kijana wao huyu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, swali lake lenye (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa mpaka sasa serikali haijapokea taarifa rasmi ya kupotea kwa kijana huyo anaetokea kambi ya Ali Khamis *Camp* kama alivyoeleza Mhe. Salmin Awadh Salmin. Lakini nitachukua jitihada za kuwasiliana na Brigedia Kamanda ambaye ndiye dhamana katika maeneo haya ya Unguja na Pemba na sehemu nyengine ili niweze kujua hilo tukio na niweze kulitolea taarifa rasmi.

Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tutachukua hatua hizo ili kupata uhakika wa jambo hili na baadaye tutawasiliana na familia kwa ukamilifu.

Nam. 22

Kuanguka Kwa Ukuta Wa Hospitali Ya Mnazi Mmoja Sehemu Ya Pwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 22 nataka nichukue fursa hii kumpa pole Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa kifo cha mama ake mzazi Bi Fatma Idarus ndugu yake Naibu Waziri wa Elimu mstaafu Mwinyiwesa Idarus alichozikwa Muyuni.

Vile vile, nataka nitoe pole kwa Dokta Maliki kwa mtihani uliomkuta na naomba tumuombee duwa Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi waliokuwepo nje, Mwenyezi Mungu amjaalie irudi hali yake kama vile ilivyokuwa mwanzo. Ni mtihani mkubwa na ni pigo kubwa kwa Wizara ya Afya. Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza swali langu kama hivi ifuatavyo:

Sehemu ya ukuta wa Hospital ya Mnazi Mmoja, eneo la Pwani imebomoka na ukuta umeanguka. Hali hiyo inatishia usalama kutokana na wizi kupita sehemu hiyo na kuingia ndani ya maeneo ya Hospitali.

(a) Lini ukuta ule utajengwa haraka ili kuzuwiya wezi kuingia ndani.

(b) Kutokana na ukuta ule kuanguka kwasababu ya nguvu za mawimbi ya bahari, kwa nini mfumo wa ujenzi wa ukuta ule usibadilishwe na kuwekwa vikuta vizito vya zege kama vile vilivyowekwa kwenye bustani ya Forodhani ambavyo ni madhubuti na vinahimili nguvu za mawimbi ya bahari.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba unipe ruhusa niweze kuwashukuru watu wote wa nchi hii kwa njia moja au nyengine walioshiriki kwa hali na mali, kwa fikra na mawazo wakati mgumu nilioupata mimi na familia yangu, lakini kutokana na wao kuwa karibu na mimi ninashukuru nimepata nguvu ninawashukuru sana.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake nambari 22 kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli sehemu ya ukuta wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ulibomoka na sababu ya msingi ulipitiwa chini yake na mizizi ya mti wa mkungu uliokuwa karibu yake na si kwamba ukuta huo haukuwa imara kama hoja ilivyojengwa. Kwa sababu kama maji yanapiga, yanapiga ukuta mzima, na ungeanguka wote na si kipande kidogo.

Dhamira na nia ya kuijenga sehemu ya ukuta huo iliyobomoka ipo na ukizingatia kuwa kwa muda huu Hospitali inakabiliwa na ufinyu wa bajeti wa kuendesha Hospitali katika shughuli zake za kila siku, kinachosubiriwa kwa sasa ni upatikanaji wa fedha ambazo zinahitajika katika ujenzi wa ukuta huo.

(b) Mhe. Spika, mfumo wa ujenzi uliopo hauna tatizo na huo unaopendekezwa pia si mbaya ila gharama zake ni kubwa ukizingatia bajeti Mnazi Mmoja inayoipata. Ukuta utajengwa mara tu Mnazi Mmoja itakapopata bajeti ya kutosha ya kujenga itazingatia gharama za ujenzi huo. Lakini kwa sasa hapo palipobomoka pana ulinzi wa askari masaa 24. Kwa hiyo, wizi umedhibitiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ya kusikitisha na ya kuvunja moyo kama huo mzizi wenyewe wa mkungu ulivyo wa kupinda pinda na majibu yake ni ya kupinda pinda. Mheshimiwa saa 11.40 alfajiri hiyo nilikuwa katika eneo hilo na kama Kamati itaniridhia twende tukaangalie huo mzizi wa mkungu uko mbali na

ukuta na sikukuta mlinzi aina yoyote nilivyoingia mimi muda huo. Na huo ukuta sifikirii kama unahitaji bajeti maana yake hata matofali 100 hayafiki.

Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja imekuwa chakavu na hili swali limehusu Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja ambayo inategemewa kuitwa Hospitali ya Rufaa, je, serikali ina mpango gani kujenga paa la ghorofa ya tatu ambapo linavuja hivi sasa na wagonjwa kupata shida wakati huu. Hayo sibahatishi ninazungumza kwa uhakika na kuyajua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ninachoweza kukijibu sasa hivi kinahusiana na ukuta, suala la paa hilo litahitaji swali jengine na niende nikalifanyie kazi. Nilipokuwa nimepita huko kwenda kuangalia ukuta na mimi kwa kumbukumbu yangu ninajua pale mkungu ulikuwepo. Na wakati huo nilipouliza maaskari walikuwepo. Niliambiwa kwamba maaskari wapo masaa 24. Sasa saa 11.00 alfajiri leo tulikuwepo? Kwa hivyo, siwezi nikajibu lolote labda niende nikafatilie nijue, je, ulinzi kweli unakuwepo masaa 24 kama walivyonambia maana saa 11.00 pengine mlinzi kenda msikitini siwezi kujibu. Lakini nilivyoambiwa kwamba mlinzi anakuwepo pale masaa 24. Hicho ndicho tu ninachoweza kusema.

Nam. 8

Msaada wa Umwagiliaji kwa Chuo cha Mafunzo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma)- Aliuliza:-

Kwa kuwa Vyuo vya Mafunzo kupitia wanafunzi na wataalamu wake wamekuwa wakizalisha mazao mengi ya kilimo ikiwemo kilimo cha mpunga na kwa kuwa mashamba yao mengi yakiwemo yale ya Kinumoshi na Langoni ni mazuri kwa uzalishaji wa mpunga, lakini yanahitaji miundombinu ya Umwagiliaji *(Irrigation).*

Je, ni lini serikali yenyewe au kupitia ufadhili itavipatia Vyuo vya Mafunzo hivyo Miundombinu ya umwagiliaji ili Vyuo hivyo viweze kuwa na uzalishaji mkubwa wa mpunga na mazao mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ -Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake na mimi nataka niungane na wenzangu kuwapa pole Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Dr. Sira vifo vya mama zao wazazi, Mungu awalaze mahali pema peponi, *Amin.*

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nimefurahishwa sana na swali la Mhe. Mwakilishi, ambalo lengo lake ni kuona kuwa tunayatumia ipasavyo na kwa ufanisi mkubwa maeneo machache ya kilimo tuliyonayo hapa nchini kwa kuzalisha chakula chetu wenyewe na kupunguza uagiziaji kutoka nje. Mabonde ya Kinumoshi na Langoni ni miongoni mwa mabonde yaliyomo katika *master plan* ya umwagiliaji maji kwa Unguja na Pemba yenye ukubwa wa ekari 8,527 ambayo yameombewa ufadhili kwa washirika wa maendeleo mbali mbali.

Hivyo, chini ya mpango huo mashamba haya yatajengewa miundo mbinu ya kisasa ya umwagiliaji maji na kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula. Kwa muda huu wakati tukisubiri Mpango Mkuu wa Serikali, Chuo cha Mafunzo kimefanya jitihada zifuatazo:-

i) Bonde la Kambi la Langoni tayari limewekewa miundombinu na kilimo cha umwagiliaji maji kimeanza.

ii) Bonde la Kinumoshi tayari michoro ya awali imeshatayarishwa na hatua ya utekelezaji inategemea maelekezo kutoka Wizara ya Kilimo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, Vyuo vya Mafunzo lini vitaanza kutumia teknolojia ya kisasa ya vifaa vya kileo baada ya kutumia jembe la mkono, ili wapate kufanya kazi kwa uzuri zaidi na kupata mafao zaidi na kupata lishe bora kwa wanafunzi wa magereza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Mwakilishi atusubirie kidogo tu hivi sasa tayari tumeshafanya mazungumzo na JKT kupitia Kampuni yake ya SUMA kwa Idara Maalum za SMZ zinazojishughulisha na Kilimo, kuchukua mkopo wa matrekta 15 kwa ajili ya kuendeleza mabonde ya kilimo ya vikosi vyetu vya Idara Maalum.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Je, ni tani ngapi za mpunga zinapatikana kila mwaka.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa hivi sasa sina idadi ya tani ngapi za mpunga

zinazopatikana maana sijaelewa ni kwa Zanzibar nzima au kwa Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri sana ya kuonesha kuwa mwaka huu vikosi vyetu vitazidi kuneemeka kwa mpango ulioweka. Mhe.Waziri, umesema tayari umeshazungumza vizuri na watu wa JKT Suma ili waweze kukuletea matrekta mengi sana kwa njia ya mkopo. Mhe. Waziri, nakumbuka huku nyuma vikosi vyengine pamoja na Wizara fulani hapa sitaki kuitaja walichukua mikopo ya matrekta, je, hii Wizara iliohusika na vikosi wameshalipa deni hata unataka mkopo mwengine.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, waswahili wanasema kila mtu atabeba mzigo wake mwenyewe. Vikosi vyangu ambavyo vimechukua matrekta vimeanza kulipa kwenye SUMA JKT na hayo ambayo tutayakopa tumejipanga vizuri na mpango wa kuweza kulipa baada tu ya kwisha kuyachukua.

Nam. 60

Malipo ya Faini kwa Wanafunzi wa SUZA
Waliochelewa kulipa Ada

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza :-

Mnamo mwezi wa Oktoba, 2013, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar “SUZA” waliochelewa kulipa ada ya mafunzo walitakiwa kulipa faini kwa kuchelewa kwao huko na kwa wale walioshindwa kufanya hivyo hawakupatiwa matokeo yao. Kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ndio lenye mamlaka ya kuidhinisha ukusanyaji wa mapato kwa Taasisi za Serikali.

(a) Je, Mhe. Waziri, maamuzi haya yamefanywa chini ya Sheria na Kanuni ipi.

(b) Pato hili lililoanzishwa na Chuo hiki lilitumika kwa shughuli zipi.

(c) Endapo vyuo vitaendelea na mfumo huo hamuoni kuwa mtawavunja moyo vijana wetu na Taifa kubakia kuwa na vijana wasiokuwa na dira au muelekeo wa maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 60 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo ya utangulizi. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinapata ruzuku kutoka serikalini ambayo haikidhi mahitaji ya Chuo na pia ina vyanzo vyake vya mapato ikiwemo ada ya masomo. Bila ya Chuo kukusanya mapato hayo, uendeshaji wa Chuo Kikuu ambao wa gharama kubwa hauwezi kufikiwa. Ni kweli kwamba wanafunzi waliojiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar waliochelewa kulipa ada ya Chuo walitakiwa kulipa faini na uongozi wa Chuo. Maamuzi hayo yalipitishwa na Kikao cha Bodi cha Chuo Kikuu cha Zanzibar, wanafunzi waliochelewa kulipa ada ya usajili walitakiwa kulipa faini katika kipindi cha wiki mbili kuanzia 3 Oktoba 2013.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kama ifuatavyo:-

a) Maamuzi hayo yamefanywa chini ya kifungu namba 12 (6) ya Kanuni za Taaluma za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar zilizotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali la tarehe 8 Machi 2013 *(Legal notice 19 0f 2013).* Kanuni hizo zimefanywa chini ya kifungu namba 56 (I) ya Sheria nam. 8 ya mwaka 1999 kilichoipa uwezo Mamlaka Baraza la Chuo Kikuu kutunga kanuni zitakazosimamia shughuli za taaluma na mitihani kwa ujumla wake.

   Kifungu nambari 12 (6) cha Kanuni za Taaluma za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Sehemu ya Tatu, Masharti ya kujisajili kinaeleza Mhe. Spika, naomba kunukuu:

   > "Kuchelewa kujisajili kwa mwanafunzi yeyote chuoni, kutalazimika kulipa malipo ya ziada yaani fidia ya shs. 25,000/- isipokuwa itakavyoelezwa vyenginevyo".

   Mhe. Spika, ndani ya kanuni hizi kuchelewa kusajili kwa mwanafunzi maana yake ni kutokamilisha masharti ya usajili ikiwemo kulipa ada ndani ya wiki mbili za mafunzo kwa kila muhula wa masomo.

b) Mapato yaliyopatikana yametumika kwa shughuli za uendeshaji wa Chuo. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinapokea ruzuku kutoka serikalini ambayo inachangia asilimia 60 tu ya gharama na Mhe.

Spika, asilimia 60 hii basi zaidi inakwenda kwenye mishahara ya walimu wetu. Asilimia 40 ya gharama za uendeshaji zinatokana na mapato ya vyanzo vya Chuo, ikiwemo ada ya wanafunzi, malipo ya kazi za ushauri na misaada ya wahisani mbali mbali. Bila ya Chuo kukusanya mapato yake, Chuo hakitoweza kujiendesha kwani fedha za ruzuku ni chache na chuo kinakabiliwa na matumizi makubwa.

c) Mhe. Spika, mfumo huu hauna nia ya kuwakomoa wanafunzi na kuwavunja moyo bali una lengo la kukiwezesha Chuo kutekeleza malengo yake mbali mbali yaliyojipangia na kwa wakati. Kitendo cha usajili wa wanafunzi bila ya kulipa ada za masomo yao kwa wakati kitazorotesha utendaji wa Chuo ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kufundishia, kulipia gharama za umeme, usafiri na maji. Hivyo, Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wazazi, walezi na wanafunzi wenyewe wajitahidi kulipa ada za usajili za watoto wao kwa wakati ili kuepuka kupigwa faini ya kucheleweshe malipo na kusababisha usumbufu wa masomo kwa watoto wao.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Spika kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mimi swali langu ni dogo sana pamoja na majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri, mimi nilikuwa nataka kujua kiwango cha fedha ambazo zilikusanywa kutokana na tozo hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sikumfahamu vizuri Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kama alitaka kujua kuhusu kiwango ambacho tunakusanya cha hii faini ambayo walitozwa wanafunzi au ni kiwango ambacho tunakusanya kwa mwaka kwa wanafunzi wote kutokana na masomo yao sikufahamu. Lakini kama ilikuwa ni hiki cha tozo faini ya asilimia 25. Mhe. Spika, naomba nimletee kwa maandishi kwa sababu hapa sina kiasi ambacho kilikusanywa.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Je, wapo wanafunzi ambao walishindwa kulipa ada na faini hizo na kama wapo ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wapo ambao wameshindwa kulipa hii faini mpaka hivi sasa, lakini kwa busara ya Chuo kwa sababu tunataka wanafunzi wetu wapate elimu, hivi sasa wapo madarasani na tumewawekea utaratibu wa kuzilipa hizo pesa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na

(b). Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Naibu Waziri kwamba lazima Chuo kilipwe ili kiweze kuendesha shughuli zake.

(a) Baada ya kuchukuliwa kwa hatua hiyo wanafunzi kuzuiliwa kupata matokeo yao, chuo walifanya tathmini na utafiti wa kina kujua ni kwa nini wanafunzi walichelewa kulipa fedha hizo.

(b) Iwanpo wanafunzi walichelewa kulipa fedha hizo kwa sababu walichelewa kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Tanzania na Zanzibar kwa nini waadhibiwe wanafunzi badala ya kuadhibiwa wahusika wa bodi za mikopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:
(a) Mhe. Spika, Wizara au Chuo hakikufanya utafiti ni kwa nini wanafunzi walichelewa kulipa ada kwa sababu mwanafunzi akichukuwa fomu pale, anajua utaratibu wote wa malipo ambao ulitakiwa kulipwa.

(b) Mhe. Spika, anasema kama kuchelewa huku ni kutokana na wanafunzi hao kutopata mkopo katika bodi ya mkopo, kwa nini adhabu hiyo iende kwa wanafunzi. Mheshimiwa, utaratibu ambao Wizara ya Elimu unaufanya kwa wanafunzi wake, mwanafunzi ambaye kakubaliwa kupata mkopo ndani ya bodi yetu ya mkopo, basi hata kama bado pesa ile hatujaipata huwa tunawaandikia vyuo kuwaambia kama mwanafunzi fulani atapatiwa mkopo na bodi yetu ya mkopo.

Tunawapelekea barua na hawazuiliwi, huwa wanaendelea na masomo yao kama kawaida na tukizipata pesa zile huwa tunazipeleka kulipia katika vyuo. Lakini inawezekana hawa wanafunzi ambao walizuilika ni wale wanafunzi ambao hawana sifa za kupata mkopo.

Nam. 18

Kupotea kwa Michezo Maarufu Zanzibar

Mhe. Nassor Salim Ali: (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma)- Aliuliza:-

Katika miaka ya nyuma Zanzibar ilitamba sana katika michezo ya ndani kama vile *'Table Tenis'*, 'Vinyoya', 'Dats' na hata mchezo wa Kuogolea. Kwa kuwa kwa sasa michezo hiyo haitambulikani tena hususan na hawa vijana wetu na kizazi kipya.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea michezo hiyo isijulikane tena pamoja na kupoteza umaarufu katika nchi yetu.

(b) Kwa kuwa mazingira ya Zanzibar yanashawishi sana kuwepo kwa mchezo wa kuogelea, ni lini serikali itajenga Bwawa kwa ajili ya kufanyia mashindano ya Kimataifa ya kuogolea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 18 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli Zanzibar miaka ya nyuma ilitamba sana katika michezo ya ndani ikiwa ni pamoja na mchezo wa vinyoya na mpira wa meza kinyume na ilivyokuwa sasa. Sababu kubwa ya kupoteza umaarufu wa michezo hiyo ni kukosekana kwa viwanja vya ndani *(Indoor Stadium)*, vifaa vya michezo hiyo na kutokuwepo mashindano ya kikanda na ya ndani. Wizara yangu kwa kutambua changamoto hizo, imeanzisha jitihada mpya za kufufua michezo hiyo kwa kutafuta wahisani na wafadhili wa kuanzisha ujenzi wa viwanja hivyo. Mhe. Spika, tayari kwa upande wa Pemba ujenzi unaendelea kwa ufadhili wa Serikali ya Japan. Aidha, uamuzi umeshatolewa wa kutumia jengo la Judo lilioko ndani ya Kiwanja cha Amani kwa michezo ya viwanja vya ndani.

Mhe. Spika, Wizara kupitia Baraza la Michezo imewapatia mafunzo ya ualimu na uamuzi wanamichezo wawili wa mchezo wa mpira wa vinyoya *(Badminton)* nchini China ili kusaidia katika kufufua na kuendeleza mchezo huo.

(b) Mhe. Spika, kutokana na Zanzibar kuwa na mazingira mazuri ya mchezo wa kuogelea juhudi za kushawishi maendeleo ya mchezo huo Zanzibar, tayari jitihada za awali zikiwemo za kuandaa michoro kutafuta eneo na kuwaomba wafadhili, zimefanyika kupitia Baraza la Taifa la Michezo kwa mashirikiano na Chama cha Mchezo cha Kuogelea Zanzibar. Tunaimani kubwa kwamba katika siku za hivi karibuni jitihada hizi zitafanikiwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa nia ya Wizara katika kufufua michezo mbali mbali ya zamani. Lakini Mhe. Spika, katika kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kumeandaliwa mchezo wa zamani mchezo wa Nage katika viwanja mbali mbali katika jiji hili la Unguja. Na mchezo huu Mhe. Spika, umependwa sana na umekuwa ukihudhuriwa na wananchi mbali mbali katika kuangalia mchezo huu.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuuendeleza mchezo huu ambao umetokezewa kupendwa na wananchi wengi hapa Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, kwa faida ya Baraza lako, kwa faida ya Wazanzibari na faida ya wanamichezo wote wa Zanzibar timu yetu ya taifa ya Zanzibar ambayo iko kule Nairobi kwa taarifa zilizokuwepo imekwama kule ambayo ilikuwa inashiriki katika mashindano ya *Challenge*, je, Wizara taarifa hizi inazo. Na kama inazo ni juhudi gani zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba timu yetu ile ya taifa inarudi nyumbani salama.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nikushukuru ni kweli kwamba Baraza la Taifa la Michezo limeanza kufufua michezo mbali mbali ambayo ilikuwa inachezwa zamani na mchezo huu wa nage ambao ameutaja nao tunaandaa hivyo.

Kwa hivyo, katika kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi yetu tumeona tuanzie hapo na ni kweli kwamba tuna mipango mingi ambayo itawafanya wapenzi wa mchezo huo waanze kushawishika na kuendelea kuucheza. Kwa hivyo, nadhani kwamba wanamichezo mbali mbali wa mchezo huo tutashirikiana na Baraza la Taifa la Michezo katika kuuendeleza ili kuendeleza burudani ambayo walikuwa nayo zamani.

La pili, ni kweli kwamba timu ya *footbal*l ya Taifa Zanzibar *Heroes* imeenda Nairobi kwa ajili ya Mashindano ya Challenge iko Nairobi haijakwama, imekwenda katika mashindano na mashindano yanaendelea hayajesha. Ingekuwa mashindano yamekwisha timu ingekuwa imesehelea kule ingekuwa imekwama, lakini bado CAFE na CECAFA kwa kushirikiana na KFF ndio wenye jukumu la kuwa na timu kule, bado wanayo wapo hoteli wanahudumiwa kila kitu na ukifika wakati wa kuwarejesha watawarejesha. Wizara na Ubalozi wa Tanzania ulioko Nairobi Kenya, tuko makini kuangalia kwamba maslahi ya vijana wetu wapo salama.

Kwa hivyo, nawambia Wazanzibari kwamba timu yetu ipo pazuri haina matatizo bado nafasi ya kurudi nyumbani wenzetu wa CECAFA ambao ndio wenye jukumu la kuwarejesha pamoja na KFF wakiwa tayari watawarejesha, sisi hawajatwambia kwamba wamekwama.

TAARIFA

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini uhakika tu kwamba timu yetu imekwama na taarifa hizi zimetolewa ndani ya chombo cha habari cha KBC ambacho ni chombo cha habari cha Kenya

kwamba timu ya taifa ya Zanzibar imezuiliwa pale na tatizo liliopo kwamba ni mgogoro kati ya CECAFA na KFF. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kusema kwamba hakuna tatizo hili si kweli tatizo lipo na nadhani angechukua juhudi kufatilia suala hili ili timu yetu irudi nyumbani kwa salama.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, bado nasisitiza kwamba timu yetu haijakwama, timu zote ambazo zimeshiriki mashindano ya *challenge* Nairobi ambazo zimetolewa bado zipo Nairobi chini ya uangalizi wa KFF yaani Federation ya mpira wa miguu ya Kenya na uangalizi wa CECAFA. Sasa wao ndio wenye jukumu la kuzirejesha timu zote ambazo zimeshiriki katika mashindano haya kwao wanakotoka.

Naendelea kusema kwamba wizara pamoja na ubalozi wetu wa Kenya unaliangalia hilo kwa makini, na tunahakikisha kwamba maslahi ya vijana wetu yako salama wakati ukifika wa kurejea nyumbani watarejea kama ilivyopangwa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nitoe pole kwa wenzetu ambao wamefiwa.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Habari na Naibu Waziri wake. Je, wizara na Mhe. Waziri, watakubaliana nami kwamba miongoni mwa kazi zetu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pia na sisi ni kushajihisha michezo ili kwenda sambamba na Sera ya Michezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli moja ya majukumu ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika majimbo yetu ya uchaguzi ni kuraghibisha shughuli za michezo mbali mbali inayochezwa. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanafanya vizuri sana shughuli hii, wameanzisha mashindano ya makombe mbali mbali. Kwa hivyo, wizara inawapongeza sana na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wengine waige mfano wa majimbo mengine, sipendi kuyataja lakini wengi sana bado hawajaanzisha utaratibu huu.

Kwa hivyo, ili tuweze kupata maendeleo mazuri ya michezo mbali mbali katika nchi yetu sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba vipaji ambavyo viko katika majimbo yetu vimeibuliwa na kuwa msingi wa kushinda katika mashindano mbali mbali ya kimataifa.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri wa Habari akijibu maswali yake katika michezo mingine ya ndani na kuogelea,

alisema serikali imeanza kufanya jitihada kwa michezo ya ndani kuzungumza na Uongozi wa Uwanja wa Amani ili michezo hiyo ifanyike, lakini katika upande wa mchezo wa kuogelea amesema kwamba tayari wameshaandaa *proposal* kwa ajili ya michezo hiyo.

Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri, wakati serikali inafanya jitihada za kuandaa maeneo mengine ya michezo ya ndani pamoja na mchezo wa kuogelea anayo habari kwamba Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* upande wa Kusini umeanza kuporomoka na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu.

Je, haoni kwamba kuna haja ya uwanja ule kuzuiwa ili usije kuhatarisha maisha na kuleta vifo kwa wananchi wa nchi hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba sehemu ndogo sana ya ukuta inayozunguka Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* sehemu ya Kusini iliporomoka kwa mvua kubwa zilizonyesha karibuni. Lakini eneo ambalo limebomoka si eneo ambalo linaweza kuhatarisha na kusababisha uwanja ufungwe. *ZFA* ambao hivi sasa ndio wanaoumiliki uwanja ule tumezungumza nao na karibu watafanya marekebisho ya pahala ambapo pamebomoka.

Kwa hivyo, hakuna sababu ya kuendelea kuzuia, na kama ambavyo tuliwahi kuripoti hapa Barazani kwamba serikali imeshatiliana mkataba na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya kufanya matengenezo makubwa Uwanja wa *Mao-Tse-Tung.* Kwa hivyo, tukimaliza Uwanja wa Amaan *Inshaallah* tutahamia Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* nao uendelee kuwa uwanja mkubwa sana wa michezo ambao utacheza michezo mbali mbali ya ndani na nje katika nchi hii.

Nam. 12

Muda wa Kazi Shirika la Bandari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika kipindi cha miaka miwili nyuma Shirika la Bandari liliwahi kufanya kazi zake mpaka usiku, hivi sasa utaratibu huo umesita pamoja na shirika kukosa vifaa vya kufanyia kazi, hali ambayo inapelekea shirika hilo kukosa mapato mengi. Kuna taarifa kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama haijaruhusu utaratibu huo uendelee.

(a) Je, sababu gani za msingi zimepelekea shirika kusita kuendelea na utaratibu wa kufanya kazi za kushusha mizigo hadi usiku na kusababisha kupungua kwa mapato.

(b) Lini Kamati ya Ulinzi na Usalama itakaa na wataalamu kutafuta njia muafaka ya usalama ili utaratibu wa Shirika kufanya kazi zake hadi usiku uendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, Bandari ya Malindi ni miongoni mwa bandari kubwa na zenye kutoa huduma za kimataifa kama vile ilivyo kwa bandari za Dar es Salaam na Mombasa. Katika utekelezaji wa kazi zake hizo, zimegawika katika mafungu mawili ambayo ni huduma za ndani (vyombo vya hapa hapa nchini) na zile meli za nje kwa maana ya huduma za meli za kimataifa.

Kwa upande wa huduma za meli za kimataifa serikali yetu inawajibika kufanya kazi kwa muda wote wa masaa 24 ya siku ili kukidhi haja na hoja ya ushindani na bandari za nchi jirani. Pamoja na changamoto zetu za vifaa bado muda tunaotumia kuhudumia meli hizo ni muafaka na wenye kuridhisha.

Aidha, kwa upande wa meli za ndani napenda kukiri kwamba utaratibu wetu ni kufanya kazi chini ya masaa 24 kwa siku. Hoja hii imezingatiwa zaidi na wenzetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Bandarini. Hata hivyo, tumewasihi na tumewashauri Kamati husika ikae na itafakari upya pindi ikiwa hoja na sababu zao zinaakisi tutaendelea kufuata utaratibu huo, na pindi ikiwa kinyume yake tutaomba tufanye kazi kwa masaa 24 kama ilivyo kwa upande wa huduma za kimataifa. Baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa sasa amri ya kutoshusha mizigo usiku inapaswa kuendelea kutekelezwa kutokana na sababu za kiusalama. Ili kuondosha usumbufu unaotokea kutokana na utaratibu huo, Shirika la Bandari linawasisitiza wenye vyombo kuanza safari zao mapema ili wafike bandarini na kufanya kazi kwa muda uliopangwa, (hadi saa 4 usiku). Kamati husika imekua ikikaa kadri ya ratiba ya vikao

vyake lakini bado imeonelea ipo haja ya kuendelea na maelekezo yake ya kufanya kazi hadi saa 12.00 kwa meli za ndani kama sababu zilizoelezwa.

(b) Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba utaratibu uliopo wa wamiliki wa vyombo vya baharini na Wakurugenzi na Mamlaka za Bandari; utaratibu wao wa kukutana na kujadiliana kwa masuala ya ufungaji wa gati wanaweza pia kujadiliana suala hilo la kuhimizana juu ya muda mzuri na muafaka kwa wamiliki hao kuwasili na vyombo vyao kuweza kupata huduma za upakuzi wa mizigo yao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kutokana na Sekta ya Biashara ya Zanzibar kukua haoni hali ya maendeleo ya Zanzibar kuwa tunakwenda mbele au tunarudi nyuma, wakati miaka miwili hizo kazi zimefanywa bila ya tatizo lolote na mtu kinachomfaa ni chake. Kama sadaka inaanzia nyumbani, itakuwaje leo meli za nje zikapate *priority* kuliko Mzanzibari halisi aliyeko hapa, haoni kuwa ni kinyume na utaratibu.

(b) Ni lini Kamati ya Ulinzi na Usalama itaangalia upya suala hili kwa maendeleo na mustakbali wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika;

(a) Ni kweli kwamba miaka miwili nyuma tulikuwa tunakwenda na utaratibu huu wa kushusha mizigo zaidi ya saa nne za usiku. Lakini kutokana na changamoto na matukio yaliyotokezea ndio pale Kamati ya Ulinzi na Usalama ilipoona ipo haja ya kusitisha utaratibu ule. Na baada ya kusitisha yale matatizo ambayo yalijitokeza kipindi kile tulichokuwa tukifanya kazi zaidi ya saa nne za usiku yameonekana kwamba yamepata ufumbuzi. Sasa nataka kumsihi Mhe. Mwakilishi kwamba hoja yake tumeipokea.

(b) Kwa sababu kwamba kuna utaratibu mzuri wa wamiliki wa vyombo, uongozi wa Bandari kila siku saa nane huwa na utaratibu wa kukutana. Suala hili nimuombe Mhe. Jaku Hashim Ayoub basi awaombe hao wamiliki wa vyombo wanapokwenda kwenye vikao husika na hili walizungumze, ufumbuzi wake utatokana na wale wenyewe ambao wanakwenda *field* na wale ndio wanaokabiliana na zile changamoto zote zinazotokana katika shughuli nzima ya upakuzi na ufungaji wa gati kwa meli zote za mizigo hapa nchini.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Naibu Waziri hili suala wenyewe watu wa Bandari wanalihitaji ndio wakanituma kuleta kwako, mimi nafikiri alichukue na kulifanyia kazi, wako tayari kufanya kazi.

Mhe. Spika: Tunakushukuru, Mhe. Naibu Waziri chukua hilo ulifanyie kazi.

Nam. 10

Ujenzi wa Viwanda vya Minofu ya Samaki

Mhe. Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar imezungukwa na bahari yenye utajiri mkubwa wa samaki ambao kwa kiasi kikubwa wameshindwa kuwanufaisha vilivyo Wazanzibari kutokana na serikali kushindwa kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi. Na kwa kuwa wananchi wa kanda ya ziwa ambao wamezungukwa na *Lake Victoria* lenye utajiri mdogo wa samaki ukilinganisha na bahari ya Hindi, tayari kwa kiasi kikubwa tangu zamani na hadi sasa wanaendelea kuneemeka na samaki kutoka kwenye ziwa hilo kwa kupata ajira kwenye viwanda vya kusindika minofu, sambamba na kwenye viwanda vya kutengeneza vyakula vya wanyama (kuku, ngo'mbe n.k) vinavyotumia mabaki ya samaki yapatikanayo baada ya kutoa minofu.

Je, serikali inashindwa kujenga viwanda vya kusindika minofu ya samaki kwa vile haina uwezo au ni kwa sababu kwamba viwanda hivyo havina faida.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, bado uvuvi wetu unafanyika katika maji ya ndani kwa kutumia vyombo na mitego ya kienyeji na mapato yote ya samaki yanatumiwa na wananchi wenyewe. Haja ya kujenga viwanda vya kusindika minofu ya samaki itaweza kutekelezwa pale tu utaratibu wa kuvua katika Bahari Kuu ambayo ndio kwetu kuna rasilimali nyingi, utapokwenda kwa kasi za kuweza kukabiliana na haja hiyo. Hii inajumuisha upatikanaji wa vyombo vya kuvulia Bahari Kuu, kuwepo kwa wataalamu wa uvuvi wa Bahari Kuu na miundombinu inayohusika na mambo hayo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Kwa kuwa serikali huwataka wananchi wake kuunda vikundi vya ushirika kama vile vya uvuvi na mifugo kwa lengo la kujikwamua kimaisha, lakini bado serikali haijawa tayari kuwasaidia wananchi hao kuwapatia vifaa kama vile boti na nyavu. Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kuwa hii ni kasoro kubwa kwa serikali kwa wananchi wake.

(b) Vile vile, haoni kwamba kuwapatia vifaa vya kuwawezesha wananchi hao kama vile boti za kuweza kuvulia samaki kina kikubwa cha maji ni kukosa utajiri wa samaki tulionao hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba swali lake la (b) alirudie kabla sijajibu maswali yake.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, swali langu la (b) linasema kwamba, haoni kutowapatia vifaa wananchi hao kama vile boti kuwawezesha, na nyavu za kuweza kuvulia kina kikubwa cha maji ambacho kina samaki wengi ni kukosa utajiri wa samaki tulionao hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

(a) Mhe. Spika, tayari serikali imevisaidia vikundi mbali mbali nyavu pamoja na vitu vyote ili kuviwezesha vikundi hivyo. Lakini kwa sasa kutokana na bajeti ilivyokuwa ndogo na hakuna mfadhili, na kama mnavyojua *MACEMP* imekwishamaliza muda wake na serikali haijawa na uwezo, lakini pindi tukipata uwezo au wafadhili wa kuweza kutusaidia tuko tayari kuwasaidia na tutawasaidia kwa karibu zaidi.

(b) Lakini kuweza kuwapatia boti na nyavu za kwendea Bahari Kuu hili ni suala ambalo serikali sasa imelivalia njuga yenyewe na tayari kuweza kununua meli kubwa ili kuwawezesha vijana wetu na kuwapa utaalamu ili kwenda kuvua katika Bahari Kuu. Sio suala dogo la kusema kuwapa wananchi wenyewe vitu vya kuvulia Bahari Kuu, kwanza kunatakiwa utaalamu wa kutosha ili tuweze kwenda huko Bahari Kuu. Serikali ina nia thabiti ya kuwapeleka vijana wale na ikikamilika na utaratibu wake basi tutawapeleka wale vijana ili tuweze kufaidika na bahari yetu kubwa wakati rasilimali tunazo za kutosha.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu nchi hii ni nchi ya visiwa na imezungukwa na bahari ina utajiri mkubwa wa samaki. Kutokana na hali ngumu ya uchumi hivi sasa tunalazimika kila mahala tunapopita tuna madeni tunalipia na tunakusanya kodi, wakati tuna bahari yenye kujaa samaki wa kutosha.

Hivi sasa tunasherehekea miaka 50 tokea Mapinduzi na miaka yote suala hili lipo. Wizara haya ina mpango gani wa kuona kuwa ili kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi itajikita zaidi katika uvuvi wa Bahari Kuu na kujenga hivyo viwanda ili uchumi upatikane na wananchi waweze kufaidika.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, serikali imefikia miaka 50 na tayari ina dhamira kubwa kama nilivyosema katika jibu letu la msingi kuwa huwezi kwenda Bahari Kuu kama hujatimiza miundombinu ya kule. Nataka niseme tu Mhe. Spika, kuwa jana tumetiliana saini na wenzeti wa *JICA* katika kufanya bandari ya meli kubwa za uvuvi. Hivyo basi, serikali imejitahidi kwa sasa na hatua moja tumeshaifikia basi tutakwenda Bahari Kuu sio zaidi ya muda mkubwa sasa ili kuweza kupata meli kwa sababu tayari tumeshapata Bandari.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali langu lenye kifungu a, b na c. Kwa kuwa bahari ya mkondo wa Pemba ina utajiri mkubwa wa samaki aina ya jodari wenye bei kubwa ulimwenguni, na kwa kuwa wavuvi wadogo wadogo wa Pemba mara kwa mara huwa wanaharibiwa mitego yao na meli kubwa zinazovua samaki hao katika bahari yetu.

(a) Je, wizara yake inalijua hilo.
(b) Je meli hizo zinazovua katika bahari yetu zimeruhusiwa au zinaiba maliasili yetu.
(c) Kwa nini wavuvi wetu huwa hawafidiwi wanapoharibiwa mitego yao na hili Mhe. Waziri, haoni kama ndio sababu ya wavuvi wetu kuwa masikini na kutopata uwezo wa kuanzisha viwanda vya samaki nchini mwetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, wizara yangu imepata habari ya kuwa meli kubwa zinaharibu nyavu au vifaa vya wavuvi wadogo wadogo ambao wanakwenda kule, utaratibu tayari umechukuliwa. Lakini mambo ya fidia hiyo tunawashauri sana wavuvi wetu wakate bima. Serikali haina utaratibu wa kutoa fidia hivi sasa, lakini suala hilo tumelichukua na tunalifanyia kazi kwa muda huu.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, awali ya yote natanguliza shukurani kwa Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana hapa kuendelea na kazi za kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar. Aidha Mhe. Spika, nakupongeza na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu lipokee na kujadili Mswada wa Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na hatimaye kuupitisha kuwa sheria kamili.

Mhe. Spika, nikianza na utangulizi Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ina jukumu la kusimamia uratibu wa sera, sheria na miongozo ya serikali yenye lengo na madhumuni ya kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha vijana wa Zanzibar kujiimarisha kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ili waweze kupata maendeleo na ustawi mzuri wa maisha yao.

Kwa mujibu wa takwimu zilizopo vijana wanachukua sehemu kubwa ya idadi ya watu kitaifa na wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya taifa.

Ripoti ya Makadirio ya Idadi ya Watu Tanzania ya mwaka 2011 imeainisha kuwa idadi ya vijana Zanzibar ni 449,586 sawa na asilimia 34.2, ambapo kati yao vijana 219,331 ni wanaume, sawa na asilimia 33.8 na 230,255 ni wanawake sawa na asilimia 34.5.

Mhe. Spika, vijana hawa wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya, maambukizi ya UKIMWI, mimba za umri mdogo, udhalilishaji wa kijinsia na ushirikishwaji mdogo wa masuala muhimu yanayochangia maendeleo yao na taifa kwa ujumla. Kutokana na changamoto hizi kuna umuhimu wa kuwashirikisha vijana katika mipango mbali mbali ya maendeleo ili kukabiliana na changamoto zao.

Mhe. Spika, ingawa kuna taasisi nyingi za kiserikali na zisizo za kiserikali ambazo zinashughulikia masuala ya vijana, lakini bado hakuna chombo au taasisi inazoziunganisha taasisi hizo na kuwa na sauti moja katika kushughulikia masuala na changamoto zinazowakabili vijana. Hivyo,

kuundwa kwa Baraza la Vijana Zanzibar litatatua changamoto hizo na litawaunganisha pamoja na kujenga uzalendo na utaifa miongoni mwa vijana na wadau wa maendeleo ya vijana nchini. Baraza litaloundwa litawaunganisha vijana wote bila ya kujali itikadi zao za kisiasa, kijinsia, kijiografia, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Chimbuko la Mswada

Mhe. Spika, hivi sasa kuna taasisi mbali mbali za vijana ambazo zimeundwa kwa mujibu wa sheria mbali mbali zilizopo. Sheria hizo ni pamoja na sheria zinazosimamia na kusajili asasi za kiserikali, *The Non Government Organization, Act. No. 6* ya mwaka 1965. *Registration of Society Act Cap. 153.* Sheria hizi ziko chini ya usimamizi wa Wizara ya Katiba na Sheria. Sheria inayosimamia na kuandikisha Vyama vya Ushirika ya mwaka 1986 inayosimamiwa na Wizara yetu ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto; chini ya sheria hizi yamejitokeza yafuatayo:-

Kila taasisi iliyoundwa au kujiandikisha ina malengo yake mahsusi badala ya kujumuisha vijana wote. Kumekuwa na mtawanyiko mkubwa wa asasi za vijana na kupelekea ugumu wa kutambulika, kusimamia, kudhibiti na kuratibu shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo vya vijana. Kumekuwa na tabia ya baadhi ya vikundi kuibuka na kutoa matamshi mbali mbali ambayo baadhi yake yanaweza kuhatarisha amani, umoja, mshikamano na maadili ya taifa letu.

Sheria zilizopo hazioneshi mfumo madhubuti wa usimamizi wa masuala ya vijana nchini. Katika ushiriki wa vijana kwenye masuala ya kimataifa kumekuwa na wimbi kubwa la vijana kupitia vikundi vyao kujiwakilisha wenyewe badala ya kuwakilisha hoja za msingi zinazojali maslahi ya taifa.

Mhe. Spika, ni miongoni mwa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015 na malengo makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2010 – 2015, katika kuhakikisha kuwa vijana wanaweza kufikiwa na kuunganishwa kwa pamoja kwa mustakabali wa taifa ili kuwa na kauli moja kwa masuala yanayohusu maslahi ya taifa. Aidha, ni utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana ya Zanzibar ya mwaka 2005 ibara ya 21(b) inayotamka kuwa, Serikali itasimamia uundwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar.

Makubaliano yaliyomo katika mkataba wa kikanda ambao Tanzania imeridhia, mkataba huo ni mkataba wa Vijana wa Afrika, *African Youth Charter* ya mwaka 2006 ambao umeridhiwa mwaka 2012. Mkataba huu unasisitiza nchi wanachama juu ya umuhimu wa kujengea vijana uwezo

ikiwemo kuwa na chombo cha kuwashirikisha katika mchakato wa maendeleo katika jamii.

Umuhimu wa kuwa na mazingira mazuri ya kuwafikia na kuwaunganisha vijana hasa katika mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na mapitio ya hoja zilizotokana na makongamano mbali mbali ya vijana pamoja na vikao vya Baraza lako tukufu.

Madhumuni ya Mswada

Mhe. Spika, Madhumuni ya Mswada huu ni kuwasilishwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar, baraza ambalo litakuwa ni chombo kitachotambulika kisheria kitakachoweza kuwaunganisha na kuhamasisha shughuli zinazofanywa na vijana ndani na nje ya nchi yetu. Aidha, kitakuwa ni chombo ambacho kitawawezesha vijana kuwa na kauli moja katika masuala yanayohusu maslahi ya taifa letu.

Hoja ya kuwa na Baraza

Mhe. Spika, hoja ya kuwa na Baraza ni kuunda chombo cha vijana kitachowaunganisha pamoja katika kutatua changamoto mbali mbali zinazowakabili ili kuleta maendeleo yao na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Kujenga uzalendo na ukaribu baina ya vijana wote wa Zanzibar bila ya kujali dini, itikadi, jinsia na maeneo wanayotoka. Vijana kuwa na msimamo na kauli katika masuala masuala mbali mbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa yanayohusu mustakabali wa maendeleo yao.

Muhtasari wa Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar

Mhe. Spika, mswada huu una sehemu sita kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, inahusu Utangulizi. Sehemu hii inazungumzia uhalali wa kuanza kutumika kwa sheria hii na kutoa tafsiri ya maneno muhimu kwa mujibu wa sheria hii,

Sehemu ya Pili, Baraza la Vijana. Shemu hii inazungumzia uanzishwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar na Uanachama wake,

Sehemu ya Tatu, Malengo, Kazi na Uwezo wa Baraza. Sehemu hii inazungumzia malengo ya Baraza, kazi zake, uwezo wa Baraza na uwezo wa Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya vijana katika uendeshaji wa Baraza hilo,

Sehemu ya Nne, Muundo wa Vyombo vinavyounda Baraza. Sehemu hii inazungumzia muundo wa Baraza na vyombo vyake katika ngazi ya taifa hadi shehia,

Sehemu ya Tano, Usimamizi na Uendeshaji wa Fedha za Baraza. Sehemu hii inazungumzia vyanzo vya fedha za Baraza, mwaka wa fedha, makadirio, ukaguzi wa fedha na uwekaji wa fedha,

Sehemu ya Sita, ambayo ni mengineyo. Sehemu hii inazungumzia kuhusu nembo na muhuri wa Baraza, Uwezo wa Waziri kutunga kanuni za uendeshaji wa Baraza, ukomo wa madaraka, taratibu za mikutano, uchaguzi na upigaji wa kura, akidi ya wajumbe katika mikutano ya Baraza, taratibu za nidhamu, maazimio ya Baraza, usawa na jinsia na uongozi.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waujadili mswada huu na hatimaye kuupitisha kuwa ni sheria. Nawashukuru kwa kunisikiliza. Kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Farida Amour Mohamed (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kusoma hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na mswada wa Sheria ya Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nielekeze sifa zote kwa Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, hivyo hatuna budi kumshukuru kwa kuturuzuku neema ya uhai na kutuwezesha kuwa na afya njema kiasi cha kumudu kukutana tena katika mkutano huu wa 14 kwa malengo na dhamira ile ile ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na mswada wa Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Kamati yetu pia ilifanya kazi ya mashirikiano makubwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, hivyo naomba pia wapokee shukurani hizi kupitia Waziri wao makini kwani bila ya mashirikiano mema kutoka kwao kazi hii isingeweza kufikia lengo.

Mhe. Spika, nitakuwa mchache wa fadhila iwapo nitawakosa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa bidii na umoja wao katika kuifanya kazi hii hadi kufikia leo hii ninawasilisha maoni ya Kamati kwa niaba yao. Nawapongeza sana na nawaomba tuendelee kufanya kazi zetu kwa mashirikiano kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba uniruhusu kuuchambua mswada moja kwa moja. Mhe. Spika, malengo ya kuanzishwa kwa Baraza la Vijana la Zanzibar ni utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana ya Zanzibar ya 2005 ibara ya 21 (b) inayotamka kuwa, "Serikali itasimamia uundaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar ambapo ni miongoni mwa utekelezaji wa malengo makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 2010- 2015 katika kuhakikisha kuwa vijana wanaweza kufikiwa na kuunganishwa kwa pamoja kwa mustakabali wa taifa ili kuwa na kauli moja kwa masuala yanayohusu maslahi ya taifa".

Mhe. Spika, aidha chimbuko la kuanzishwa kwa Baraza la Vijana ni makubaliano yaliomo katika mkataba wa kanda ambao Tanzania imeridhia. Mkataba huo ni mkataba wa vijana wa Afrika *(African Youth Charter 2006)* ambao umeridhiwa mwaka 2012. Mkataba huu unasisitiza nchi wanachama juu ya umuhimu wa kuwajengea vijana uwezo ikiwemo kuwa na chombo cha kuwashirikisha katika michakato ya maendeleo kwenye jamii.

Mhe. Spika, kamati yetu inakubaliana na azma ya kuanzishwa kwa Baraza la Vijana kwani kitakuwa ni chombo cha kujenga uzalendo kwa vijana kitakachowasilisha masuala yao ndani na nje ya nchi kwa kuwajenga vijana kuwa imara kijamii, kiuchumi na kiutamaduni jambo ambalo halikuwepo hapo kabla. Hivyo Kamati yetu inapenda kuipongeza sana serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kuanzisha chombo muhimu kwa ustawi wa vijana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha malengo mahususi ya kuanzishwa kwa Baraza hili katika nchi yetu yanafikiwa, ni vyema serikali ikalipa hadhi na uhuru wa kujiendesha Baraza hili pasi na kuingiliwa katika shughuli zake ili vijana wawe huru katika kujadili na kuimarisha mambo ya msingi yatakayowahusu kitaifa na kimataifa kwa madhumuni yale yale kwa kujenga mustakbali mzuri wa taifa letu, kwani taifa lenye vijana wanaojitambua daima hupiga hatua kubwa ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa Baraza hili litakuwa katika ngazi mbali mbali kuanzia Shehia, Wilaya hadi taifa kwa lengo la kupata uwakilishi wa vijana katika maeneo yote ya Zanzibar, bali kamati yetu inapenda kusisitiza wananchi watakaojiunga na Baraza hili kuwa na sifa zilizoelezwa na sheria hili ili kupata uwakilishi wao ulio bora katika ngazi mbali mbali.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwashajihisha vijana wa Kizanzibari kuitumia fursa hii adhimu kujiunga katika Baraza hili ili kujiimarisha kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine, kamati yangu inaipongeza wizara kuweka kifungu ambacho kitaelezea sababu za kusimamishwa au kuondoshwa kwa mwanachama au kiongozi kwenye Baraza hili ambapo miongoni mwa sababu hizo ni kuwa iwapo mwanachama au kiongozi yeyote atathibitika kufanya shughuli za kisiasa ndani ya Baraza atapoteza sifa ya kuwa mwanachama au kiongozi.

Kamati yetu inaunga mkono suala hili kwani pindi tutakaporuhusu siasa katika Baraza hili tutashindwa kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake. Hivyo, napenda kutoa indhari kwa vijana watakaobahatika kujiunga katika Baraza hili kuwa ni mwiko kuingiza masuala ya ushabiki wa siasa katika chombo hiki.

Mhe. Spika, baada ya kuupitia mswada huo kamati yetu inapendekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuimarisha mswada huo. Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niyaainishe baadhi ya marekebisho kama ifuatavyo:-

Kwanza tukianzia na marekebisho ya kuongeza kwa baadhi ya vifungu Mhe. Spika, kamati yetu imependekeza kuongezwa kwa kifungu cha 4 (5) (h) kitakachosomeka, "Kudhihirisha ushabiki wa siasa ndani ya Baraza".

Sababu za kuongezwa kwa kifungu hiki ni kutoruhusu ushabiki wa kisiasa katika Baraza ambapo pindi wanachama au kiongozi yeyote wa Baraza atakapoenda kinyume matakwa ya kifungu hiki atasita kuwa mwanachama au kiongozi wa Baraza hilo.

Mhe. Spika, aidha kamati yetu imeongeza kijifungu kwenye kifungu cha 12 kinachoelezea sifa za kuchaguliwa kwa Katibu Mtendaji ambaye miongoni mwa sifa hizo ni kuwa na shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya jamii, elimu ya jamii au sheria. Uzoefu katika masuala ya maendeleo ya vijana na sifa nyengine kama tulivyoeleza katika waraka wa marekebisho uliogaiwa kwa Wajumbe wako wote. Madhumuni ya kuingizwa kwa kujifungu hiki ni

kupatikana kwa Katibu Mtendaji atakayekuwa na sifa kwa lengo la kuliongoza Baraza kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, kamati yetu pia imerekebisha kifungu cha 10 (2) (e) ambacho neno "Waziri" linaondoshwa na kuingizwa maneno "Kutoka kwenye mtandao wa Jumuiya zao". Kifungu hiki kimependekezwa hivi ili kuwapa fursa wanajumuiya husika kuwachagua wenyewe Wawakilishi watakaoingia katika mkutano mkuu badala ya Wawakilishi hao kuchaguliwa na Waziri anayesimamia masuala ya vijana ambapo pengine panaweza kutokea hali ya upendeleo katika kuchagua kwake.

Mhe. Spika, kamati yetu pia ilifanya marekebisho ya uchapaji kama yanavyoonekana katika waraka wetu tuliowasilisha kwako na nakala za waraka huo kusambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Kwa msingi huo kwa kujali muda wako Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa waupitie waraka huo ili kuona baadhi ya vifungu ambavyo sikuwahi kuvitolea maelezo hapa.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu hii, ningependa kuwapongeza vijana waliohudhuria katika kamati yetu wakiwa ndio wadau na walengwa wakubwa wa mswada wa sheria hii ambapo miongoni mwao ni *Zanzibar Youth Forum*, Jumuiya ya Umoja wa Vijana CCM, CUF na CHADEMA, Umoja wa Wawakilishi wa Wanawake Zanzibar, Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Al-Fattahi Islamic Production Daawa pamoja na wengineo ambao walitusaidia katika kuuchambua mswada huu muhimu.

Napenda kuwahakikishia kuwa kwa kuanzishwa kwa Baraza hili itakuwa ni njia nzuri ya vijana wa Zanzibar kupiga hatua ya kimaendeleo, kijamii na kiuchumi. Hivyo wajitokeze kujiunga katika Mabaraza yao ya kisheria ambapo sifa zinazoelezwa kwa mswada huo wa sheria.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda niwashukuru kwa mara nyengine tena Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku, na ninaomba kuwataja kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamada Omar	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Farida Amour Mohamed	-	Mjumbe
4. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad	-	Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
6. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
7. Mhe. Abdi Mossi Kombo	-	Mjumbe

8. Ndg. Asha Said Mohamed - Katibu
9. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda kutamka bayana kuwa mimi binafsi kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii tunaunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kabla sijaondoka naomba uniruhusu dakika 2 nitoe maoni yangu binafsi angalau mawili matatu katika kuboresha zaidi mswada huu.

Mhe. Spika, kwa sababu ya dhamira ya Mhe. Rais wa Awamu wa Saba katika kutekeleza agizo hili la kuunda Mabaraza ya Vijana ya Zanzibar, lengo lake ni kuwakusanya vijana wetu wa Kizanzibari katika kujikusanya kutafuta maendeleo kiuchumi, kiutamaduni na kadhalika. Sasa Mhe. Spika, katika mswada huu Mhe. Waziri alipokuwa akiusoma maelekezo yake yote na mengi yalikuwa yakizungumzia kuhusu kutoingizwa mambo ya kisiasa ndani ya mswada huu.

Mhe. Spika, tukumbuke kama katika nchi hii Tanzania, tuseme Zanzibar kwa sababu Baraza ni la vijana wa Zanzibar, sote tuliomo humu na walioko nje, wote ni wanasiasa. Kwa hivyo, mimi nina ombi langu moja kubwa kwa Mhe. Waziri pamoja na Wizara yake. Kwa sababu sisi tumeshaelezwa mengi wana kamati lakini naomba suala hili walichukue kwa umakini sana walipeleke kwa wadau ambao ni vijana hasa katika ngazi za Shehia ambazo kuwa suala hili litaanza, wapewe elimu ili wafahamu na wao kuwa suala hili chombo hiki hakikiundwa kwa sababu ya kisiasa, kimeundwa kwa sababu ya kufanya kazi, kukusanyishwa pamoja vijana wa Zanzibar kwa kutafuta maendeleo ya nchi.

Elimu ni kitu muhimu Mhe. Spika na cha msingi, Zanzibar ni yetu sote Wazanzibari. Kwa hivyo, naomba walishughulikie sana suala hili katika kutoa elimu Mhe. Spika, kwa vijana wetu hasa katika ngazi za Shehia ambapo baadhi ya wakati huwa kunatokezea matatizo.

Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Farida Amour Mohamed, tunakushukuru kwa maoni hayo kwa niaba ya Kamati na pia kwa niaba yako mwenyewe ambapo hatimaye umeunga mkono hoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi leo kuweza kunipa nafasi kuweza kuchangia mswada huu wa Baraza la Vijana ambao wenye mantiki kubwa sana, wenye uelewa mzuri lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri na Katibu wake, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wake, wataalamu wake na wanasheria wake.

Mhe. Spika, kuona hiki kitu kukileta hivi sasa ni wakati ambao ni muafaka na ni wakati mzuri sana, na kwa nini nikasema hivi kwa sababu hivi sasa kuna changamoto mbele huko wa mfumo wa Katiba ambayo imo rasimu hiyo na pengine sisi wenyewe tutakuwa na utengenezaji wa Katiba yetu. Sasa imekuwa uzuri kuleta suala hili ili tukalitengeneza vizuri katika muelekeo wa Katiba yetu tutakapokuja kukaa kitako.

Mhe. Spika, niingie sasa katika Katiba ya Zanzibar kwenye ukurasa wa 3 ambapo unaosema kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake kifungu nambari 5 ambacho Mhe. Waziri humu nacho alikitumia hicho. Mhe. Spika, kuna kipindi fulani mimi nilizungumza suala hili la kuwatafutia haki zao Wazanzibari hasa vijana katika shughuli za kazi, ilikuwa na mzozo mkubwa sana, lakini kumbe Mhe. Waziri, alinifahamu nilikuwa na mantiki gani na hivi ndivyo tunavyopenda Mhe. Spika, kwa sababu wengine tunapozungumza hapa Mawaziri watatutafsiri kwa nia nzuri na kuweza kuleta kitu ambacho kitakachoweza kutusaidia.

Leo Mhe. Spika, amenionesha tena hapa ukurasa wake wa mwanzo kabisa, anasema Mzanzibari ina maana sawa alivyoelezwa katika sheria ya Mzanzibari Nam. 5 na ndio hii niliyoinukuu hapa.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo suala la kuundwa Baraza la Vijana asilimia mia kwa mia. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusu vijana kuwatafutia haki zao lakini niseme kwamba nimshukuru sana Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman, *wallahi* anajitahidi sana na yeye kufungua kampuni ambazo zinawashajihisha vijana kuwatafutia ajira za ndani na za nje. Hili nimpongeze sana.

Hivi karibuni kafungua kampuni moja *GSA Agency Company* ambayo inayoshughulikia na masuala ambayo ya kusafirisha vijana wetu na kuwasaidia ajira za nje na ndani kwa mujibu wa taratibu na sheria zote zinazohusiana na wizara yake inatekeleza wajibu huo.

Nalo hili nimshukuru Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman, Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee na suala hilo hilo la kuwatafutia vijana ajira ili waondokane na umaskini. Lakini nikiingia katika mswada huu Mhe. Spika, jinsi ambavyo ulivyopambwa vizuri sana na wanasheria hawa na kutuelekeza jinsi gani hawa

vijana wenyewe wanavyotaka kuanzishwa na kuweza kutafutwa wapi watapatikana. Mimi nakubaliana nalo.

Tunaanzia na sheria, mimi hilo sina tatizo nalo, kwa sababu sheria ndio inayowajua wale vijana wenye akili zao timamu. Kwa sababu hili Baraza si la mchezo, hili Baraza linatunga sheria, linajulikana kimataifa, sio tutajulikana hapa tu hata kimataifa watakuwa na uwezo inavyoonesha kwa mujibu wa sheria hii, Baraza hili litakuwa na uwezo wa kutafuta *funds* katika nchi za madola, ndio mantiki yake ilivyo. Na ndio maana tukaona tukipitisha sheria hiyo.

Sasa sheria hiyo mimi nakubaliana nayo lazima tunaanzia sheria, hilo mumeliotea ndoto hata nilikuwa nataka kukwambieni hapo mwanzo mukianzisha suala hili nendeni kwenye sheria, lakini kumbe wenyewe mumeona wataalamu wako wameona hili suala kuwa ndio huko kuliko *foundation* yenyewe. Lakini sasa tuwe na utaratibu. Utaratibu wangu ninachoomba ni hivi, unajua kunako neema siku zote lazima mambo mengine yatajitokeza.

Tusiwape tena Masheha wetu wakaona hii ndio ulaji, wakatuharibia zile sifa, kabisa hili lazima tuseme ukweli kwa sababu Masheha wengine wakishaona vitu kama hivi ataanzisha yeye atawaambia njoo nikujazishe fomu lakini fomu utoe pesa. Tuangalie sana hapa wanasheria, tuangalie hiki kitu ambacho hapa kidogo kisiwe na tatizo ili tukaliondolea ile dhana yote ikawa nzuri ikaharibiwa na mtu huyu mmoja.

Naomba sana tuwe na utaratibu maafisa ambao waliomo katika wilaya au mikoa tayari washuke chini kwa kufuatilia haya masuala ya utaratibu wake mpaka unakamilika. Naomba hilo. Lakini Mwenyekiti hapa alisema jambo kuwa elimu, mimi nasema kuwa ni semina. Hizi semina mimi naomba ziwe mara kwa mara, kwa sababu gani, unajua tuna watu wengi hawajui hili Baraza likoje. Maana yake ni lazima tuseme ukweli hali halisi. Mimi nitajua lakini kijana hajui nini maana ya Baraza. Tutakuja kukosa watu waliokuwa wazuri, tutakuja kuchukua watu watatuletea fujo kwenye Baraza letu.

Kwa sababu ninavyofahamu mimi Baraza ni muundo ambao tayari vijana watakuwa na sehemu ya kuweza kupeleka malalamiko, mawazo yao ili serikali iweze kuyatekeleza. Na ni kweli mawazo hivi sasa vijana hawana pa kuyapeleka wanatupa sisi hapa lakini tukishasema kila mtu *brief case* anaondoka, utekelekezaji wake unakuwa ni mdogo.

Lakini sasa Baraza chombo kitakuwa kina sheria, kitakuwa kina nguvu, kitakuwa na uongozi wake kamili. Lakini zaidi na wizara itakuwepo pale.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Spika, twende katika mfumo ambao huo nilioutoa mawazo yangu kuwa lazima tuwe *serious* nalo, na kupitia katika Masheha wetu ili kuweza kufanyisha hili suala liwe kwa uzuri sana.

Kwa sababu leo vijana Mhe. Spika, wanasikia hivi kuwa sasa hivi tunaanza kuwatungia Baraza lao, lakini wanajiuliza huko nje, Baraza letu litakuwa vipi, tutajulikana vipi, tutaliunda vipi, tutakwenda vipi, hawajui. Lakini nafikiri Wizara itaandaa mfumo mzuri ili watu waweze kufahamu na nini tunachokwenda nacho.

Nikiendelea katika ukurasa wa 343 Mhe. Spika, lakini vile vile uzuri wake kuwa Baraza hilo hilo litakuwa na uwezo wa kushtaki na kushtakiwa, Mimi kifungu hiki nakubaliana nacho Mhe. Waziri. Nilisema watakuwa na uwezo wa kumiliki na kununua, ndio haya tuliyoyazungumza kuwa uwezo huo utakuwepo wa kuweza kumiliki na kununua lakini tuwe wakweli katika kuwatekelezea hii sheria ambayo tunayoifanya.

Mhe. Spika, hivi sasa vijana wetu hawana kazi, vijana wengi hawana ardhi hivi sasa za kufanyia kazi zao. Mhe. Spika, Mhe. Waziri nashukuru sana kwamba upo karibu na Mhe. Waziri wa Ardhi hapo. Nimshukuru na yeye kwa jitihada zake kusema la ukweli *alhamdulillah* Mwenyezi Mungu anajitahidi sana kuzirejesha zile ardhi ambazo zilizokuwa mikononi mwa watu kuwatafutia njia vijana kuwamilikisha. Mimi hilo ninafurahi sana na *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie aendelee hivyo hivyo, kwa sababu kijana kama hana ardhi hana maendeleo.

Sasa kifungu hiki kinaeleza kuwa waweze kuwa na vitu kama hivyo na waweze kuuza katika misingi ambayo inayotakiwa kwa mujibu wa sheria. Hilo nashukuru sana Mheshimiwa mujitahidi sana katika masuala kama hayo, lakini mfumo ambao maalum hivi sasa wa vijana wa Kizanzibari kupata kazi haupo. Lakini mfumo huu unaokwenda nao wa Baraza lako Mhe. Spika, kutakuwa na vijana sasa *alhamdulillah* kazi zitapatikana, kazi Wazanzibari jamani hawana la kufanya na sio kwa kuwa hawana, hakukuwa na chombo cha kuweza kuwasimamia.

Lakini leo chombo kipo kwa mujibu wa Katiba hii inayosema kuwa nani Mzanzibari atajulikana humu Katiba hii, na Baraza hili linasema nani Mzanzibari ataonekana humu.

Mhe. Spika, Wajumbe hawa watapitisha haraka mswada huu, sina wasiwasi nao kabisa. Na kwa sababu hivi sasa Mhe. Spika, vijana wetu hivi sasa wengi wamesoma wameamka katika kitaaluma ya kusoma lakini wanapokwenda katika mfumo wa kutafuta kazi kupewa kazi Mhe. Spika, wanakuwa hawapati

zile kazi inavyotakiwa. Wanakwenda vizuri, zile shahada zinazotakiwa Mhe. Spika, wanakuwa nazo vizuri lakini kama huna uenyeji, huna mkubwa hawana kazi. Hilo kwa kweli lazima tuliseme.

Lakini leo ninawaambia vijana wasishughulikie sasa mkubwa watakuwa naye ni Baraza, ni Baraza lao ambalo ndilo litakalopeleka malalamiko yao, litakwenda kutafuta ajira kupitia Baraza lao. Vijana hivi sasa wasishughulike.Waziri mama hivi sasa ameamua na ni mlezi mwenyewe hasa kwa mujibu wa sheria, kwa sababu mama ndiye mwenye huruma, ameona yeye kwa makusudi kuwa kama sitokuwa na Baraza mimi vijana wangu wataumia, kwa sababu hivi sasa Mhe. Spika, hali ni ngumu, ubakaji umezidi, vitoto vidogo vinabakwa, tena ni wanaume wanabakwa.

Mhe. Spika, ningekuwa mimi ni Rais wa Zanzibar ningesema wapigwe sindano ya kufa, kwa sababu vitoto vidogo vinapata taabu sana. Lakini hili Baraza ndio shughuli zake hizo, zitaharakisha hizi kesi kwenda na kumshtaki mtu, ndio ninavyofahamu mimi ndio mfumo wa Baraza hili, litawasaidia kusukuma mbele kesi ambazo kwa mujibu wa sheria zinatakiwa ziende mbele.

Mhe. Spika, nikiendelea ukurasa wa 344 kuhusu Kazi za Baraza. Kazi za Baraza zinaainishwa hapa vizuri tu, zinasema kuwa, kushauri na kushauriana na Wizara katika masuala yote ya vijana ya mipango na maendeleo. Kushajihisha upatikanaji wa haki za vijana, kupanua wigo wa uendelevu wa maendeleo kujumuisha sera, kanuni na sheria, mambo ya kimsingi na mipango.

Juzi tulikuwa tunasomeshwa hapo jinsi gani mambo ya kutengeneza sera, jinsi gani mambo ya sheria. Tunashukuru sana nao *UNDP* ndugu zetu hawa na wao wanatusaidia sana kutupatia taaluma kwa kuelelewa na kufahamu. Mimi nilikuwa sijui nini maana ya sera, nilikuwa sijui sera ipi na sheria ipi, ipi inayotakiwa mwanzo na ipi inayotakiwa mwisho na ipi itakuwa ni sheria, nilikuwa sijui.

Kumbe sheria ni sheria, sera ni utengenezaji wigo wa kupanua mambo ya kutekeleza ili yafanyike yaingie kwenye sheria, kwa nilivyofahamu mimi taaluma yangu mwalimu wangu alivyonisomesha. Sasa hapa wasiwasi wangu upo mmoja, ninatoa tahadhari. Vijana wana akili sana, wana muono sana, lakini jee wizara itakuwa tayari kupokea ushauri kwa vijana, kuelekeza na kupanga mpango wa sera nzuri ili zitakazowasaidia wao katika maisha yao na kutengeneza sheria ile sera ambayo ili iweze kuwa ni halali, sasa mimi hapo ndio wasiwasi wangu utakuwa upo hapo.

Mambo mengi sana tunajaribu kuyatengeneza Mhe. Spika, ni mambo mengi sana hapa tunaunda kwa mujibu wa sheria lakini utekelezaji wake upo finyu kabisa. Hili ukweli tuseme, hasa kutokana na sheria hii ya vijana ya kazi. Naomba Mhe. Waziri, wangu Mwalim Haroun Ali Suleiman hapo aendelee na hii sheria ya kuwaelimisha wananchi, sheria ya kazi, utaratibu wa kazi. Wimbi kubwa hivi sasa wafanyakazi vijana wanafukuzwa tu ovyo ovyo bila ya sababu yoyote Mhe. Spika.

Anapelekwa mtu kazini hapewi mkataba mtu anafanya kazi kwa muda wa miaka kumi na nane, hana mkataba anatafutiwa sababu ya kijinga tu halafu anafukuzwa. Mhe. Spika, hili linatia huruma sana. Mhe. Spika, vijana sasa hivi haki zao ni finyu katika ardhi yao kupata kazi, inakuwa ni finyu sana kabisa, nalo hili bado halijaangaliwa, na ndio maana nikasema tunatunga sheria nyingi lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo.

Leo ukienda hapo mahotelini Wakenya wamejaa kibao kabisa, watu wanakuja kujifundisha kudhalilisha watu hapa. Sisi tumeondoa ukoloni mambo leo, tumeshawaondoa *long time ago* Mhe. Spika, sasa tunajitanafasi wenyewe, lakini watu hivi sasa wanatafuta njia ya kuja kuturudisha nyuma wanatunyanyasa kabisa kwenye ardhi yetu, vijana wanadhalilishwa.

Mhe. Spika, hili tumeshasema sana kuwa vijana wanadhalilishwa. Kila siku mimi siku moja ninapokea kesi tatu. Ninashukuru ...

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ninashukuru sana nakwenda katika wizara husika inafanya kazi lakini bado ipo *slow*, inafanya kazi sisemi kama haifanyi kazi. Kesi mbili nimeshawapelekea, moja ipo kwenye *line* na nyengine ipo njiani wanasheria watakwenda kuikamilisha.

Mhe. Spika, hili tunaomba sana, namuomba sana Mhe. Haroun Ali Suleiman na Mhe. Waziri, mama kuwa hiki kitu ambacho hivi sasa tunachokitunga hapa sheria basi *wallahi* kifuate mkondo, kifanye kazi kwa mujibu wa taratibu tuliokubaliana hapa.

Mhe. Spika, dakika 5 hizi mimi nitazimaliza hapana tatizo lolote.

Mhe. Spika, ukurasa wa 345 "Kusaidia kushajihisha vikundi vyenye maslahi ya maendeleo na vijana katika kuanzisha mafunzo kwa vijana na mipango ya maendeleo, utafiti, kuunga mkono mipango inayoshuhudiwa na vijana, kukuza kutumia..."

Mhe. Spika, mimi ninakubaliana nacho ni kweli hivi vijana, serikali haina ajira. Kuwashajihisha vijana katika vikundi ni moja katika ajira, lakini tuwafundishe jinsi ya kutengeneza *write up project* ili waweze kutafuta kazi nchi za nje, nalo hili linakosekana. Mzungu huwezi kumwambia tu bila ya kumfahamisha, kwa sababu ile *write up project* yenyewe ina mambo mengi mle ya yule mzungu kukuona kwamba kumbe kweli unataka kufuga kuku au kweli unataka kufanya jambo fulani, afahamu hivyo.

Sasa nalo hili tuna ukosefu wa kupata taaluma kwa vijana wetu, tunawakusanya vikundi, serikali haina *funds* za kuwapa, *funds* zao ni ndogo sana. Lakini tukiwafundisha jinsi ya kuandika, naamini mimi baada ya miaka miwili au mitatu hapa vijana wote watakuwa ni matajiri. Tukikubaliana na tukiwa na moyo mmoja kwa ushujaa tukajitolea, tukasema sasa vijana umaskini basi. Hilo mimi nakubaliana nalo.

Nimalizie Mhe. Spika, katika ukurasa huo huo chini hapo, kwenye kifungu cha 7, ambacho kinasema kwamba;

Kifungu cha 7

> "Katika kuhakikisha kuwa linafanyakazi zake kiufanisi kwa mujibu wa sheria hii, Baraza litakuwa na uwezo wa kuajiri watendaji wa baraza kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma, sheria nyengine yoyote ambayo inahusiana na hayo"

Hapa kidogo naomba Mhe. Waziri unisaidie Kiswahili kidogo kimenichanganya, kwa sababu Kiswahili changu mimi ni cha Kaskazini.

Naomba nirejee tena Mhe. Spika, kifungu (a)

Kifungu (a)

> "Kuajiri watendaji wa Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, au sheria nyengine yoyote inayohusiana na hayo katika Zanzibar"

Sasa wataajiriwa wale watu wa Baraza wenyewe, wataajiriwa wapi, mimi sioni wataajiriwa kutoka sehemu gani, kwenye wizara yenyewe husika au kwenye mawizara na ni hawa hawa watakuwa ni wajumbe wa Baraza tu ndio watakaoajiriwa, hao wengine wakose ajira. Naomba Mhe. Waziri, suala hili unisaidie sana ili niweze kuunga mkono zaidi. Maana yake nimeshakuunga mkono tayari asilimia mia kwa mia sina wasi wasi nao kabisa. Lakini nizidi kukuunga mkono kwa kifungu hiki nisije nikapiga buti na sitaki kupiga buti..

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri, tahadhari yangu iko hapa kwa kumalizia. Mhe. Spika, hali ni ngumu sana ya vijana. Hali hii inapelekea kwenda kula unga, na kuwa wizi. Lakini naamini chombo hiki ambacho tutakipitisha hapa na hawa waheshimiwa wenzetu waliokuwepo hapa mamufti wengine humu, basi iwe ndio sumu ya kuondoa tatizo hili kwa vijana waondokane na wizi, na kula unga na iwe ndio sababu kubwa sasa hivi ya kuondokana na umaskini. Vijana wetu wawe katika hali ya utajiri katika nchi yao, waweze kula matunda ya nchi yao ambayo tunakwenda nayo sasa hivi ya sherehe yetu ya miaka 50, matunda ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono, ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na tukaweza kukutana tena hapa. Pili, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Vile vile, Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapa pole wale wenzetu ambao wameondokewa na wazazi wao. Pia, niwatakie wale wenzetu ambao ni wagonjwa Mwenyezi Mungu awape nafuu na tuweze kuendelea nao, akiwemo Mwakilishi wangu wa Jimbo la Wawi.

Mhe. Spika, nataka nianze kutoa mchango wangu mdogo sana kwa sababu hali yangu hainiruhusu leo, lakini kwa sababu kuna mambo yamenikereketa katika huu mswada nimeona nitumie japo dakika mbili kutoa mchango wangu. Nitaanza mchango wangu katika tafsiri kwenye ukurasa wa 342.

Mhe. Spika, tafsiri ya mualikwa kiofisi inahitaji kurekebishwa, kwa sababu kwenye mswada inatafsiriwa kama ni wageni waalikwa. Ninachokusudia hapa Mhe. Spika, mualikwa wa kiofisi ni mmoja, lakini tafsiri imesema kama ni wageni waalikwa ambao ni wengi. Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, panataka kufanyiwa marekebisho.

Jengine ni kuhusu tafsiri ya kiongozi mtendaji wa chama cha siasa kuwa na maana ya mtu mwenye nafasi ya uongozi wowote katika chama cha siasa. Hii Mhe. Spika, pia inahitaji kutazamwa upya. Kwa maoni yangu kiongozi mtendaji anatakiwa awe na dhamana ya utendaji katika kile chama, ukisema ni kiongozi yeyote, kuna nafasi za uongozi lakini sio za utendaji katika chama. Kwa hivyo, hapa naomba pafanyiwe marekebisho. Ikiwa tunahitaji iendane na tafsiri hii basi neno utendaji liondolewe.

Mhe. Spika, kabla ya kuendelea mbele zaidi naomba nieleze kwamba nimeutazama sana mswada huu katika sehemu ya madhumuni na sababu, kwenye ukurasa wa 354. Kwa kweli Mhe. Spika, mimi nimeshindwa kufahamu madhumuni na sababu kwa nini serikali imeleta mswada huu na

maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri hayana ufafanuzi mzuri. Kwasababu Mhe. Spika, iliyotolewa hapa ni kuwapa nafasi vijana kujikusanya pamoja. Ikiwa hiyo ndio sababu basi namuomba Mhe. Waziri, atueleze ni lini serikali italeta mswada hapa wa Baraza la wanawake, au la wa Baraza la wazee na watoto.

Kwa sababu Mhe. Spika, kila kundi katika rika linahitaji kukaa pamoja, sasa kwa nini serikali ikiwa imeona hiyo ni sababu ilete mswada wa Baraza la vijana tu, wakati na wengine wanahitaji kukaa pamoja. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupe sababu au atuambie hasa wamekusudia nini hapa.

Vile vile, Mhe. Spika, mimi hapa nina hofu na uanzishwaji wa Baraza hili la vijana kuja kutumika kwa malengo ya kisiasa. Mhe. Waziri, tumemsikia katika uwasilishaji wake, amesema kwamba hakutakiwi siasa. Lakini yeye aliyekuwepo sasa hivi ni waziri makini na hii sheria haitotumika akiwepo yeye tu. Kutakuja kila aina ya mawaziri na sheria hii itatumika. Je, tukijakupata waziri aliyekuwa sio makini, hatuoni Baraza hili linaweza likajakutumika kisiasa. Mhe. Spika, hapa panahitaji mazingatio makubwa.

Mhe. Spika, vile vile tukienda katika kifungu cha 4(1), ukurasa wa 343, kinaeleza kuhusu wanachama kupitia mabaraza yao ya vijana kwenye Shehia. Hapa Mhe. Spika, naomba nipatiwe ufafanuzi pataanzwaje. Hizo fomu zitatolewa na nani, au mratibu wa shughuli hizo atakuwa ni Sheha. Ikiwa Mhe. Spika, mabaraza haya yakianza kuratibiwa na Masheha basi nadhani mambo yatakuwa mazito na ndio nikasema panahitaji ufafanuzi mkubwa. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna mambo ambayo yameanzwa na Masheha na kila siku tukisimama humu Barazani ni kelele. Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, naomba paangaliwe.

Mhe. Spika, suala jengine ni kifungu cha 4(3). Mwanachama wa Baraza atakuwa na haki na wajibu ufuatao:-

Kifungu cha 4(3)(e)

"Kutunza siri za taarifa zote za siri za Baraza"

Sasa hapa Mhe. Spika, nataka Mhe. Waziri, anifahamishe, hili Baraza litakuwa na siri gani. Kwa sababu mimi nilitegemea Baraza hili litakuwa na uwazi na shughuli nyingi zitakazoendeshwa. Mhe. Spika, mara nyingi shughuli za uwazi huwa zinafanikiwa, kuliko zile zilizokuwa na mambo ya siri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atueleze hiyo siri iliopo ni siri gani, ambayo mwanachama lazima aifiche.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6(h) kwenye ukurasa wa 345 kinahitaji ufafanuzi zaidi, naomba nikinukuuu:

Kifungu cha 6(h)

> "Kuazisha, kuendesha na kusimamia miradi yenye na isiyoletea faida katika kuunga mkono maendeleo ya vijana kama inavyoonekanwa inafaa"

Mhe. Spika, tumezoea hata sisi wananchi huko mitaani na kwenye vikundi, tukianzisha miradi tunategemea faida na lengo la kuanzisha mradi ni faida. Lakini leo hapa tumeelezwa kama kuanzisha, kuendesha na kusimamia miradi isiyoleta faida kwa vijana. Mimi Mhe. Spika, kifungu hiki sikikubali, kwa sababu hao vijana wanaotusikiliza wataona hatuna imani na wao tuliowaanzishia Baraza hili la Vijana. Sasa kifungu hiki ni cha nini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atueleze hapa kakusudia nini, hiyo miradi isiyo na faida ni miradi ipi na kwa nini waanzishe miradi hiyo, si bora wakae wawe hawana miradi kuliko kuanzisha miradi isiyo na faida. Au hapa Mhe. Waziri, kategemea atakachokichuma ni nini hasa, kwa sababu ikiwa unaanzisha miradi iliyokuwa haina faida, pengine lengo lake ni kuanzisha mradi ulete hasara. Hapa namuomba Mhe. Waziri, atupe ufafanuzi.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 346 kifungu cha 10(2) kumetajwa ngazi za mkoa, lakini hakuna ufafanuzi wa kuanzishwa Baraza la Vijana la Mkoa. Sasa ikiwa sheria haitaji kuanzishwa Baraza la Vijana la Mkoa, Mwenyekiti wa Vijana, Katibu wa Vijana na wananchama watatu wa vijana wa mkoa watapatikana kwa taratibu gani. Naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, pia, katika kifungu cha 12(3) kimetaja wakuu wote wa idara. Lakini katika sheria hii hazikutajwa hizo idara na wala hatukuona chombo kilichopewa mamlaka ya kuanzisha hizo idara na hao wakuu wa idara. Sasa namuomba Mhe. Waziri, aniambie hizi idara zitaanzishwa na nani na katika sheria hatukuona, au hao wakuu wa idara watateuliwa na nani. Hapa namuomba Mhe. Waziri, pia, anipe ufafanuzi.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, katika mswada huu kumetajwa nafasi mbali mbali za uongozi, katika ngazi ya taifa, wilaya, shehia wakiwemo wenyeviti wa vijana taifa, wilaya, shehia na makamo wenyeviti. Pia kuna katibu mtendaji ambaye atateuliwa na Rais. Lakini Mhe. Spika, hawa wote wametajwa na hawakuekewa sifa zao, ambapo Baraza hili la vijana taifa linakuwa ofisi ya umma kwa sheria.

Mhe.Spika, ni vizuri wangewekewa sifa zao, hii kwa kweli ni kasoro kubwa ambayo nadhani inahitaji kuekewa utaratibu, viongozi hawa wa Baraza elimu yao iwe ni kiwango gani, lakini kwa kuachia hivi hivi tu Mhe. Spika, nadhani hatutopata ufanisi katika suala hili.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaomba nipate maelezo ya Mhe. Waziri ili niweze kuupitisha mswada huu kama wenzangu. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya kuchangia machache kuhusu mswada ulio mbele yetu. Mhe. Spika, ingawa mbele yangu hakuna saa, lakini nitatumia muda mfupi na nitakuwa nikigeuka nyuma kutazama wakati ili nisitumie wakati mwingi sana.

Mhe. Spika, kwanza nianze kukushukuru wewe, waziri pamoja na watendaji wake wote. Pia nirudi katika taarifa yako uliomsifu sana kiongozi muanzilishi wa taifa la Afrika ya Kusini, Mzee Nelson Mandela ambaye alifariki wiki iliyopita, kwa ujasiri wake alioufanya kuikomboa nchi yake na baada ya ukombozi yeye kwa kuwa lengo lake ni kuikomboa basi aliongoza kwa awamu moja tu.

Kwa hivyo, ningewaomba na viongozi wengine wa Afrika na hasa hapa kwetu Zanzibar wafuate mfano wa Marehemu Mzee Nelson Mandela, iwe lengo lao ni kukomboa zaidi kuliko kuongoza kwa muda mrefu. Mzee Nelson Mandela alionesha mfano mzuri katika viongozi wote wa Afrika na kutokana mazuri hayo hivi sasa takriban dunia nzima iko Afrika ya Kusini kushiriki katika mazishi yake.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, nichangie mswada huu ambao ni wa vijana. Kijana katafsiriwa kuwa ni kuanzia umri wa miaka 15 hadi 35 ndio kijana na ndio anayetakiwa kuwemo katika uundaji wa mabaraza ya vijana. Kwa kuwa kashirikishwa katika mswada sharti kuwa ni kijana, na uongozi wowote katika nchi hii ni lazima mtu awe ni Mzanzibari na huwi Mzanzibari Mkaazi kama huna kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Je, ina maana huyo kijana wa miaka 15 tutampa huu Uzanzibari Ukaazi ili aweze kuwa katika Baraza la Vijana. Hapa kwa maoni yangu nahisi kuwa kijana wa miaka 15 hadi 17 asiingizwe kwa sababu kisheria ya nchi hawezi kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari. Mhe. Spika, wote wenye umri wangu na wako, kama hana kitambulisho bado hajawa ni Mkaazi, na Wazanzibari wote tuliokuwa na *ZID* bado sio petu sisi ni wakaazi tu, sijui kwetu ni wapi.

Mhe. Spika, nije katika huu muundo wa hili Baraza, limeanza juu, limekuja kati na linakuja chini kabisa. Kama tuseme mswada huu ningeutunga mimi

ningeanza kwenye shehia, jimbo, wilaya, mkoa, na taifa. Lakini waliotunga wameanza juu kuja chini, kumbe kwenye kujenga ni lazima uanzie kutoka chini na sio kuanzia juu. Utakuwa ni fundi wa ajabu kujenga nyumba tofali la mwanzo likaanza juu, na mswada huu ndio ulivyo.Halafu hapa katikati pana uwazi, hapana jimbo, hapana mkoa.

Kwa hivyo, Baraza hili litakuwa linaning'inia tu, muundo wake kwa maoni yangu haukukamilika. Lakini huko mbele kuna wajumbe ambao wanatajwa katika mkoa, wametoka wapi wakati ambapo katika muundo wenyewe mkoa haupo. Mhe. Spika, kutokana na hayo ningeomba ufanyiwe marekebisho ama wale wajumbe wanaoingia kwa mkoa waondolewe au katika muundo mkoa uingizwe.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 344 kwenye sehemu ya kusita kuwa mwanachama au kiongozi, katika kifungu cha 4(5)(c) kwa kiongozi mtendaji katika chama cha siasa.

Mhe. Spika, Wazanzibari walio wengi au tuseme ni wote ama kwa dhahiri au kwa siri zao ni wanachama wa chama fulani, hakuna Mzanzibari yeyote atakayekuambia mimi sio mwanachama, hapana. Chama anacho na ni viongozi wa vyama.

Mhe. Spika, ilivyokuja sheria ya vyama vya siasa na wakatakiwa wafanyakazi wasiwe viongozi katika vyama vya siasa, ile sheria kuna watu iliwabana walipotambulikana kuwa wao ni wafanyakazi lakini pia ni viongozi katika vyama vya siasa, walitimuliwa kazini. Ingawaje kuna watu walikuwa ni viongozi katika vyama vya siasa na pia ni viongozi katika serikali, hawa waliendelea kujitanua.

Kwa hivyo, nina hofu na sheria hii isijekuwa kama ile ya vyama vya siasa. Iwe kuna vijana fulani tu ukionekana wewe msimamo wako wa kisiasa uko hivi, akaambiwa amepoteza sifa, lakini mwengine ni kiongozi katika chama fulani cha siasa yeye ikawa sifa zake bado zipo na akaendelea kuwa kiongozi. Hapa ni lazima tuwe makini sana katika Baraza ambalo tunategemea kulianzisha.

Mhe. Spika, pia ametajwa mtu atapoteza sifa akiwa na tabia mbaya au mwenendo mbaya. Ningeomba nipate ufafanuzi kidogo hii tabia mbaya ni ipi na mwenendo mbaya ni upi. Haina maana kwamba sijui kitu kibaya ni kipi, lakini hapa katika mswada, kwa sababu unataka kuwa sheria, ningependa kujua lile ambalo mswada huu wa sheria utaona kuwa hili ni baya, ni jambo gani, kwa sababu yako mambo ambayo mimi nayahisi ni mabaya, lakini kwa mwengine ni mazuri.

Mhe. Spika, kuna watu wanamuamini vibaya mlevi, kuwa ulevi ni tabia nzuri na kuna wengine wanasema kama sijapata chochote kichwa changu hakifanyi kazi. Lakini kwa muono wangu mimi ulevi ni tabia mbaya.

Mhe. Spika, katika ukurasa huu huu nije katika kifungu cha 5(a) na (c) malengo ya Baraza. Malengo ya Baraza kuwajenga vijana kutambua utaifa wao, hali ya umoja na mashirikiano, kujiheshimu na pia kuifahamu kwa kina jamii kiuchumi, hali halisi, kiutamaduni na upeo wake. Hapa nakusudia kusema jambo moja kidogo, huu utaifa wa Mzanzibari ni upi na ikiwa kama Mzanzibari asili yake awe ni Mtanzania ni upi na wakati ambapo yeye hapa ni mkaazi tu, ana utaifa gani. Kwa hivyo, hapa mimi sijajua utaifa wa kijana wa Zanzibar ni upi, si wa Kitanzania, kwa sababu huu mswada unahusu Zanzibar.

Mhe. Spika, (c) kushajihisha, kujengewa uwezo vijana ili kuwafanya wazalishaji katika jamii. Mhe. Spika, uzalishaji hauji mpaka kwa kufanyakazi ambayo inazalisha. Kwa bahati mbaya kwa muono wangu mimi, serikali inajaribu kuandaa vijana kuzalisha na kujitegemea, lakini hatimae wataanza kusema kumbe hawa watafikia lengo la kujitegemea, basi serikali katika vituo vyao vya kuzalisha ghafla inawatimua.

Mhe. Spika, mimi binafsi zaidi ya Pemba na Unguja sidhani kama kuna nchi popote duniani iliyokuwa kama Zanzibar ambayo inawasumbua, inawadhalilisha vijana wake au watu wake kama sisi hapa. Nasema hili kwa mfano mdogo wa hivi karibuni. Mimi nakaa hapa Chukwani, napanda gari ya Chukwani zamani nilikuwa nateremka Darajani, leo nateremka Kikwajuni.

Kwa mimi kutoka pale mpaka Darajani ninapokwenda ni zoezi, lakini kuna watu ni adhabu, suala hili tunaiomba serikali ilifikirie. Kuna mtu anatoka Bububu anateremshwa kwa Bakharesa, pengine ana pakacha zake za mihogo tunamuadhibu, na serikali inafanya hivi kwa makusudi sio kwa bahati mbaya. Hili kwa kweli hatuoneshi upendo kwa tunaowaongoza. Tunajiona sisi tuna gari zetu, tunaingia mjini tukitoka, hatujali waliokuwa nyuma yetu wakoje. Kumbe hawa tunaowafanyia hivi ndio waliotuweka.

Mhe. Spika, mtu anatoka Pemba na ndizi zake na mihogo, hana nauli nyengine. Watu wanaacha bidhaa zao bandarini mara nyengine, kwa sababu mtu hawezi kutembea na pakacha lake mpaka anakokwenda. Kwa hivyo, sioni hapa kama mswada huu una lengo la kuwasaidia vijana kama tunavyozungumza. Kama ingekuwa ni kweli basi ungekuwa ni mswada mzuri, lakini je, hivi ulivyo ndivyo utakavyokuwa, kwa sababu hofu yangu...

Mhe. Spika: Unazo dakika tano kumaliza mchango wako.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Spika. Kwa sababu nyuma yangu hakuna saa ndio maana ikawa hivyo. Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha 6(h) kinasema;

Kifungu cha 6(h)

> "kuanzisha, kuendesha na kusimamia miradi yenye na isiyoletea faida katika kuunga mkono maendeleo ya vijana kama itakavyoonekanwa inafaa"

Mhe. Spika, kwanza kifungu hiki kwa mtazamo wangu mimi tukiondowe, mtu hawezi kufanyakazi isiyokuwa na faida, kuanzisha mradi ambao hauna faida itakuwa hatujafanya jambo zuri. Kwa hivyo, ningeomba kiondolewe kwa sababu sio busara kwa Baraza hili kuidhinisha mradi ambao utawaletea hasara. Sisi watu wazima na akili zetu kuidhinisha jambo ambalo lina hasara kwa vijana litakuwa halileti maana. Kwa hivyo, nitaomba kifungu hiki kisiwepo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa ukurasa wa 346, kifungu cha 10 (2) (a) na (b). Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha (b) naomba kunukuu kidogo;

> Kifungu cha 10 (2) (b) kinaelezea hivi:-
>
> > "Wawakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka Mtandao wa Jumuia zao za Vijana"

Kwa kweli jumuia zoa hapa Zanzibar ni zile za kisiasa. Kwa mfano, tunayo Jumuia ya Vijana ya CCM na Jumuia ya Vijana ya CUF. Sasa kwa kuwa wanatoka katika jumuia zao, pengine hawa watakuwa ni viongozi katika jumuia zao na tumesema kwamba Baraza hili kusiwe na viongozi wa kisiasa. Kwa hivyo, sijaona mantiki ya kuingiza vijana wanaotoka kwenye Jumuia za Kisiasa katika Baraza ambalo tunasema si la kisiasa.

Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mawazo yangu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii muhimu ya kuweza kutoa mchango wangu katika Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar.

Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu (*Subuhanahu Wataala*), alienijaalia pamoja na wenzangu kuwa katika hali ya uzima kuweza kusimama katika Baraza lako tukufu hili.

Vile vile, nichukue nafasi hii kwa kuwapa pole wale wenzetu waheshimiwa wajumbe wenzetu walioondokewa na wazazi wao akiwemo Mhe. Saleh Nassor Juma, ambaye ameondokewa na mama yake mlezi pamoja na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya kwa kuondokewa na mama yake mzazi. Kwa hivyo, tunawapa pole na wawe wastahamilivu katika kipindi hiki kigumu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia kheri.

Mhe. Spika, nikianza na utangulizi wangu, ni ukweli usiopingika vijana ndio nguzo na nyenzo muhimu ambapo kama wakiwezeshwa wanaweza kutoa mchango mkubwa katika taifa letu hili la Zanzibar.

Mhe. Spika, katika shughuli za maendeleo tunategemea sana nguvu kazi ya vijana, hasa kwa sababu Baraza hili la Vijana limeanzishwa wakati muafaka, tukijaaliwa tukiwaweka vizuri vijana wetu basi tunaweza kuwaepusha na mambo mengi ambayo ni mabaya na kujishughulisha na shughuli za kikazi.

Nikianza mchango wangu niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 343 kifungu cha 3(1), Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Ukurasa wa 343 kifungu cha 3(1) kinaeleza hivi:-

> "Kuanzishwa kwa Baraza la Vijana (*ZYC*), ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa"

Mhe. Spika, wasi wasi wangu hapa namuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa kufanya majumuisho, basi atupe ufafanuzi wa kutosha kuhusu hili neno *ZYC* alieleze kwa kina kwa sababu lina maana nyingi, pamoja na kwamba limetajwa kwa ufupisho wake ni vyema pia liandikwe kwa urefu wake, ili tupate kuelewa.

Nikiendelea kwenye ukurasa huo huo kifungu cha 4(1) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 4(1) kinaeleza hivi:

> "Uwanachama kwa Baraza utakuwa wazi kwa vijana wote kupitia Mabaraza yao ya Vijana na Shehia"

Mhe. Spika, jambo hili ni zuri. Lakini kupitia kwenye sehemu ya shehia lazima tuwe makini katika kutoa elimu ya kuwafahamisha mambo yatakayohitajika mpaka ukaupata huo uwanachama na elimu ianze huko kwenye Mabaraza ya Shehia. Basi vijana wetu watafahamu nini malengo na madhumuni ya kuanzishwa hili Baraza, kwa sababu huko ndiko kwenye

utashi mkubwa, lakini tukishafahamu huko chini basi na juu itakuwa ni murua kabisa.

Vile vile, kwenye kifungu cha 4(3) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

"Mwanachama wa Baraza atakuwa na haki na wajibu kama ifuatavyo"

Mhe. Spika, kuna mambo kama saba ambayo yameorodheshwa hapa tena yote mazuri na wala sipingani nayo. Lakini kungekuwa na miko ambayo ingeelezwa wazi wazi. Nadhani nivitaje hivi vigezo ambavyo vimetajwa:

(a) kuchagua na kuchaguliwa,
(b) kutoa maoni na mapendekezo na ushauri kwa Baraza,
(c) kuhudhuria vikao kwa wakati na mahala ulipopangwa,
(d) kuwa muaminifu na mkweli,
(e) kutunza siri za taarifa zote za siri za Baraza,
(f) kuwa ni mfano kwa wengine utekelezaji katika kuhusisha masuala ya vijana,
(g) sheria, sera na mipango na kulipia ada za uwanachama na malipo mengineyo.

Kwa kweli jambo hili ni zuri, lakini kungekuwa na miko kwa sababu sifa zimetajwa, atakayekiuka mambo haya ni hatua gani zitakazochukuliwa. Nadhani hii ingekuwa wazi na hapo tungepata Baraza ambalo litakuwa zuri kwa ajili ya kuwajenga vijana wetu katika mazingira ambayo ni mazuri.

Kwa mfano tukiangalia vijana ndio wenye kuleta neema au shari kama itakumbukwa. Mhe. Spika, ukitaka kuwatumia vizuri vijana basi watakuwa na malengo mazuri na ukitaka kuwapindua basi wanakuwa ni kikwazo, kama vile kulikuwa na vikundi hapa vinajiita Ubaya Ubaya na mambo mengine kama hayo. Sasa hapa tuwe na Baraza ambalo litakuwa na mustakabali mwema.

Mhe. Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 344 kuna malengo na uwezo wa Baraza. Kwa maana hiyo, Baraza limelazimika na malengo yafuatayo:-

1. Kuwajenga vijana kuwatambua utaifa wao, hali ya umoja, mshikamano, kujiheshimu pamoja na kuifahamu kwa kina jamii kiuchumi, hali halisi, kiutamaduni pamoja na upeo wake.

Haya kwa mujibu wa sheria hii ni mambo mazuri sana kama yatafuatwa. Lakini kwenye mambo haya ni kwamba vijana wayafahamu hayo malengo yaliyokusudiwa na pia wasishiriki katika mambo ya kisiasa na wakianza tu

kushiriki mambo ya kisiasa kwenye Mabaraza yao, basi hakuna litakalofanikiwa hata moja.

Kutokana na hali hiyo, nadhani ni vyema vijana wakapewa elimu ya kutosha na utakapofika muda wao wa kuunda Mabaraza, basi kila mtu akajifahamu itikadi hii haifai na ipi inafaa katika kujenga mustakabali mzima wa Baraza. Kwa sababu wamepewa uwezo mkubwa na hasa kulitambua taifa lao imesisitizwa hapa. Mhe. Spika, taifa ambalo lenye uchumi mzuri na mafanikio mema katika kujenga taifa letu na sio taifa la kujenga vijana ambao watakuwa walevi.

Kwa hivyo, tukilitambua hilo katika kutoa elimu basi kuna mafanikio mazuri sana.. Sasa kama tutapanga mambo mazuri kama hayo na elimu ikatolewa, kwa sababu jambo lolote kama hujapata elimu basi haliwezekani likawa zuri.

Namuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kazi hii ifanyike mapema ya kuwapa elimu vijana katika ngazi ya shehia na wilaya kwa ajili ya kufahamu na baadae basi watakuwa na malengo mazuri, lakini wakitoka kama kila mtu anataka kuingia kwa ushabiki basi hakuna litakalokuwa.

Mhe. Spika, imeelezwa hapa kwenye ukurasa wa 346 kifungu cha 10(1), naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 346 kifungu cha 10(1), (2) na kinaeleza hivi:-

1. “Mkutano Mkuu wa Taifa ni chombo cha ngazi ya juu cha kufanya maamuzi katika Baraza la Vijana la Zanzibar".

2. Mkutano Mkuu Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:-

   (a) Mwenyekiti wa Baraza Mkoa, Katibu na wanachama watatu kutoka kila mkoa wa Zanziabar kwa kuzingatia jinsia,

   (b) Wanachama wote wa Baraza la Watendaji,

   (c) Wawakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa umoja wa wanafunzi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, hoja yangu ipo hapa, kwa kweli hapa tayari imeshaelezwa kwamba wajumbe watakavyopatikana na kuzingatia jinsi na kwamba tunajua jinsi ni mke na mume.

Lakini tunamuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba angeweka wazi hapa kama ni wanawake au wanaume wangapi, kwa sababu pengine inawezekana kama kwenda kupiga kura jinsi moja isipite na ikawa ni tatizo. Kwa maana hiyo, angeeleza hapa ingekuwa jambo zuri zaidi.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 354 kuhusu madhumuni. Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo hapa.

Ukurasa wa 354 unaeleza kuhusu madhumuni. Madhumuni ya kuanzisha Baraza hili ni kuwajenga vijana katika kulijenga taifa lao. Lakini vijana katika kujenga taifa lao lazima kuwe na mfuko maalum wa kuweza kuwasaidia na kinyume chake itakuwa ni kuunda tu na hili litakuwa ni tatizo. Itakuwa ni vyema kuwe na mfuko maalum ambao utawawezesha kupata nyenzo za kufanyia kazi. Kwa kweli tunayo matumaini makubwa kwamba vijana wetu watapata nyenzo za kufanyiakazi, basi *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kutakuwa na mafanikio makubwa sana.

Mhe. Spika, zipo fursa kama vile watu waliojiweka kwenye vikundi, kama ni wavuvi basi wasaidiwe katika nyenzo za kiuvuvi, pia wajasiriamali wengine wasaidiwe kwa jinsi walivyojipanga kwenye shughuli zao nzima wanazozifanya, isipokuwa ni lazima kuwe na mfuko maalum wa kuweza kuwasaidia.

Kwa mfano hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi, basi vijana wawe na fungu lao la bajeti kwa ajili ya kuweza kujiwezesha kwenye mambo hayo na itakuwa ni vizuri zaidi na wakiwa na fungu wataweza kusonga mbele na kama hawana basi watarudi nyuma sana. Kwa sababu itakuwa umewapanga tu na wala hawana nyenzo zozote za kufanyiakazi, lakini wakiwa na fungu maalum na wakipata zile nyenzo basi wataweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu hayo machache na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, tumeupitia sana na tunawaomba wenzetu wote wauchangie na baadaye mswada huu tuupitishe kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, asante sana awali ya yote nachukua nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu aliyetujaalia uhai pamoja na kutupa uzima, na akatukutanisha hapa leo kwa ajili kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia, na mimi niungane na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa wenzetu waliopata misiba ya wazazi wao na Mwenyezi Mungu awape subira na marehemu awalaze mahala pema peponi, amin.

Mhe. Spika, pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa angalau maneno machache kwenye mswada ambao uko mezani wakati huu.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mhe.Waziri, pamoja na watendaji wake kwa kuamua kutuletea mswada huu mezani, ambao unahusiana na kuunda kwa Baraza la Vijana la Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa kweli tunajielewa kwamba katika taifa vijana ndio muhimili mkubwa wa kujenga uchumi pamoja na ustawi wa nchi. Mhe. Spika, tukielewa kwamba sisi ndio wenye majukumu kama serikali ya kuweza kuwaelimisha, kuwafahamisha pamoja na kuwaweka vyema vijana katika kuwafunza mwelekeo unaokubalika na unaoendana na mila na silka za nchi wanayoishi.

Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwa wakati tulionao tumeona wazi wazi kwamba kundi la vijana linakwenda bila ya kujielewa, wapi lipo na linaelekea wapi. Kutokana na hali hiyo, nimejengeka imani kuona kwamba serikali imeona sasa umefika wakati wa kuwakusanya vijana wa kizanzibari wa kuwaweka pamoja katika mtiririko wa mabaraza, ili wajielewe, wajifahamu, waangalie na waelimishwe mila, silka pamoja na tamaduni za Zanzibar kwa ajili ya kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Sote tunashuhudia kwamba vijana wetu kwa wakati huu katika mambo mbali mbali wanajihusisha na mambo kadhaa, ambayo yanapelekea mmong'onyoko wa maadili na yanapunguza nguvu kazi na uchumi wa taifa letu.

Vile vile, tumeshuhudia vijana kuharibu mambo mbali mbali ya kimaendeleo, pia vijana kutokuwa na mila na tamaduni ama kujielewa, kusimama katika majukwaa tofauti wakitoa matusi kinyume na mila na silka za kizanzibari. Kwa hivyo, nimejengeka imani sana kuona kwamba kuwepo kwa mabaraza haya sasa ni kweli tumeamua kuwafunza vijana wetu na tukielewa kwamba Waswahili wanasema "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Mhe. Spika, nina imani kwamba sasa tunawataka vijana wetu wa Zanzibar wapi waelekee. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nampongeza sana Mhe. Waziri, kwamba sasa umefika wakati wa kuwaona vijana wasikae vijiweni na kuvuta bangi, madawa ya kulevya na hali ngumu ambayo imelikabili taifa ya janga la UKIMWI. Mhe. Spika, ninamwambia hongera Mhe. Waziri, lakini anahitaji usimamizi wa kina, uadilifu, busara pamoja na ukaribu kabisa na vijana hawa ambao anakusudia kuwakusanya pamoja.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu kupitia huu mswada baada ya utangulizi wangu huo, nianze kwenye ukurasa wa 342 sehemu ya kwanza ya utangulizi, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Ukurasa wa 342 Sehemu ya Kwanza Utangulizi unaeleza hivi:-

> "Baraza maana yake ni Baraza la Vijana la Zanzibar kuanzia ngazi ya kitaifa hadi ya shehia"

Mhe. Spika, napenda kusema kwamba ingependeza zaidi tuanze kusema kuwa tuanze na ngazi ya shehia na kuja hadi taifa, kwa sababu tunajua kwanza mtoto anaanza kuwa mdogo na hatimae akafikia huko juu. Kwa hivyo, tungependa sentensi hii ibadilike kidogo na ianzie hivyo na wala isiwe kitaifa na iwe taifa lakini ianzie kwenye shehia kwa kuwa ndiko inakoanza.

Nikiendelea kwenye sehemu hii ya kwanza kuna tafsiri naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Sehemu ya Kwanza kuhusu tafsiri inaeleza hivi:-

> "Mualikwa kiofisi" maana yake ni wageni walioalikwa ambao watatokea katika taasisi za serikali kuhudhuria kwenye mkutano wa Baraza"

Mhe. Spika, hapa nataka kuhoji kwa ajili ya kupatiwa ufafanuzi, hivi hili Baraza litaalika taasisi za kiserikali tu, maana hii tafsiri inaonesha kwenye mswada huu kwamba itaielekeza moja kwa moja kuwaalika watu wa taasisi za serikali. Kwa hivyo, nasema kwamba kwa tafsiri hii itawanyima vijana ambao hawapo katika hizi taasisi za kiserikali na hali hiyo ni kuwatenga vijana hao na kuonesha kwamba wao hawatapata nafasi hiyo ya uwalikwa.

Kwa maana hiyo, ninapenda sana isiwe kualikwa kwa taasisi za serikali tu, isipokuwa iwe tu ni waalikwa ili tuweze kuwapa fursa na wale ambao wako nje ya taasisi nyengine ambazo si za kiserikali. Hii itakuwa ni kwa ajili ya kwenda kushirikiana na vijana wenzao ili kuweza kujiendeleza na kupata mambo mbali mbali au kuzungumzia hatma ya vijana hao.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende sehemu ya pili kwenye kifungu cha 3(1)(c) naomba kunukuu kidogo hapa.

Kifungu cha 3(1)(c) kinaeleza hivi:-

> "na uwezo wa kumiliki, kununua na kupata na kuuza mali inayohamishika na isiyohamishika na linaweza kupokea zawadi, gawio na msaada kwa jina lake"

Namuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipatie ufafanuzi ili niweze kuelewa kifungu hiki. Kwa kweli kuna zawadi ambazo zinawezekana baadaye zikaja zikageuka zikaenda kwenye misingi ya rushwa ambayo kwa taifa letu tunapiga vita kwa asilimia mia moja. Kwa hivyo, ninahitaji ufafanuzi wa kina ili niweze kuelewa kwamba hizi zawadi zinakusudiwa vipi au ni zipi hizo zawadi ambazo zinazokusudiwa kwamba wanaweza wakapatiwa hawa vijana na ikawa ni sahihi.

Jambo jengine ni kuhusu kifungu cha 3(2) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 3(2) kinaeleza hivi:-

> "Baraza litakuwa katika mpangilio ufuatao:-
>
> (a) Baraza la Vijana Taifa;
>
> (b) Baraza la Vijana Wilaya na
>
> (c) Baraza la Vijana Shehia"

Mhe. Spika, kwa mfumo na utaratibu mzima tulionao katika utaratibu wetu wa ngazi mbali mbali katika nchi yetu tunaanza na shehia, jimbo, wilaya, mikoa na hatimae taifa. Kwa maana hiyo, ni vyema vijana hao wakapangiliwa kwa mtiririko huu, basi ungeweza kuwaunganisha kwa uzuri pamoja na ukaribu zaidi, kwani ukitoka shehia unakwenda kwenye jimbo na watakuwa katika jimbo lao na kufanya mambo yao. Wakitoka hapo watakwenda wilayani, mkoa na kumalizia taifa. Kwa hivyo, ushauri wangu ni huo tu kuhusiana na suala hili.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye kifungu cha 4(3) kuhusu uwanachama wa Baraza, Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 4(3) kinaeleza hivi:-

> "Mwanachama wa Baraza atakuwa na haki na wajibu, na hapa zimeelezwa kuanzia (a) mpaka (g)
>
> (e) Kutunza siri za taarifa zote za siri za Baraza"

Mhe. Spika, naomba kumueleza Mhe. Waziri kwamba malengo yanayofanya mabaraza haya na kuwakusanya pamoja vijana wa kizanzibari kwa lengo la kujiendeleza, basi lazima tupate tafsiri nzito na tupate ufafanuzi wa kina, kwamba vijana watakuwa na siri gani itakayotunzwa ambayo ikisambazwa inaweza kuleta mashaka. Kwa hivyo, uwazi kwa vijana wetu ni suala la msingi la kuweza kupatiwa misaada ya kifikra na kimawazo, ili tuweze kuwaendeleza.

Mhe. Spika, siri hii ni ipi basi ni vyema Mhe. Waziri kwa ruhusa yako Mhe. Spika angeifafanua na kuiweka wazi ili ieleweke. Labda ingekuwa rahisi na kila mmoja wetu kufahamu kwamba hao vijana wanatayarishwa na siri zao. Lakini vyenginevyo kila mjumbe atakayeinuka atakuwa anazungumzia hii siri.

Vile vile, kifungu cha 4(5) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 4(5) kinaeleza hivi:-

> "Mwanachama au kiongozi atasita kuwa mwanachama kutokana na yoyote au sababu zifuatazo, zikaelezwa kutoka (a) mpaka (f).
>
> (f) Kwa kufikia umri wa miaka 35 na zaidi"

Lakini kwa kuwa tulipotoka kwenye tafsiri ya maneno tulisema kwamba kijana ni kuanzia miaka 15 hadi 35. Kwa hivyo, napenda kusema hapa basi yule ambaye hatakuwa kijana ni miaka 36 na kuendelea, lakini hili ukiliacha hapa maana yake kwenye 35 katika tafsiri limewekwa hivyo. Mhe. Spika, napendekeza kwamba liwekwe hivyo, ili liweze kusomeka vizuri.

Kifungu cha 7 naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 7 kinaeleza hivi:-

> "Katika kuhakikisha kuwa linafanyakazi zake kiufanisi kwa mujibu wa Sheria hii, basi Baraza litakuwa na uwezo wa"

Mhe. Spika, sentensi hii haikukaa vyema, hivyo ni vizuri ingewekwa wazi kwamba Baraza ili kuhakikisha litafanya kazi zake vizuri na kwa ufanisi kwa mujibu wa sheria hii, Baraza litakuwa na iwe hivi. Lakini tukianza tu katika kuhakikisha kuwa linafanyakazi zake, haikukaa vyema, basi ni vizuri iwekwe katika utaratibu ambao unaoneshwa mwanzo hicho kitu ambacho kinafanyakazi vizuri.

Pia, kwenye kifungu hichi cha 7(d) naomba kupata ufafanuzi, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 7(d) kinaeleza hivi:-

> "Kupokea michango au hiba iwe ni ya fedha au mali nyengine kutoka kwa mtu au taasisi, kwa ajili ya kuendeleza utekelezaji wa malengo yake, isipokuwa pale ambapo mtu au taasisi hiyo wanajihusisha na matendo yaliyokinyume na sheria au maadili"

Namuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze vizuri maana ya hiki kifungu, nakiona kwamba kimesema *hiba* na hii *hiba* naomba tafsiri yake pamoja na undani wake ili tuweze kulijua. Vile vile hivi kilivyokaa hiki kifungu kinaonekana si vizuri kukaa hapa.

Katika ukurasa wa 346 kifungu cha 9(3) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 9(3) kinaeleza hivi:-

> "Watendaji wawili wa serikali ambao wataalikwa kutokana na utaalamu wao ili kuunga mkono Mkutano Mkuu wa Taifa"

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 3 baada ya (a), (b) na (c) tuongeze kijifungu kimoja ambacho kitawajumuisha taasisi za uma na binafsi. Kwa hivyo, kuna sentensi nyengine kinyume na ile tafsiri ambayo tumeiacha kule, labda kijifungu chengine kiingie hapa "Mjumbe mmoja labda kutoka vyuo vikuu".

Kwa sababu tusiwape nafasi hao kusudi na wasomi wapate hizo nafasi ili kuweza kuliendeleza hilo Baraza lenyewe, liwe la kileo na la kitaalamu kabisa ambalo litakuwa la ubunifu na mambo kadhaa ambayo yatawafanya waweze kuja juu. Tukiweza kuwaweka hawa Wajumbe bila ya kuingiza, tukisema ni kutoka serikalini tu.

Nadhani hapa katika hao itakuwa inasomeka "Mkutano Mkuu utakuwa na wanachama wafuatao waalikwa ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura". Kwa hivyo, wakaelezwa hapa. Hawa walioelezwa ni sahihi. Lakini nasema ni vyema basi tuongeze hawa kutoka vyuo vikuu vilivyopo Zanzibar, nadhani ingekaa vizuri. Ili nao kuwapa nafasi na kushirikiana na wenzao katika kuona kwamba Baraza lao linapata nafasi vizuri.

Baada ya mchango wangu huu Mhe. Spika, naona mimi kwa mtazamo wangu haya ndiyo ambayo nimeyaona yana mapungufu kidogo na yanahitaji marekebisho. Niendelee kwa kusisitiza Mhe. Waziri, katika muundo huu ni lazima kuwa na usimamizi. Lakini pia, zitolewe taaluma ili wapate elimu hao vijana. Kama tunavyojuana Zanzibar kwamba siasa zimepoteza mambo yetu mengi ya kimaendeleo, tumepoteza nguvu kazi zetu, tumepoteza uchumi wa Taifa kwa sababu ya mambo ya siasa.

Ningependa kwa wakati tulionao, tunataka kuwajenga Wazanzibari, washikamane wawe pamoja, waweze kufanya kazi kwa pamoja, waweze kuwa pamoja kwa ajili ya maendeleo yao, basi tusije kabisa tukajaribu kuyafanya mambo haya katika mifumo ya kisiasa au mambo ya kisiasa. Badala yake vijana ambao wana uwezo, wana nafasi waweze kupewa kwa ufanisi mkubwa, wapewe taaluma, wapatiwe hiyo misaada, waanzishe hivyo vikundi na taratibu mbali mbali ili waweze kufanikiwa.

Mhe. Spika, tukijielewa kwamba Zanzibar kwa wakati huu tuna majanga yaliyotukabili ambayo yamekuwa ni tishio kwa uchumi wa taifa letu kulega lega. Lakini pia, kupata vijana wa maadili ambao watakaoweza kuja kuirithi Zanzibar na kuweza kuiongoza. Tuna watu wavuta unga ambao sasa hivi ni waathirika wakubwa zaidi na imekuwa ni hatari. Vijana wetu wanaathirika na majanga ya Ukimwi, sote tunaliona hilo.

Ni vyema kabisa tukawaelekeza vijana kuunda mabaraza yao na kuona wana uhuru wao wenyewe wa kujadili yale yanayowagusa vijana wenyewe wasitoke wengine wakaingia kati au wakawa Wajumbe wa kwenda kuwachochea kuwapotezea malengo ya uundwaji wa Baraza hili. Baada ya kuyasema hayo Mhe. Spika, nasema ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima. Aidha nikupongeze na kukushukuru binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi sana kwenye Mswada huu ambaye Mhe. Waziri, wa Ustawi wa Jamii ameuwasilisha.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, kwa jinsi ambavyo ametuletea Mswada huu, jambo ambalo aliahidi muda mrefu kwamba kama Waziri basi ameamua kusimamia suala hili la vijana na hatimaye leo azma yake imetimia. Nimpongeze binafsi kwamba ni Waziri ambaye ametekeleza ahadi yake.

Nilipokuwa katika Kamati ya Ustawi wa jamii, Mhe. Waziri, alituahidi kwamba jambo hili atalifanya akijaaliwa ndani ya miaka hii mitano na kweli leo imetimia ahadi yake. Naomba nimpongeze sana kama Waziri aliyefanya wajibu wake.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa niseme tu kwamba malengo na madhumuni ya Mswada huu kama Mhe. Waziri alivyoeleza, basi naunga mkono mia kwa mia. Kwamba ni kuwasilisha maslahi ya vijana kitaifa Kanda na Kimataifa kwa mujibu wa sheria. Madhumuni haya ni sahihi na naomba niunge mkono madhumuni haya ya Mswada huu.

Niende kwanza kwenye tafsiri, niungane mkono na wenzangu Mhe. Spika, kwamba hatuwezi kuwa na Baraza ambalo limeanzia kileleni. Baraza la Vijana huwa linaanzia Taifa, Wilaya hadi Shehia, nadhani kimahesabu na kitaalamu tuanze Shehia na kwenda Taifa. Ukisema unaanzia Taifa inaonesha kwamba kuna watu umewalenga kwamba hawa ndio Taifa na tayari unao mkononi. Kwa hivyo, tuchaguane kuanzia shehia, shehia wazae wilaya, wilaya izae mkoa na mkoa uzae taifa. Hilo ndio Baraza la Vijana la Taifa.

Mhe. Spika, kwa msingi huo tafsiri ya neno Baraza kifungu cha 2, maana yake ni:

Kifungu cha 2

> "Baraza la Vijana la Zanzibar kuanzia ngazi ya Kitaifa hadi ngazi ya Shehia ..."

Naomba isomeke kuanzia ngazi ya shehia nadi ngazi ya kitaifa, tuanzie chini kuelekea juu, sio uanze juu kuja chini, wasi wasi wangu ukianza juu, wachini utawasahau hatimaye itakuwa ni Baraza la watu fulani.

Mhe. Spika, vile vile, tafsiri ya mualikwa kiofisi maana yake ni wageni waalikwa ambao watatokea katika taasisi za serikali kuhudhuria mkutano huo. Mhe. Spika, serikali hii hii imesisitiza dhana ya PPP, lazima tuwashirikishe wadau binafsi. Baraza tusiwape nguvu tu ya kuwaalika serikalini, tuwaalike watu wote wenye maslahi na Baraza, tualike serikalini na watu binafsi ambao tunahisi kwamba watachangia mchango kwenye Baraza.

Kwa hivyo, tafsiri ya mualikwa iwe ni waalikwa kutoka Serikalini na Taasisi binafsi ambao watatoa mchango kwa Baraza. Tusiwafunge watu wenye mawazo mazuri na uwezo mzuri kwa ajili ya Baraza tukadhani kwamba wao hawana fursa hiyo.

Mhe. Spika, jengine kifungu cha 3(1)(c) ukurasa wa 343. Dhana moja ya Baraza tukasema kwamba na uwezo wa kumiliki na kununua kupata na kuuza mali inayohamishika na isiyohamishika na inaweza kupokea zawadi, gawio na msaada kwa jina lake.

Mhe. Spika, naomba tuongeze kwamba mapokezi hayo ya gawio, msaada, basi tuongeze maneno kwamba chini ya utaratibu halali na wa kisheria, tusipokee tu gawio na msaada, lakini kuna utaratibu halali wa kisheria ambao tumekubaliana. Ukimwambia tu kwamba Mkurugenzi au Katibu Mtendaji apokee zawadi hatimaye atapokea zawadi ambavyo si sahihi kwa malahi ya Baraza. Nadhani zawadi hiyo iwe kwa utaratibu halali na ambao umekubalika kisheria.

Kifungu cha 3(2)

"Baraza litakuwa katika mpangilio wa muundo ufuatao"

Mhe. Spika, naomba tuanzie ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa na hadi Taifa. Ngazi ya Mkoa Mhe. Spika, ni muhimu sana, kwa sababu hapa tumesahau ni lazima tuanze na ngazi ya Shehia, Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

Kifungu cha 4(3)

"Mwanachama wa Baraza atakuwa na haki na wajibu ifuatavyo:
(a) Kuchagua na kuchaguliwa"

Mhe. Spika, narejea kusisitiza kwamba sheria hii inamtambua kijana kwamba miaka 15. Naunga mkono kabisa na wale wote wanaosema kwamba kijana awe ni miaka 18. Kwa nini Sheria ya Mtoto ambayo tumeipitisha mwaka juzi inamtambua kwamba mtu mwenye umri wa miaka 15 kwamba ni mtoto. Anapaswa asikilizwe, lakini hana maamuzi. Ni lazima asikilizwe maoni yake, hatimaye wenye maamuzi waamue.

Kwa hivyo, sheria hii tukiweka kwamba miaka 15 ni kijana maana yake kwamba apige kura, Katiba ya Zanzibar hairuhusu hivyo, kifungu cha 7(1) kinatambua kwamba mtu mwenye uwezo wa kupiga kura ni lazima awe miaka 18 kama mtu mzima. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, kwamba kijana tumtambue kwa tafsiri hii kwamba ni kijana mwenye

umri wa miaka 18 - 35 ambaye maamuzi yake yatakuwa halali kwa mujibu wa Katiba na hata maazimio na sheria za Kimataifa.

Kifungu cha 4(3)(g)

"Kulipia ada za uwanachama na malipo mengineyo"

Naomba tuongeze yaliyoidhinishwa na Baraza. Asije tu Katibu Mtendaji akamwambia mwanachama lipia ada hii kumbe haijaidhinishwa na Baraza. Lazima ada ile iwe imeidhinishwa na Baraza kwa madhumuni ya Baraza na sio kwa madhumuni binafsi.

Kifungu cha 4(4) ukurasa wa 343:

> "Mwanachama au kiongozi wa Baraza anaweza kusimamishwa au kuondoshwa katika uongozi au uwanachama na Kamati ya Nidhamu kutokana na sababu zifuatazo"

Mhe. Spika, naomba tafsiri ya Kamati ya Nidhani tuiweke. Kamati ya nidhamu ni ipi. Humu nimejaribu kutizama sijaiyona tafsiri yake. Kwa hivyo, Kamati ya Nidhamu kama imo ni chombo maalumu, basi kiwekwe tuambiwe kwamba Kamati ya Nidhamu ni kamati gani. Na kwa utaratibu gani ataonywa na atapewa karipio au akishakuonekana kwamba kafanya kosa atimuliwe tu.

Kwa hivyo, tuweke utaratibu maalumu ambao utalinda haki ya kijana pale atakapofanya kosa, ili vijana wakifanya kosa wahukumiwe kwa mujibu wa kosa. Lakini na viongozi wa Baraza vile vile na wao wahukumiwa kwa mujibu wa kosa. Mhe. Spika, nasisitiza kwamba tafsiri ya neno kamati ya Nidhamu lazima tuelezwe.

Mhe. Spika, ukurasa wa 345 Kifungu cha 7(b):

> "kuanzisha vitega uchumi au kuzishughulikia fedha ambazo bado hazijahitajika kimatumizi..."

Mhe. Spika, hakuna fedha ambayo haihitajiwi kutumika fedha zote zinahitajika kutumika. Naomba tusijizonge. Tuseme tu kwamba kuanzishwa vitega uchumi kwa njia inayoonekana inafaa na Baraza. Fedha zote zinahitajika hata fedha ziwe Benki, zinahitajika, lakini zimehifadhiwa tu. Kwa hivyo, haya maneno mengine ningemuomba Mhe. Waziri, tuyafute tuweke sentensi fupi kabisa, kwamba kuanzishwa vitega uchumi kwa njia inayoonekana inafaa kwa malengo ya kuendeleza Baraza.

Kifungu cha 7(c):

> "kusimamia, kuhakikisha usalama, kukodisha, kuondosha, kuwekarehani..."

Mhe. Spika, Rais Abeid Amani Karume, tarehe 8 Machi, 1964 alipiga marufuku poni na kuweka rehani. Leo sheria hii inatwambia kuweka rehani ni halali. Mhe. Spika, tukifute kifungu hichi, hatuwezi kupingana na malengo ya Mapinduzi ambayo yameasisiwa 1964, leo tukasema kwamba kuweka rehani kwa sheria hii ni halali. Mhe. Waziri, nakuomba sana ufute neno rehani na utafute lugha nyengine ambayo inakubalika.

Kifungu cha 10(2)(c):

> "wawakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa umoja wa wanafunzi wa Zanzibar"

Mhe. Spika, ni mtandao upi. Hivi sasa hapa kuna mitandao ya wanafunzi mingi tu, kuna vyuo vikuu, kuna *nursery*, kuna msingi na kuna sekondari, ni mtandao upi uliokusudiwa. Namuomba Mhe. Waziri, atwambie ni mtandao upi. Kwa sababu tumeshuhudia hivi karibuni, mie ni Mjumbe wa Bodi ya Jumuiya ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu anajivunia Mhe. Hamza Hassan Juma. Lakini wamegombana tayari ipo *ZAHILFE (A)* na *ZAHILFE (B)* sasa ni mtandao upi unaokubalika.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri, atwambie ni mtandao upi wa Jumuiya ya Wanafunzi ambao unaokusudiwa kuwekwa katika Baraza hili.

Lakini vile vile, Jumuiya ya Vijana kifungu cha 10(d). Jumuiya za Vijana zipi. Vijana wanaopambana na Ukimwi, vijana wanaopambana na madawa ya kulevya, vijana wanaopambana na ubakaji ni wepi. Tuambiwe huu mtandao utakuwa umeanzishwa au Waziri anao mkononi tayari anaujua ni mtandao upi. Mhe. Spika, naomba tueleweshwe.

Kifungu cha 10(3) nadhani hakina haja, nikuombe kwamba kifutwe. Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wanachama wafuatao waalikwa ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura, wametajwa hapa Katibu Mkuu wa Wizara, Mkurugenzi wa Idara ya Wizara, watendaji wawili wa serikali. Mimi naona kifungu hiki hakina maana na naomba kifutwe.

Kama kuna mtendaji wa Wizara au mtendaji wa *NGO* ana maslahi na Baraza la Vijana, vijana watamualika kutokana na uzoefu wake na kutokana na taaluma yake. Ukiwawekea lazima Katibu Mkuu aalikwe, lazima Mkurugenzi

aalikwe, maana yake unaingiza serikali ndani ya Baraza, jambo ambalo litakwaza utendaji wa Baraza.

Mhe. Spika, tuwaachie huru vijana, tuwaelekeze kitaalamu vijana, lakini tusiingize nguvu ya serikali ndani ya Baraza hatimaye tukasema lazima waalikwe, watalazimisha mambo ambayo hayendi sambamba na matakwa ya Baraza. Mhe. Spika, kifungu cha 10(3) naomba kifutwe na kama kunahitajika Katibu Mkuu aalikwe au Mkugenzi aalikwe, nadhani Baraza watakuwa na uwoni huo, watashauriwa na Waziri wataalika watu wenye uwezo na taaluma zao kwa mujibu wa mahitajio yao na tusilazimishe kuagiza kualika Katibu Mkuu, Mkurugenzi na watu wa serikali ili kuwaepushia usumbufu na vikwazo ambavyo havina maslahi.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye Mswada huu sehemu ya ukurasa wa 351 Kifungu cha 21(2):

> "Hakuna matumizi yatakayofanywa kutoka katika fedha za Baraza, isipokuwa yawe yameidhinishwa na Katibu Mtendaji"

Mhe. Spika, hatuwezi kumpa rungu Katibu Mtendaji ambaye yeye ndiye mwenye kuidhinisha fedha peke yake. Katibu Mtendaji ni muajiriwa ni mtendaji mkuu wa Baraza. Pia, huyo huyo ndiyo aidhinishe fedha za Baraza. Mhe. Spika, si utaratibu wa matumizi ya fedha za umma, lazima Katibu Mtendaji fedha hizi azitumie chini ya uangalizi wa Baraza. Kwa hivyo, muidhinishaji wa fedha hizi ni Baraza la Utendaji, liidhinishe kazi za Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji atumie ili baadaye tuweze kumuangalia tuwe na *follow up* na *monitoring* ya fedha hizi. Sio yeye mwenyewe aidhinishe, atumie, aagize.

Mhe. Spika, lazima tudhibiti na kifungu hiki nikuombe sana kwamba huyu asiidhinishe, aweze kuongoza na kutumia, lakini adhibitiwe na Baraza la Watendaji ili wao waidhinishe na wasimamie fedha hizi kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niende kwenye mambo ya jumla niseme tu kwamba afisa wa vijana, wilaya ambao ni *secretariat* wa Baraza la Wilaya ameambiwa kwamba atoke wizarani. Mhe. Spika, Zanzibar Sera ya Elimu sasa hivi ipo wazi, kwamba tumeamua kuanzisha Sera ya Elimu ya chini kwamba sasa mtoto wa Zanzibar amalize *degree* ya kwanza akiwa chini ya miaka 18.

Vijana wapo wengi sana hapa Zanzibar wenye *degree* ya kwanza chini ya miaka 35, tusilazimishe kuwaweka wetendaji wa Baraza hili wakiwa ni

serikali. Tuwaachie vijana wachague watu wao bila ya Chama cha CCM na CUF watawale Baraza lao.

Mhe. Spika, Afisa wa Wilaya asiwe wa serikali na tuwaachie vijana waajiri mtu wao hasa kwa vile tumeweka mwanya kwamba Baraza hili litaajiri vijana kulingana na Sheria ya
Utumishi wa Umma. Tuwaachie waajiri mtu wao kwa sifa zao, kwa vigezo vyao na asiwe ngazi za Wilaya, awe ni Katibu wa Baraza la Wilaya.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kusema kwamba Katibu wa Baraza tumesema kwamba tumpe Rais amteuwe si vibaya mimi naunga mkono, Rais amteuwe, lakini tupendekeze majina matatu ambayo tumwambie Rais, majina matatu haya yenye sifa hizi basi tuchagulie mmoja awe ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Vijana. Na hivyo hivyo Mhe. Spika, tuweke elimu, tusiteuwe tu. Tukiacha wazi hivi hivi ilivyo, wataachwa watu wenye uwezo, watapelekwa watu kwa mtizamo wa kisiasa jambo ambalo sio sahihi.

Mhe. Spika, nadhani tuweke majina matatu ili Rais ateuwe moja kati ya majina matatu na tuweke vigezo vya taaluma. Napendekeza Mhe. Spika, tuanzie na angalau *degree* ya kwanza. Katibu Mtendaji Mhe.Spika, lazima awe na elimu angalau *degree* ya kwanza ndio awe Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Vijana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo, Mhe. Waziri, akimfuta muidhinishaji wa fedha Katibu Mtendaji, nitaunga mkono hoja hii, kama hajamfuta nitazuia fungu langu. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, muumba mbingu na ardhi, kwa kutujaalia kuendelea kuwa hai na wazima na tukakutana tena tangu tulipoachana mwezi wa Oktoba, tukiwa tunatekeleza majukumu waliyotutuma wananchi wa Zanzibar.

Pili, Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu kuhusiana na Mswada huu wa Sheria kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, haitokuwa haki kuingia katika Mswada bila ya kuanza japo kwa ufupi kuzungumzia machache kuhusu yale ambayo ulitueleza asubuhi kupitia taarifa ya Spika, yaani msiba ambao umeikumba dunia kutokana na kifo cha mwanaharakati na kiongozi mashuhuri si tu Afrika ya kusini na Afrika bali ni dunia nzima naye ni Mzee Nelson Mandela.

Maelezo mengi umeyatoa Mhe. Spika, na haina haja ya kuyarejea, lakini mazito ni yale ambayo umeyaongezea mwenyewe ya mwisho. Kwamba miongoni mwa sifa zake nyingi ambazo ataendelea kukumbukwa nazo Mzee Nelson Mandela ni ule ushujaa wa nafsi yake. Pamoja na kuwekwa ndani kwa kifungo cha miaka 27 na mateso mengine mengi, lakini dhati ya nafsi yake na mapenzi ya nchi yake na kuthamini utu kulimtuma kukubali kusamehe yaliyopita na kuleta siasa za maridhiano Afrika ya Kusini. Siasa ambazo zimeifanya Afrika ya Kusini ikabakia kuwa salama na tulivu baada ya ubaguzi wa rangi.

Mhe. Spika, Mzee Nelson Mandela alikuja Zanzibar mwaka 1990 baada ya kutoka gerezani, ni katika nchi za mwanzo alizozitembelea. Nakumbuka nilikuwa mwanafunzi tulikuwepo pale uwanja wa Amani na yeye alimkumbuka na kumtaja kwa heshma Rais wa kwanza wa Jamuhuri ya Watu wa Zanzibar marehemu Mzee Abeid Amani Karume, ambaye alimtaja walikutana kwa mara ya mwanzo mwaka 1962 Mjini Addis Ababa na akaomba kwamba apelekwe katika kaburi lake. Kwa hivyo, ni mtu ambaye pia alikuwa na hisia fulani kwetu Zanzibar.

Ni vyema na ni mahala pekee kumthamini kwa Baraza hili kufanya kitendo tulichokifanya asubuhi hii chini ya uongozi wako Mhe. Spika, kutaka tusimame kwa heshima kwa dakika moja kumkumbuka shujaa huyu.

Mhe. Spika, wakati tunamkumbuka Mhe. Mzee Nelson Mandela ambaye atazikwa tarehe 15/12/2013, nadhani ni haki yake vile vile kuwakumbuka viongozi wengine wawili ambao wameiga mfano wake karibuni hapa Zanzibar nao ni Rais wa awamu ya Sita wa Zanzibar Mheshimiwa Dokta Amani Abeid Amani Karume na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar wakati huo akiwa Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad, ambao nao walitupandia mbegu kama ile aliyoipanda Mzee Nelson Mandela kwa kutuletea siasa ya maridhiano Zanzibar tukaweza kuvuka salama kwa mara ya mwanzo katika uchaguzi wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba wele wote waliojaribu kuchochea tena vurugu na kuhubiri siasa za ubaguzi watajifunza sio tu kwa Mzee Nelson Mandela, lakini vile vile kwa viongozi hawa wawili wa Zanzibar Rais Mstaafu Dokta Karume na Mhe. Maalim Seif ili kuona kwamba Zanzibar irudi tena ilikotoka na inasonga mbele katika zama mpya za kutumikia wananchi katika misingi ya ummoja, uzalendo na maridhiano kwamba ambavyo wameanzisha viongozi wetu hawa.

Ni lazima wajifunze Mhe. Spika, kwamba Zanzibar imeshatoka kule na wakiendelea kuhubiri ubaguzi wanaofanya hivyo, wanahatari ya kukimbiwa na vijana ambao hawakubali tena siasa za kipuuzi za aina hiyo.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa nizungumzie Mswada huu. Mhe. Spika, dhana ya kuleta Mswada wa Baraza la Vijana Zanzibar ni dhana nzuri sana. Wawakilishi wengi humu ndani walikuwa wakihimiza serikali juu ya suala hilo. Lakini baada ya kuupata Mswada na kusikiliza maelezo ya Mhe. Waziri, nimepata wasi wasi kidogo Mhe. Spika. Najiuliza kwamba nini malengo ya serikali katika kuleta Mswada huu. Hivi kweli lengo la kuanzishwa Baraza hili ni kuwapa fursa vijana wakawa na chombo cha kuwaunganisha bila ya kujali, itikadi zao, maeneo ya kijiografia wanayotoka, dini zao, rangi zao au misingi mengine yeyote au lengo ni kudhibiti vijana.

Katika maelezo ya Mhe.Waziri, alivyokuwa akiwasilisha alitumia neno hilo na nimelinukuu Mhe. Spika, kwamba lengo moja ni udhibiti wa vijana, mimi nimeshtuka. Na nilivyouona Mswada wenyewe ulivyo, nahisi kwamba kweli malengo ya serikali si kuwawezesha vijana, lakini ni kuwadhibiti vijana. Sasa kama malengo ni hayo Mhe. Spika, sisi wengine kidogo tutapata kigugumizi kuunga mkono Mswada huu.

Lakini bado nasema tunayonafasi ya kufanya marekebisho ili lile lengo lililokusudiwa kama ndio kweli la kuwawezesha vijana, kuwaweka pamoja na kuwapa chombo ambacho kitawaunganisha liweze kufikiwa. Mhe. Spika, kwa nini nasema hivyo. Kwanza nahisi mkono wa serikali umekuwa mkubwa mno katika Baraza hili na wenzangu wametaja baadhi ya mambo. Moja ni nilichokiona mimi nitakitaja katika vifungu vyake ni kwamba madaraka ya Waziri ni makubwa mno katika chombo kama hichi.

Mhe. Spika, nalisema hilo kwa nia safi kabisa. Dunia inabadilika kwa kasi sana na zama hizi tumeshuhudia Mhe. Spika, katika nchi tafauti na katika Mabara tofauti ya dunia, vijana wakijivisha wenyewe dhamana na nguvu ya kuamua mustakbali wao na wa nchi zao. Nchi nyingi zimeingia katika mchafuko, vijana walipofika kuamini kwamba kuna tabaka linalotawala ambalo haliwakilishi maslahi yao.

Tusifichane Mhe. Spika, hata hivi sasa tutakuwa ni wanasiasa wa ajabu humu ndani kwamba hatutaki kukubali ukweli wala hatutaki kukaa nao vijana huko nje. Vijana ambao wanaotuona kwamba wengi wetu hatuwakilishi maslahi yao,lakini tunatizama maslahi yetu sisi wenyewe, ziko hisia hizo Mhe. Spika.

Mimi ni mmoja ninaetamani kwamba Baraza hili liendelee kubeba hadhi ile ambayo tuliyokuwa nayo siku zote ya vijana kuona kwamba waliokuwemo

humu ndani tumo kwa ajili ya maslahi yao. Ili na wao vijana wa Zanzibar wasije wakachukua mkondo kama ule waliochukua vijana katika nchi nyengine. Nadhani hii ndio nafasi ya kihistoria ya kuwasaidia vijana wetu na kuisaidia nchi yetu kupata muelekeo huo uliokuwa mzuri, tusiwakatishe tamaa Mhe. Spika.

Najua jitihada mbali mbali zimekuwa zikifanyika za kusaidia kuleta jukwaa la majadiliano baina ya vijana na serikali ili kama kuna ufa mkubwa wa mawasiliano uwezo kuondoka baina yao. Karibuni katika jimbo langu la mji Mkongwe katika ukumbi wa Taasisi pale tulizindua jukwaa la majadiliano ambalo limeanzishwa na majimbo mawili, jimbo ninaloliwakilisha la mji Mkongwe na jimbo la Kikwajuni chini ufadhili wa Serikali ya Marekani, lakini likihusisha na serikali hasa Idara ya Polisi.

Lengo lake moja ni kufanya haya matukio ya kihalifu yanayotokea na yanayoongezeka, vijana wahisi kwamba na wao wakipata taarifa wanao wajibu wa kuisaidia serikali na taasisi zake kuweza kufikisha taarifa. Lakini tukifika pale tukaonesha kwamba lengo letu ni kuwadhibiti hawawezi kutoa ushirikiano huo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, nadhani ni muhimu sana kuona kwamba tunalizingatia hilo. Kwa sababu hiyo basi naomba niseme machache kuhusiana na vifungu mbali mbali vya Mswada huo. Kwa maelezo niliyokuwa nimeyatoa nianze na kifungu cha 2 kinachohusu tafsiri. Nimesema tunayo nafasi ya kurekebisha ikiwa serikali itakuwa sikivu na itakubali kufanya marekebisho Mswada huu. Sitopenda mimi niwe ni mmoja nitaokuja kuhoji, nikanyoosha mkono wa kuukataa Mswada huu kwa sababu naona malengo yake ni kudhibiti, tunaweza tukaurekebisha.

La kwanza Mhe. Spika, ni kifungu ambacho kimeshazungumzwa na wenzangu kinachoelezea tafsiri ya Baraza, niwaunge mkono wale wote waliosema kwamba tafsiri hii inapaswa ibadilishwe na isomeke kwamba Baraza maana yake linaanzia ngazi ya Shehia, Wilaya hadi Taifa badala ya kutoka Taifa likaja Shehia.

Lakini la pili, ni tafsiri ya neno mualikwa kiofisi. Mimi nakubali dhana ya mualikwa, lakini nakataa dhana ya mualikwa kiofisi. Ni kawaida vyombo vyote kama hivi vinakuwa na mamlaka ya kumualika mtu ambaye kutokana na uzoefu, utaalamu na umahiri wake kwenda kushauri chombo kile kikiona kina haja hiyo.

Lakini tunapowekea mualiko ambao tumemuekea Afisi maalum wa kiofisi ambaye ni kuwaingizia maafisa wa serikali, hii haioneshi dhana ya serikali

kweli kwenda kuwawezesha, lakini labda ile aliyoisema Mhe. Waziri, kwenda kuwadhibiti vijana. Sasa haya maeneo mawili katika tafsiri nilikuwa naomba Mhe. Spika, yarekebishwe.

Eneo jengine Mhe. Spika, kifungu cha 4 (4) kinazungumzia mwanachama au kiongozi wa Baraza anaweza kusimamishwa au kuondoshwa katika uongozi au uanachama na kamati ya nidhamu kutokana na sababu zilizotajwa pale. Lakini ukitizama mswada mzima hauelezi hiyo kamati ya nidhamu itaundwa na nani na muundo upi. Sasa mambo haya kuyaachia hivi Mhe. Spika, yanaweza kutoa fursa ya kuweza kutumika vibaya, nilikuwa naomba hilo Mhe. Waziri, alione na akija aje atupe ufafanuzi.

Jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 4 (5) (c), kifungu cha 5 kwa ujumla wake au kijifungu kidogo cha 5 cha kifungu cha 4 kinazungumzia hali ambayo mwanachama au kiongozi atasita kuwa mwanachama kutokana na hiyo katika sababu zilizotajwa pale. Sasa (c) imesemwa Kiongozi Mtendaji katika Chama cha Siasa. Mhe. Spika, mimi napata tatizo ukinambia Kiongozi
Mtendaji katika Chama cha Siasa asiwe kiongozi katika Baraza la Taifa la Vijana la Zanzibar naikubali, ili tuepushe mgongano wa maslahi.

Lakini yule akinambia mpaka mwanachama wa Baraza hawezi kuwa kwa sababu tu ya nafasi ya uongozi katika Chama cha Siasa, napata mashaka Mhe. Spika. Mimi nadhani kwa muda mrefu tumekuwa na Jumuiya za Vyama vya Siasa za vijana na makundi mengine ya kijamii.

Na haya yataendelea kuwa na nafasi yake Mhe. Spika. Sasa kama watapata uhalali wa kuchaguliwa katika maeneo yao wakaingia katika Baraza kama wanachama, mimi sijaona ubaya wake Mhe. Spika, kama kiongozi kama alivyosema nakubali. Kwa hivyo, kifungu hiki Mhe. Waziri akione kifungu cha 4 (5) (c).

Mhe. Spika, kifungu cha 5, lugha iliyotumika sikuipenda inasema Baraza linalazimika kuwa na malengo yafuatayo; si lugha ya kiuandishi ya sheria hiyo, ilipasa iseme Baraza litakuwa na malengo yafuatayo, nilikuwa nadhani hilo turekebishe.

Lakini Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho pia ningeomba nikitolee maoni ni kifungu cha 6, hapa sina mchango mahsusi wa kusema turekebishe kitu gani, lakini hoja yangu ni ile ambayo wengi wameizungumzia, naomba sana serikali ikipe uhuru chombo hiki, isije ikakiingilia kikaonekana kina upendeleo wa aina yoyote Mhe. Spika, kikija kikifika hapo hakitakuwa chombo cha kitaifa na hakitapata ushirikiano wa vijana wala serikali isije ikajidanganya, kwamba kwa kudhani tu kwamba labda kikachangia bajeti

tunaweza tukakitumia chombo hiki kwa maslahi yake, kama nilivyosema vijana wa leo wameamka sio vijana wa zamani.

Kwa hivyo, ni muhimu sana katika utekelezaji wa haya majukumu au kazi za Baraza zilizotajwa katika kifungu cha 6, kusiwe na upendeleo na serikali ijikinge kutokana na kuingilia chombo hiki.

Lakini jengine Mhe. Spika, nataka nitolee maoni vile vile kifungu cha 7 (b), katika uwezo wa Baraza imesemwa ni kuanzisha vitega uchumi au kuzishughulikia fedha ambazo bado hazijahitajika kimatumizi kwa dhamana na katika njia nyengine itakayoona inafaa na kubadilisha au kufanikisha vitega uchumi hivyo. Hapa tahadhari Mhe. Spika, tena kwa serikali kwa sababu ni la kusimamia utekelezaji wa sheria hii.

Tumeshuhudia mara nyingi jumuiya au vyombo kama hivi unapotoa mwanya wa kuweka vitega uchumi, watu kutumia nafasi zao kuendekeza maslahi yao binafsi na kuingiza mambo ya ufisadi na rushwa.

Mhe. Spika, wakati wa chama kimoja ninafikiri utakuwa unakumbuka kulikuwa na chombo kinaitwa SUKITA, kilihujumiwa kutokana na rushwa na ufisadi kutoka kwa wanaokiendesha na mifano kama hii inaendelea hata sasa Mhe. Spika. Kwa hivyo, kuwapa fursa kuanzisha vitega uchumi si vibaya, lakini natahadharisha tu kwamba isije ikawa ni mwanya wa ufisadi na rushwa.

Mhe. Spika: Una dakika 5 kumaliza mchango wako.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nitaomba uniongeze na dakika 5 ili nimsaidie Mhe. Waziri vizuri katika mswada huu. Na leo Mhe. Spika, tuseme kidogo tunapata tabu kwa sababu mbele huko hakuna saa, kawaida huwa kuna saa inatuongoza hapo, lakini inatupa kazi kubwa kweli kweli leo Mhe. Spika, watendaji wako ninafikiri utazungumza nao.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 hiki ndicho kilichonipa mashaka zaidi, kinasema, "Waziri anaweza kutoa maelekezo na ushauri kwa Baraza kuhusiana na utekelezaji wa kazi zitakazopokewa itapotokea umuhimu wa kufanya hivyo kwa maslahi ya vijana".

Mhe. Spika, mimi kutoa ushauri nakubali, Waziri kutoa maelekezo kwa Baraza siungi mkono kama ni chombo ambacho ni huru cha vijana waachiwe wenyewe wafanye maamuzi kupitia vyombo vyao, kutoa ushauri hakuna ubaya ningeomba hicho kikarekebishwa.

Jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 9, hapa lugha tu mtiririko wake 9(c) katika vyombo vya Baraza kumetajwa sekreteriet, lakini huko mbele Mhe. Spika, katika mswada huu huu katika sehemu ya mwisho kunazungumzwa Kamati tendaji, sasa ninafikiri waamue wanataka kuita jina gani Sekreterieti au Kamati Tendaji.

Jengine Mhe. Spika, na hapa ndio penye hoja zangu hasa ni kifungu cha 10(2) kinazungumzia Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, sasa hapa Mhe. Spika, pana mwanya wa kuja kuvurugwa sana. Kwanza Kifungu cha 10 (2) (c) kinazungumzia Wawakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa umoja wa wanafunzi wa Zanzibar.

Sasa hapa ndio Mhe. Hija Hassan Hija, pia, kazungumzia kwamba huu mtandao wa umoja wa wanafunzi anaouzungumzia ni upi, kwa sababu hakuna mtandao mmoja ambao serikali inautambua mpaka sasa hivi. Kuna jumuiya huko kwa mfano *ZAHIFE* imeanzishwa, kuna umoja wa wanafunzi wa sekondari zimeandikishwa serikalini kisheria, lakini serikali haijatambua kama huu ndio umoja unaotambulikana, sasa huu mtandao utakaochagua Wawakilishi ni upi.

Lakini kwa hoja hiyo hiyo Mhe. Spika, ni kifungu cha 10 (2) (d) kinachozungumzia Wawakilishi wawili wa vijana waliochaguliwa kutoka mtandao wa jumuiya za vijana, huu mtandao wa jumuiya za vijana ni upi. Je, ni *Zanzibar Youth Forum*, ni *Zanzibar Association of youth for education and parliament*, maana yake ziko nyingi Mhe. Spika, na hakuna mtandao mmoja uliyoziunganisha zote. Sasa hawa Wawakilishi watachaguliwa kutoka wapi na kwa utaratibu upi nilikuwa nadhani kwamba hilo ni muhimu liwekwe sawa. Na je, watachaguliwa na hizo jumuiya zenyewe au watachaguliwa na nani kifungu hakikuweka sawa.

Vile vile, Mhe. Spika, nilikuwa nadhani kifungu cha 10 (2) (e) kinachozungumzia vijana 2 wanaowakilisha vijana wenye ulemavu awali kilisema walioteuliwa na Waziri, ninashukuru Kamati imeliona imerekebisha imesema watakaochaguliwa kutoka katika Jumuiya za watu wenye ulemavu. Lakini nilikuwa nadhani isemwe basi ni upi kama tunautambua Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar UWZ kama ndio Wawakilishi itajwe kwa sababu inatambulika kisheria, tusiweke mwanya Mhe. Spika, wa kuja kufanya sheria hii ikawa nguvu katika utekelezaji.

Mhe. Spika, haraka haraka naomba niende kwenye kifungu cha 10(3) nimeshakitolea maoni pale mwanzo kuhusu waalikwa mimi sikiungi mkono. Naunga mkono kiwepo kifungu 10(3) kiseme Baraza litakuwa na mamlaka au uwezo wa kumualika mtu yoyote ambaye litaona kwamba kutokana na uzoefu

wake au utaalamu wake anaweza kulisaidia, lakini hao watendaji wa serikali wasiingizwe kwa nyadhifa zao Mhe. Spika, hata kama tunaambiwa hawana kura, hawa ndio wanaotoa bajeti, wakiingia
pale hata kama hawana kura wana uwezo mkubwa zaidi kutumia nafasi zao kwenda kushawishi maamuzi pale Mhe. Spika, mimi siwezi kukiunga mkono hiki.

Mhe. Spika, nimalizie haraka haraka kuna maeneo mawili, vile vile, siungi mkono kifungu cha 12(1) kinachozungumzia Katibu Mtendaji kuteuliwa na Rais. Mimi nadhani Mhe. Spika, kama ni chombo huru tumefika pahala tuone kwamba Baraza lenyewe liteuwe na kama haliwezi kuteuwa basi angalau kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija, lipendekeze kwa Rais angalau majina 3 ambayo kutokana miongoni mwao Rais ndio atachagua Katibu Mtendaji.

Vile vile, Mhe. Spika, kwa msingi huo huo yule Afisa wa Vijana wa Wilaya katika kifungu cha 14(c) kwamba ndio atakuwa Katibu wa Baraza la Wilaya. Pia, kwa msingi huo silikubali. Lakini vile vile, Mhe. Spika, katika kifungu cha 18(2) pamezungumzwa muundo wa Kamati Tendaji ya Shehia, pametajwa pale 18 (2) (c) Katibu, lakini katika mswada hapana sehemu yoyote inayozungumzwa huyu Katibu ni nani, atapatikana vipi, haikuelezwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba pia nipate maelezo.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, naunga mkono mapendekezo ya Kamati kwamba katika utungaji wa Kanuni hivi ulivyo mswada kwamba Waziri ndio imempa mamlaka yote, mimi sikubaliani nayo na nakubaliana kabisa na rai yao kwamba awe Waziri, wao wamesema kwa kushauriana, mimi ningependekeza iongezwe kwa kushauriana na kukubaliana na Baraza ndio atatunga kanuni za yale mambo ambayo yametajwa pale katika kifungu cha 26 kwa sababu haya ni mambo ya msingi ya Baraza Mhe. Spika, akiachiwa Waziri kutunga kanuni pia Baraza litakuwa halina meno limewekwa pale ili kufanya shughuli ya kudhibiti badala ya kufanya shughuli ya kuwawezesha vijana.

Baada ya kwisha kusema maneno hayo Mhe. Spika, kama nilivyosema awali, dhamira nzuri nitaiunga mkono ikiwa haya marekebisho ambayo nimeyataja serikali itayakubali tukaona kweli kwamba lengo lake ni kuwawezesha sio kuwadhibiti vijana.

Baada ya hayo Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nikushuru kwa dhati kabisa na mimi kunipatia nafasi hii kuchangia mswada huu ambao ni nguvu kazi ya vijana wetu na ndio tegemeo la taifa. Lakini kabla ya hapo Mhe. Spika,

nichukuwe nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika uadhimishaji wa miaka 50 ambayo ndio iliyotukomboa baadhi yetu tukafika hapa. Lakini nichukuwe nafasi hii niwashukuru sana kinamama wote ambao walinifanya nikarudi tena kwenye Baraza hili nikashuhudia kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nimpongeze sana Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kumtakia kila la kheri kwa kutimiza miaka mitatu katika utawala wake wa awamu hii ya saba.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijampongeza Mhe. Waziri, nimpongeze sana Mhe. Waziri ambaye na yeye ni mlezi na ni mzazi ameona kwamba kile kilio cha Waheshimiwa Wawakilishi kilichokuwemo humu basi amekitekeleza kwa mujibu wa matakwa ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kuundwa Baraza hili ambalo ni Baraza litaloweza kushikamana na kujenga taifa hili kwa mustakbali mzuri.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu ambayo takriban mengi nimefilisiwa, lakini si vibaya nikaongezea. Mhe. Spika, niseme na niwatake wanasiasa wenzangu wa Baraza hili kama kweli tunataka Baraza hili la Vijana kuanzia shehia mpaka mkoa, basi kwanza tujiulize sisi wenyewe tuko tayari kusaidia? Lakini kama tutafanya mambo ambayo Mhe. Spika, yatatuletea vurugu kwa sababu huko nyuma tumekosa mambo mengi sana kwa kuingia kwenye siasa. Niombe Mhe. Spika, niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tuwache tuliyonayo ili tuweze kuwashughulikia vijana wetu ambao kila kukicha vijana wetu wanatakiwa wafanyiwe mambo ambayo yanayowagusa wao wenyewe moja kwa moja.

Mhe. Spika, unapokuwa kijana basi akili yako inakuhakikishia chochote unaweza ukafanya. Niwaombe vijana ambao leo tunawatungia sheria ya kuundwa mabaraza wahakikishe kwamba sheria hii ikishakufika kuwa ni sheria basi waitumie ipasavyo. Si vyema kuwa wanalalamika tu kwenye maredio, wenzangu wameeleza hapa kwamba vijana wengi wanajishirikisha na mambo ambayo si ya kuridhisha katika nchi yetu. Lakini niwaombe na niiombe serikali ni vizuri wanapochaguliwa tu kwenye mabaraza basi serikali iwapige *brush* vijana, ihakikishe inaweka Baraza la maadili ili waende sambamba na maadili ya ujana na maadili ya nchi.

Mhe. Spika: Hivi hii *brush* inahitaji ufafanuzi. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nifute neno la *brush* maana huko nyuma Mhe. Spika, sisi vijana tulikuwa tunaambiwa leo mnakwenda kupigwa *brush* kutolewa tongo za macho na masikio kwa Kiswahili cha Wazanzibari.

Mhe. Spika, niseme kweli kwamba nia ya kuwasaidia vijana wetu, wenzangu wameeleza hapa kwamba vijana hawa wanatakiwa wakusanywe kwa pamoja, lakini vijana hawa si kuwadhibiti ni kuwapa uhuru wao jinsi ya kujiletea maendeleo yao katika shehia mpaka Mkoa. Ninaiomba serikali pamoja na kwamba yatakuwa ni mambo ya muda mrefu, lakini ni vyema serikali tukajiandaa kuhakikisha kila Wilaya inatafutwa sehemu ambayo ya kuweza kuwafanyia vijana hawa na maendeleo ya kilimo na kuwaletea maendeleo ya ufugaji maendeleo ambayo ya kujinasua katika shughuli zao za kuleta ufanisi wa kuweza kujipatia chochote. Niiombe serikali ifanye utafiti ili kila Wilaya kutengwe eneo maalumu la kuhakikisha kwamba vijana wetu wanajituma. Si vizuri tukaunda mabaraza haya tukayaachia bila ya kuwapa muelekeo na mstakbali mzuri wa taifa letu.

Lakini jengine kubwa Mhe. Spika, niseme kwamba ni vyema uratibu huu kama wenzangu walivyosema uanze shehia uje Mkoa. Lakini unaanza shehia, unakuja Wilaya na kisha unakuja kitaifa. Kwa sababu tukifanya mabaraza mengi katika Mkoa mmoja tunaweza tukenda kombo. Niunge mkono maneno ya wenzangu ambao wameyasema tuanze shehia, Wilaya ambayo ile shehia ndio tutaunda mabaraza ya Wilaya na Baraza la Wilaya tutaunda Baraza la Mkoa na tunakusudia la kitaifa.

Sasa niseme tu kwamba vijana ni vijana, Mheshimiwa mimi nimeupitia, lakini sikuupitia wote siwezi kusema uongo nitasoma kifungu kwa kifungu. Lakini niseme tu kwamba na mimi niunge mkono maneno ya Waheshimiwa Wajumbe tuwape uhuru vijana wetu wajue namna gani ya kujiendesha wao wenyewe. Si vyema tukaingilia ni vyema tukawafunza kidogo kidogo mpaka tukafikia lengo ambalo tumelikusudia namna gani vijana wetu wawe.

Lakini na mimi nitilie mkazo Mhe. Spika, *tender of education* ni muhimu, kwa sababu mutakuwa na mambo mbali mbali ambayo yanawalenga vijana wenyewe, kuwe na taaluma mbali mbali za vijana. Na humo humo katika yale mabaraza ambayo nilisema kutengwe nafasi maalumu, haidhuru itakuwa ni kwa muda mrefu.Hiyo serikali basi waweze kufunzwa mambo mbali mbali ya kuweza kuwasaidia wao wenyewe.

Mhe. Spika, na mimi nitilie mkazo kwamba watendaji wetu wameisahau saa, saa iko kwa nyuma mbele haipo. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba itabandikwa ili tuweze kuona vizuri mtu anapozungumza kujua ule wakati ambao anatarajiwa azungumze. Lakini na mimi niunge mkono neno moja ambalo ni kubwa na ndilo litakaloweka mabaraza yetu kuhakikisha kwamba yanakwenda sambamba na taratibu na sheria zetu zilizowekwa. Kamati ya Nidhamu, Mheshimiwa, iwekwe wazi ijuilikane ili wende sambamba na taratibu na sheria za mswada.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba lengo si kuwadhibiti, lengo ni kuwawezesha vijana wetu na mimi nalo nilitilie mkazo ili tuwawezeshe vijana wetu hawa kwa matakwa ambayo yamewekwa kwa mujibu wa taratibu na sheria. Na hasa ninavyojua kwamba Mhe. Waziri ambaye kwa kweli ni mmoja anaumia sana katika shughuli zake hizi baina ya vijana, wanawake na watoto na watoto ndio miongoni mwa hao wanakuwa mpaka vijana, ni imani yangu kwamba Mhe. Waziri atakuwa makini katika mswada huu na kuhakikisha kwamba yale yaliyozungumzwa humu basi yanatolewa ufafanuzi mzuri ili tukiondoka humu Mhe. Spika, tuwe kitu kimoja.

Mwisho nirejee tena mabaraza haya Mhe. Spika, kama kuyaua tutayaua sisi wanasiasa, kama kuyajenga tutayajenga sisi wanasiasa, tusijiingize tuwape uhuru vijana wetu ili watupangie mipango yao kwa mujibu wa taratibu na sheria ambayo baadae huu mswada utakuwa ndio sheria ya kuwaongoza vijana wetu.

Baada ya kusema hayo niwatake Waheshimiwa wenzangu tuunge mkono huu mswada ili kuwapa fursa vijana wetu kupambana na mambo ambayo yatamdhibiti kijana, yatamsaidia kijana na yatamuwezesha kijana kufanya mambo ya maendeleo katika taifa hili. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa tuliyoyaonesha, majadiliano yataendelea jioni ambapo tutaanza na Mhe. Wanu Hassan Ameir, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, na Mhe. Amina Idd Mabrouk. Tunategemea michango kwa mswada huu tutamaliza leo jioni na kesho nimuombe basi Mhe. Waziri, aje kufanya majumuisho asubuhi baada ya kipindi cha maswali na majibu.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kuendelea na majadiliano ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya hadi hivi leo kutuwasilishia Mswada huu wa Baraza la Vijana ambapo kwa muda mrefu tulikuwa tukilisubiri Baraza ambalo litakuwa chombo cha sauti ya pamoja ya vijana.

Mhe. Spika, sote tunajua kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukihimiza uanzishwaji wa Baraza hili na mimi binafsi nilikuwa mmoja wa Wajumbe ambao walikuwa wakihimiza serikali kuleta chombo hiki.

Mhe. Spika, naomba nichangie machache ambayo mengine nitapata ufafanuzi na mengine nitatoa kama ushauri kwa Mhe. Waziri ili tuone Baraza hili linatimiza yale madhumuni yake yaliyoanzishiwa.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia katika vifungu vya mswada huu kwanza naomba kutoa angalizo kwa serikali. Mhe. Spika, kumekuwa na uzoefu wa kupitisha sheria hapa za kuanzisha taasisi mbali mbali na baadae serikali huchukua muda kwamba sheria inakuwa imeshakuwepo lakini taasisi ile inachelewa kuanza kazi zake.

Baraza hili tumelisubiri kwa muda mrefu sana, kwa hivyo naiomba serikali baada ya kupitisha sheria hii isichukue muda mkubwa tukawa tunasubiri Baraza hili kuanza kazi. Lakini kwa upande wa vijana wenzangu Mhe. Spika, naomba tutumie chombo hiki ipasavyo ili tuone kwamba Baraza linatoa msaada kwa matatizo ambayo vijana yanawakabili. Pia iwe sauti ya pamoja ya vijana juu ya matakwa yao mbalimbali yanayohusiana na uchumi, kijamii na kiutamaduni.

Mhe. Spika, vile vile, naunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri, wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto na Wajumbe mbalimbali ambao wamesema kwamba Baraza hili liachiwe liwe huru na lisichanganywe likafanywa chombo cha kisiasa. Mimi naunga mkono kama kuna vijana ambao wanahisi wanataka kufanya siasa Mhe. Spika, vyama vyetu vina Mabaraza ya Vijana kwa kila chama. Kwa hivyo, tunawaomba waende kwenye vyama vyao wakafanye siasa huko waache Baraza la Vijana la Taifa la Zanzibar liwe huru ili iwe chombo cha msaada cha kuwakwamua vijana kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Lakini pia nitoe angalizo kwa wanasiasa wasijihusishe na Mabaraza haya. Mhe. Spika, tumezoea kwamba sisi wanasiasa kila sehemu tunatia mkono. Kwa hivyo, nilikuwa naomba wanasiasa wenzangu waliache Baraza liwe huru lifanye kazi zake, likomboe vijana wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, nikiingia katika vifungu nianze sehemu ya nne kifungu cha 10(2), naunga mkono maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kazi ya uchaguzi wa Wajumbe watakaowakilisha vijana wenzao waachiwe vijana wenyewe wakachague bila ya Waziri kuingiza mkono wake. Lakini Wajumbe pia wamechangia na kuonesha wasiwasi juu ya hii mitandao ya vijana itakavyopatikana, kwa sababu ipo mingi, tofauti na haina *umbrella* moja chini yao.

Mhe. Spika, jumuiya hizi vyovyote zitakavyoji-*organize* wachague wajumbe hawa lakini *whatever the case it may be*, namuomba Mhe. Waziri, asitie mkono wake, aache vijana wajichague wenyewe ili ile dhana nzima ya Baraza hili la Vijana liwe la vijana kweli kweli.

Lakini la pili, Mhe. Spika, katika kifungu hichi cha 10(2) kinataja Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa pamoja na wajumbe, wanachama ambao watakuwa ni waalikwa. Mhe. Spika, ninaomba sana sheria hii itambue uwepo wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao wanawakilisha vijana katika Baraza hili. Hii ni kwa sababu itakuwa ni fursa nzuri ya Wajumbe hawa wa Baraza la Wawakilishi wa Vijana kujifunza na kujua ni nini hasa vijana wa taifa hili wanataka na kuwasilisha matakwa yale katika chombo chako hiki kitukufu.

Mhe. Spika, kwa hayo naomba sana Mhe. Waziri, aangalie hilo hata kama hawatokuwa wanachama basi angalau wawe wajumbe wale ambao wanaalikwa na Baraza. Baraza kama Mhe. Hija Hassan Hija, atakavyoona kuwa kuna umuhimu wa kuwaalika wajumbe hawa wawaalike ili waone kwamba wanapata Wawakilishi wao kutoa matakwa yao katika Baraza la Vijana na kuleta katika Baraza hili tukufu.

Nikimalizia kifungu cha 10(2) Mhe. Spika, naomba niingie kifungu cha 14(2)(d), naunga mkono na nampongeza Mhe. Waziri kwa kuzingatia jinsia. Pia nichukue fursa hii kuwaambia vijana wanawake wajitokeze katika mabaraza haya na wagombee nafasi za uongozi kuanzia shehia, wilaya mpaka taifa.

Mhe. Spika, kifungu kinasema kwamba, kuwachagua wanachama saba wa Baraza la Watendaji wa Baraza kwa kuzingatia kwamba angalau wanachama watatu kati ya wanachama saba wawe ni wanawake. Mimi naomba niwaambie wanawake wenzangu vijana kwamba angalau nafasi tatu tuwashitue, nafasi tatu wanazo haki yao lakini ikiwezekana hata zote saba kama wanaweza wazichukue.

Mhe. Spika, pia naomba kama mswada huu ulivyozingatia jinsia naomba na miswada yote mingine ya sheria inayoletwa mbele yetu waige mfano wa

mswada huu, waige mfano wa Mhe. Waziri waone kwamba wanapoleta miswada yao na kunakuwa na nafasi za uongozi wawe wanazingatia jinsia sana, tumechoka kufikiriwa sasa tunataka tutambuliwe rasmi, kwamba miswada ikija kuna nafasi za uongozi kama uongozi wa juu ni mwanamme basi anayefuatia awe ni mwanamke.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba niingie sehemu ya tano vifungu vinavyohusiana na fedha. Vifungu hivi Mhe. Spika, kifungu cha 22(2) nilikuwa naomba ufafanuzi kidogo, kifungu kinasema hesabu za Baraza zitakaguliwa na mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za serikali au mkaguzi aliyethibitishwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu ndani ya siku 20 na baada ya kwisha kwa mwaka wa fedha.

Mhe. Spika, hizi siku 20 naona haiku-*clear* siku 20 zipi, nilikuwa naomba Mhe. Waziri, akija hapa anifafanulie ni siku 20 zipi, lakini pia katika tafsiri ya Mswada huu neno 'Baraza' lilitafsiriwa kama Mabaraza yote ya kuanzia shehia, wilaya mpaka taifa. Swali langu ni kwamba, huyu Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua mpaka zile hesabu za Mabaraza ya Shehia au itakuwaje. Namuomba Mhe. Waziri, akija anipatie ufafanuzi.

Kifungu cha 23(2) kinasema kwamba, fedha zitakazokusanywa kutokana na malipo ya ada ya uanachama zitatunzwa katika *account* maalumu kama itakavyoelekezwa na Baraza, na Baraza la Shehia linaweza kuchukua kiasi kwa ajili ya kuendesha shughuli. Mhe. Spika, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hii kiasi itajwe asilimia ngapi.

Kwa sababu kusema hivi kiasi na kuiacha wazi tu hivi itaachia mwanya kwa wale ambao watakuwa wanaratibu haya Mabaraza katika shehia itatoa mwanya kwa watu kuchota kiasi cha fedha chochote ambacho wanataka na kutumia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hii kiasi iwe asilimia fulani ambayo Mabaraza ya Shehia yanachukua na kutumia.

Mhe. Spika, sehemu ya sita kifungu cha 26 kinachosema Waziri anaweza kwa kushauriwa na Baraza, na kwa kuhakikisha utekelezaji bora wa masharti ya vifungu vya sheria hii bila ya kuathiri masharti ya jumla ya sheria hii, kutunga kanuni kuhusiana na mambo hayo yaliyotajwa.

Mhe. Spika, na mimi naungana mkono na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nafikiri alisema kwamba ni kushauriwa na kukubaliana na Baraza kwa sababu Waziri atapokaa na kutunga kanuni ambazo vijana hawatokubaliana nazo Mhe. Spika, italeta vurugu kweli. Kwa hivyo, namuomba sana Waziri anapotunga hizi kanuni sisi tunampa madaraka yeye akatunge, lakini tunaomba akae na

vijana ashauriane nao na akubaliane nao yale ambayo wanayataka ili kuona kwamba wakati hii sheria itakapoanza kufanya kazi kutakuwa hakuna utata.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja hii na nawaomba Wajumbe wenzangu waunge mkono na waupitishe mswada huu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kunipatia fursa hii, lakini na mimi kabla ya kuanza kuchangia naomba niungane na wenzangu ambao walitangulia kuwapa pole wenzetu ambao walipatwa na msiba hivi karibuni kufiliwa na wazazi wao Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra, lakini pia awajaalie marehemu waliotangulia mbele ya haki awaweke mahala pema peponi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nami naomba nichangie kidogo katika mswada huu na nianze kwenye lengo na madhumuni ya mswada. Lakini kwanza pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuuleta huu Mswada ambao ulikuwa ni kilio cha Wajumbe siku nyingi.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kuundwa Baraza la Vijana ambalo litakuwa chombo chenye mamlaka na hadhi ya juu. Mhe. Waziri, alipokuwa anawasilisha hotuba yake alitueleza vijana wameunda taasisi mbali mbali na kila taasisi ina dhamira yake.

Ni kweli vijana wapo na wako na taasisi zao mbali mbali, lakini mimi nichukue fursa hii kuwaomba vijana hao katika hizo dhamira mbali mbali ambazo wanazo, basi dhamira yao kuu kwanza waelewe kama wao ndio warithi wa nchi hii, kama wao ndio warithi wa nchi hii basi walenge dhamira yao kuu iwe ndio kuiendeleza na kuilinda amani na utulivu ambao upo katika nchi hii ili hayo yote ambayo wanayadhamiria wao kuyafanya yaweze kufanikiwa kwa lengo kubwa sana.

Mhe. Spika, sasa niende katika hivi vifungu vya mswada. Nianze na ukurasa wa 343 kwenye kifungu 3(1). Mhe. Spika, kifungu hichi kinasema kunaanzishwa Baraza la Vijana kwa kifupi itakuwa *ZYC* ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa na mambo haya ambayo yametajwa hapa. Lakini mimi nataka kuongeza kwa sababu hili Baraza kwa hivi sasa litakuwa linapewa ruzuku na serikali, lakini baadae Baraza hili kwa kuwa limetajwa liweze kuwa na mamlaka yake hivyo lazima baadae litatakiwa liweze kujitegemea wenyewe. Kwa hivyo, Baraza hili pia lipewe uwezo wa kuazima fedha ili liweze kuendesha mambo yake na baadae serikali iweze kuwasimamia vizuri ili kwa muda mfupi sana waweze kusimama wenyewe kwa miguu yao.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa huo huo katika kifungu cha 4(4). Hapa kuna kifungu kinasema mwanachama au kiongozi wa Baraza anaweza kusimamishwa au kuondoshwa katika uongozi au uanachama na kamati ya nidhamu kutokana na sababu zifuatazo:-

(a) Kwa uvunjifu mkubwa wa masharti mwenendo na Kanuni za Baraza.

Mhe. Spika, mimi nilitaka niombe hili neno ‘mkubwa’ liondoshwe na ibaki kwa uvunjifu wa masharti. Kwa sababu dhambi yoyote hata kama ndogo huwa inahesabiwa ni dhambi. Kwa hivyo hii ‘mkubwa’ iondoke na ibaki kwa uvunjifu wa masharti.

Nikiendelea nije katika ukurasa wa 344 katika kifungu cha 6(c) ambacho kinaeleza kuwawezesha na kuimarisha mashirikiano miongoni mwa jumuiya zilizosajiliwa na vijana kitaifa, kikanda na kimataifa. Mimi hapa naomba niongeze maneno ‘ambazo zitaendana na tamaduni na silka zetu’.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 345 katika kifungu cha 7, katika kuhakikisha kwamba linafanya kazi zake kiufanisi kwa mujibu wa sheria hii Baraza litakuwa na uwezo. Sasa hii (a) kuajiri watendaji wa Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine yoyote inayohusiana na hayo katika Zanzibar. Mhe. Spika, mimi naomba iainishwe sifa za hao watendaji.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa huu huu kifungu cha 7(f) mimi naomba kiongezeke na kifungu chengine ambacho kiongezwe maneno, pia vijana washirikishwe katika kufanya maamuzi badala ya vifungu hivi vyote viliopo lakini kuongezeke na kifungu hiki.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 347 kifungu cha 10(5) kinaeleza kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa utafanya mkutano wake mara moja katika kila mwaka na mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wote wa mkutano mkuu. Lakini hii 10(6) inaeleza kuwa Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza kufanyika wakati wowote pindi ikihitajika kufanya hivyo.

Kwa kuwa Mkutano Mkuu huwa ni jambo la hasara na gharama kubwa, kwa hiyo hapa lazima waweke ikitokea dharura yoyote maana yake ndio utaweza kufanyika, lakini sio kama uweze kufanyika tu, lakini ikibidi kutokea dharura ya kufanya hivyo basi ndio wanaweza wakafanya.

Mhe. Spika, kwa kweli mchango wangu haukuwa mkubwa sana na nilitaka pia niungane na wale Wajumbe waliosema kama Baraza lianze ngazi ya chini na baadae liende juu katika ngazi ya taifa. Lakini pia Mhe. Spika, hapa kumekosekana ngazi ya mkoa, yaani ukitoka wilaya unakwenda taifa moja

kwa moja, pia mimi ningelishauri ile ngazi ya mkoa wangeliiweka. Tumezoea utaratibu ukitoka katika ngazi ya wilaya unaingia mkoa badae unakwenda taifa, ikiwezekana wangefanya hivyo.

Mhe. Spika, mchango wangu kama nilivyosema ni mdogo kwa hivyo sina budi na mimi kutoa shukurani za dhati kwa Mhe. Waziri, kwa mswada huu, tunaomba kheri na mafanikio mswada huu uweze kupita na iwe sheria ili vijana wetu waweze kufaidika na hili. Lakini pia niwakumbushe wanasiasa wenzangu kwa sababu mswada huu umeeleza wazi kama vijana hawatakiwi kujihusisha na siasa katika Baraza hili ili chombo hiki kiweze kwenda vizuri. Sasa na sisi ndio wanasiasa, na hao vijana sisi ndio watoto wetu, watoto wa ndugu zetu, wajukuu zetu ndio watakaounda hilo Baraza. Kwa hivyo, niwasihi Waheshimiwa wenzangu ili tusiwapandikizie maneno hawa watoto wetu wakaja wakazitumia hizo nafasi vibaya na baadae wakaja wakakosa hizo nafasi katika mabaraza yao.

Mhe. Spika, nilitaka kusema hayo machache na mimi kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi jioni hii kupata fursa ya kusema machache kuhusu Mswada huu wa Baraza la Vijana. Mhe. Spika, mimi kidogo nataka nitofautiane na wengi waliotangulia kusema kabla yangu. Mimi Mhe. Spika, nahesabu au naona mswada huu kama vile umekuja kuongezea mzigo serikali na kumpa mashaka Waziri wa Fedha ambaye sasa atakuwa na jukumu jengine la kutafuta fedha kwa ajili ya Baraza hili ambalo nina wasiwasi pengine Rais wakati wowote atatia saini mswada huu na Baraza hili kuwepo.

Mhe. Spika, kwa nini nasema hivyo? Hivi sasa ninachokifahamu mimi kwamba tunazo jumuiya nyingi ambazo zinawashirikisha vijana, na nathubutu kusema katika Baraza lako hili tukufu wamo Wajumbe ambao wanatoka katika jumuiya hizo za vijana. Sasa ilikuwa najiuliza, je, hizi jumuiya zetu za vijana zilizoko huko katika maeneo yetu zimeshindwa kufanya kazi kiasi kwamba tuweke chombo chengine kitakachokuja kufanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, tukisema kwamba tunataka kuunda Baraza la Vijana na wengine wako, kwa sababu hawa ni watu ambao labda tunawaweka walio na mahitaji maalum, lakini watu walio na mahitaji maalum katika nchi hii sio vijana tu, sasa nina wasiwasi na serikali keshokutwa inaweza kusema kwamba sasa tuunde Baraza la Wazee ili mimi na Mhe. Ali Mzee Ali, hapa na sisi tuingizwe kwa sababu na sisi tuna mahitaji maalum. Sasa kipi kilichosababisha leo kwa vile jumuiya tunazo na nina imani kwamba Wizara

ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ilizitumia jumuiya hizi katika kupeleka uwezeshaji wake, na vijana hao wapo, na nina imani maendeleo yamepatikana kama tunavyokuja tukipewa ripoti katika Baraza lako tukufu. Sasa leo tena tunataka kuanzisha jumuiya nyengine au Baraza jengine ambalo kazi yake itakuwa ni ile ile inayofanywa na hizo jumuiya zetu zilizoko katika sehemu zetu.

Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya kuunda Baraza hili naomba ninukuu inasema kwamba,

> "Ni muda mrefu umepita ambapo vijana wa Zanzibar wamefanya juhudi za makusudi katika kuhakikisha kuwa wanapata nafasi ya kujiunga pamoja, kusikilizwa na kujieleza kuhusiana na mambo yenye maslahi na wao na taifa kwa jumla kwa hivi sasa na kwa wakati ujao"

Haya ndiyo madhumuni ya kuundwa Baraza hili. Mhe. Spika, ikiwa haya ndiyo madhumuni ya kuundwa kwa Baraza hili sasa mambo yao ni mengi na moja katika masharti waliyopewa kwamba wanachama wa Baraza hili hawatakiwi kujishungulisha na mambo ya kisiasa, lakini mimi najiuliza hawa vijana wakishakaa pamoja hayatojitokeza mambo ya kisiasa.

Kwa sababu mimi imani yangu kwamba kila kitu hivi sasa ni siasa, kuna wanachama wengine watadai kwamba mimi ukosefu wangu ni jambo fulani, hata hizo ajira ni imani yangu watarudi serikali watasema vijana hawapatiwi ajira kwa hivi sasa, kusema hivyo Mhe. Spika, ni tayari umejiingiza katika siasa sababu tunasema siasa ni uchumi na uchumi ni siasa.

Sasa leo moja katika vifungu vinakataza shughuli hii, sasa hili Baraza litafanya kazi vipi kiasi kwamba lisijiingize katika siasa. Kuna baadhi ya vijana Mhe. Spika, wamekosa haki zao za msingi za kikatiba za kuwa wao wanatakiwa wapewe haki ya kitambulisho cha cha ukaazi kujulikana kwamba wao ni Wazanzibari. Bila shaka wao watakapofika katika majukwaa yao hili litakuwa ni moja kati ya changamoto, sasa sheria ya Baraza hili inakataza usijishughulishe na siasa lakini yeye itakuwa ndio changamoto yake kwa wakati ule.

Mhe. Spika, hapo mimi siungi mkono kwa hilo, kwa sababu Baraza hili ni lazima moja kwa moja litajihusisha katika suala hilo. Kwa sababu mambo ambayo yanamhusu kijana pia siasa imo leo vipi tunaweka sheria inayosema kwamba Baraza hili la Vijana lisijihusishe na mambo ya kisiasa, hapo ni kinyume. Mhe. Spika, naomba tuangalie tena.

Nikiendelea Baraza ninavyofahamu mimi linatakiwa liwe huru, yaani *independent*, lakini muundo wake hivi sasa unanishangaza mimi kusema kwamba Baraza litachangiwa watu ambao watateuliwa na serikali kwenda kufanya nini. Bila shaka kwenda kushawishi. Kwa nini tufanye hivyo, mimi nafikiri kama tumekusudia Baraza liwe ni Baraza basi watu hawa hawana umuhimu wa kuingia kule, kuingia kwao kutakuwa kuna maana maalum. Kwa hivyo, liachiwe lifanye kazi wenyewe, hakuna haja ya kupeleka watu ambao watakuwa na ushawishi tena watu ambao watatoka serikalini.

Mimi ni imani yangu kwamba mabaraza kama haya huko ulimwenguni yanafanya kazi pia ya kuikosoa serikali, sio kazi ya kusubiri serikali imewapa pesa wazitumie basi, aa, wao pia wanafanya kazi *as a pressure group* kuona kwamba hivi sasa serikali inakwenda hivi, sisi tuishauri hivi au twende kinyume na hivi, sio kusubiri tu wakawa wao ni *received*, sisi tunasubiri maagizo ya serikali sio hivyo.

Sasa kwa hivyo, kwa muundo huu wa Baraza maana yake Mhe. Spika, hili Baraza litakuwa halina mamlaka ya kufanya kazi wenyewe, kwa hiyo umuhimu wake wa kuwepo mimi naona turejee kule kule kwenye jumuiya zetu tuziwezeshe kama tulivyopanga kuziwezesha baadae tuangalie matunda yake, lakini kwa kuja kuipa tena serikali mzigo mimi siungi mkono.Waziri wa Fedha sasa itabidi ajipange vyengine kuwatafutia watu hawa fedha na kazi watakayoifanya ni ile ile, kwa sababu wao tushawakataza wasijiingize katika baadhi ya mambo na hayo ndio yanayowakera katika maendeleo yao.

Mhe. Spika, mimi yangu yalikuwa ni hayo na nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kukutana hapa tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Spika, lakini pia niombe radhi kwamba sauti yangu haitokuwa nzuri kwa sababu ya mafua. Kwa hivyo, kama itakuwa haitoki basi kutosikilikana vizuri, naomba radhi.

Mhe. Spika, lakini nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo ili na mimi niwe mmoja ya wachangiaji wa mswada huu. Mhe. Spika, nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kukushukuru na kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kuleta mswada huu muhimu sana kwa vijana wetu na watoto wetu. Sote ni mashahidi tulikuwa tunapigania suala hili tokea kipindi kilichopita...

Mhe. Spika: Hebu Waheshimiwa hizo simu tuweke sawa, nafikiri kuna simu inatutaabisha kidogo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, kama tunavyokumbuka katika kipindi kilichopita mimi ndio nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Wanawake na ilikuwa mara kwa mara tulikuwa tunamsisitiza Mhe. Waziri, lini utaletwa mswada wa uundwaji wa Baraza la Vijana, kwa sababu inaonekana kwamba vijana wetu bado hawajapata pahala maalumu pa mkusanyiko ili waweze kuzungumza mambo yao ambayo yanahusu vijana. Lakini leo Mhe. Waziri, ametuletea mswada huu kwa kweli sisi sote tunamshukuru sana.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo basi sasa naomba niingie moja kwa moja katika mswada huu. Naamini kwamba Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake walikuwa makini katika kuandaa mswada huu na unaonekana kwamba mswada huu upo kamilifu hauna kasoro nyingi. Kwa hivyo, naamini kwamba sitokuwa na mchango mkubwa katika mswada huu.

Mhe. Spika, mimi basi niingie katika Sehemu ya Nne ya mswada huu kuhusu "Muundo wa Baraza". Mhe. Spika, kwenye sehemu hii ya Nne inayoelezea muundo na vyombo vinavyounda Baraza. Nahisi mimi kwa mtizamo wangu ingefaa kwamba sheria kuhusiana na muundo huu wa Baraza, suala la kuanzisha idara ambazo zitakuwa zinaeleza suala zima la mabaraza haya.

Katika mswada huu Mhe. Spika, Mabaraza haya ya vijana, idara imeonekana imekuwa tu katika mswada huu, lakini haikuainishwa kwamba Mabaraza haya yatakuwa na idara. Ni vyema basi katika mswada huu ingeonesha wazi kwamba itakuwa na idara mbali mbali ambazo zitashughulikia Mabaraza haya.

Lakini jengine Mhe. Spika, niingie katika suala zima kwenye kifungu cha 3 (2) imesema kwamba, "Baraza litakuwa na mpangilio wa muundo wa Baraza la Vijana taifa, Baraza la Vijana Wilaya na Baraza la Vijana Shehia. Lakini kwenye kifungu cha 10 (2) (a) mswada unasema, "mkutano mkuu wa taifa miongoni mwa wajumbe wake ni mwenyekiti wa Baraza la Vijana Mkoa".

Mhe. Spika, mimi nadhani kutajwa kwa mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Mkoa, kama haikuwa kwa makosa basi panahitajika marekebisho au ufafanuzi kwa vile kwa mujibu wa kifungu cha 3 (2) "Hakutokuwa na mwenyekiti wa Baraza la Mkoa". Lakini hapo hapo kwenye mpangilio huo ningependa kujua sababu zilizomfanya Waziri asiweke kwenye mswada huu mapendekezo ya Mabaraza kwenye ngazi ya taifa, Mkoa, Wilaya na Shehia na badala yake kuruka Mkoa.

Mhe. Spika, nije katika suala linalohusiana na sifa za umri za wanachama kwenye tafsiri. Mswada unasema ni miaka 15 hadi 35, lakini kwenye kifungu 4 (5) (b) mswada unasema, "Mwanachama au kiongozi atasita kuwa mwanachama au kiongozi akifikia umri wa miaka 35 au zaidi. Nadhani Mhe. Spika, kifungu hicho cha 4 (5) (b) kinahitaji kuwekwa sawa kwa kuandikwa kwamba, "kwa kupindukia miaka 35", kwa sababu kwa mujibu wa tafsiri miaka 35 ni kikomo cha uanachama au uongozi lakini bado mwanachama au kiongozi atakuwa na sifa mpaka pale atakapopindukia umri huo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa kwa sababu Mhe.Waziri, amezungumzia kila kitu, lakini niliona kwa kuwa na mimi ni mdau wa mswada huu, kwa vile na mimi nimetokea vijana ijapo ninaelekea kuwa mzee, kwa hivyo nikaona kwamba na mimi nitoe maoni yangu Waziri kama itawezekana basi ni muhimu sana kuyazingatia, lakini hasa hili suala la uundwaji wa idara, japo kwamba katika mswada si lazima aandike kama kutakuwa na idara hii na hii ambazo zitashughulikia, lakini ioneshe, kama haijaonesha katika mswada huu basi tutakuwa hatuna pahala pengine pa kutia suala hili.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ambayo tunaendelea nayo. Kwa kweli sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo hapa katika Baraza hili tukufu
tukiwa wote salama na kwamba wote tukiwa tumetimia, naweza kusema tupo *full team,* hakuna mtu ambaye amepungua. (*Makofi*).

Kwa kweli sina budi kuwaombea kila la kheri wazee wa wazee wetu kama Dr. Sira ambaye amefiliwa na mama yake na Mwanapinduzi Saleh kwa kufiliwa na mzazi wake wa kumlea. Sina budi kuwaombea kila la kheri Mwenyezi Mungu awaweke mahala pema.

Vile vile, kumuombea shujaa wetu wa Afrika Mhe. Nelson Madiba Mandela, Mungu amuweke mahala pema peponi. (*Makofi*).

Kwa kweli leo Mhe. Spika, sitokuwa na mengi sana ya kuchangia mchango huu isipokuwa kumpa hongera Mhe. Waziri kwa wakati mzuri wa kuuleta mswada wake na tukaweza kuuchangia kwa pamoja katika Baraza hili.

Kwa kweli Baraza la Vijana ni jambo zuri sana ambalo tulikuwa tunalihitaji muda mrefu kwamba lifike ili tuweze kulichangia kwa pamoja na kuweza

kuwapa nafasi vijana na wao waweze kuwa na Baraza la kuweza kuchangia mawazo yao kwa vijana wenzao. Nikiangalia kwenye ukurasa wa 4 (1) Wanachama wa Baraza kwanza uwe huru, uwazi kwa vijana wote kupitia Mabaraza ya Vijana na Shehia zote.

Mhe. Spika, mwanachama wa Baraza atakuwa na haki ya kutoa maoni na mapendekezo na kushauri kwa Baraza bila ya ubaguzi ama ukabila ama rangi ama elimu aliyonayo Barazani. Kwa kweli Mhe. Spika, wachaguliwe vijana waaminifu na wakweli wanaojua kusoma na kuandika, isiwe kama tulivyochangia kwamba Baraza hili liwe na digrii na diploma, hapo tutaanza kuwabagua vijana na kuwaweka kama hawapo pamoja. (*Makofi*).

Kwa kweli tukiteuwa vijana ambao wana busara, vijana hawa wasiwe na jazba za kushawishiwa na viongozi wa siasa wenye hamu ya madaraka. Mimi pamoja na Jimbo langu la Koani napendekeza uongozi mzima wa vijana ili kutunza nidhamu na vijana wetu waweze kuliwezesha Baraza hilo kujikimu kimaisha na vijana lazima wapatiwe mafunzo na historia ya nchi hii, waelewe madhumuni ya Baraza la Vijana, kwa vile mswada umeletwa na wizara ni vyema wizara hii ikaongozwa na mwenyewe Waziri ambaye anahusika na mswada huu. (*Makofi*).

Kwa kweli vijana wetu Mhe. Spika, si kweli kwamba wana nafasi peke yao ya kujiongoza bila ya kuongozwa, ni kama vile tulivyopata maelekezo kwa Baba wa Taifa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Aman Karume, ambaye alichangia sana serikali yetu kutufahamisha iende vipi. Kwa kuchangia Baraza la Vijana kwamba liwe na wasomi za digrii na diploma peke yao, hiyo ndio chanzo cha kuwagawa vijana wetu (*Makofi*).

Jambo muhimu Mhe. Spika, tufuate wasia wa Baba wa Taifa Mzee Abeid Aman Karume, aliyetoa wakati wa uhai wake, na hivi sasa kila wakati asubuhi huwa *ZBC* inatoa hotuba zake inasema kuanzia darasa la sita mwananchi anaweza kuongoza serikali, na kweli nimechunguza usemi wake ni wa kweli, kwa sababu hadi sasa hivi ninapozungumza serikali inaongozwa na wazee na vijana walioanzia darasa la sita na sio digrii na diploma peke yao. (*Makofi*).

Kwa kweli tukifuata wasia wa Marehemu Baba wa Taifa, taifa letu litakwenda linavyotakiwa. Lakini tukifuata mambo yanayokuja ya siasa na ushabiki wa kisiasa kwamba vijana wetu tuwatenge wenye masomo ya madarasa madogo, kwa kweli tutakwenda ambapo sipo alipotufahamisha Baba wa Taifa. (*Makofi*).

Kwa nini iwe ni digrii na diploma ni kuliangamiza taifa. Nikisema hivyo wenzangu ambao wamechangia kwamba vijana wetu ambao tutawapendekeza kuwa waingie katika Baraza hili la vijana wawe na digrii na diploma, naona wamekosea sana. Kwa sababu wangelikosoa kwanza hili Baraza letu tuliomo humu ndani kwamba sijawaona wenye digrii na diploma. Hata mwenyewe aliyechangia pengine ana darasa lake *form four* au *form six* na wengine tuna darasa la saba kwa kusoma na kuandika tunaongoza Baraza hili ambalo ni Baraza tukufu linalostahiki kuwepo katika nchi yetu. Kwa kweli kuchangia kwamba vijana wenye digrii na diploma kwa kweli tutarudi nyuma hatua kubwa sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kweli hivi sasa tukitaka Baraza letu lihakikishe kwamba linaongozwa na wazee, halafu vijana ndio wawe mbele katika kujiongoza, hivyo tutafika katika sehemu ambayo tuliyokusudia. Hapo hapo Mhe. Spika, ninahakikisha kwamba tuchague vijana ambao waingie kwenye Baraza hili, tukihakikisha kwamba vijana wanaoingia humu ni wale wenye nidhamu ambao ni vijana waliokuwa na ukweli na ambao ni vijana wamesoma na kuandika inatosha kwamba Baraza hili litajiongoza hadi kufikia muda wake wa kujiongoza baadae mbele.

Lakini kwanza ni lazima tuhakikishe kwamba Baraza hili linaongozwa na Mhe. Waziri aliyetoa mswada huu ili vijana waongoze kwanza ndio waweze kujiongoza katika Baraza lao.

Mhe.Spika, kwa kweli mimi sitokuwa na mchango mkubwa sana, isipokuwa ninahakikisha vijana ambao wataingia katika Baraza hili ni vijana wale ambao tumekusudia na wasiokuwa na jazba katika maamuzi yao, mazungunzo yao na katika maamuzi ambayo watayaamua kwenye Baraza hili.

Kwa kweli Mhe. Spika, mimi na Jimbo langu la Koani naunga mkono hoja kwamba Baraza hili liweze kupitishwa na liweze kujiendeleza katika shughuli zake za Baraza. Ahsante sana Mhe. Spika (*Makofi*).

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kwanza kumshukuru Allah kutujaalia jioni hii tukawa tupo wazima wa afya na kuweza kuendeleza majukumu yetu haya kwa raha mustarehe.

Lakini pia, na mimi niwape wenzetu mkono wa pole wale waliopata misiba ya kufiliwa na wazazi wao na Mwenyezi Mungu awajaalie wazee hao awaweke mahali pema, *Amin.*

Mhe. Spika, sina budi na mimi kuishukuru na kuipongeza serikali kufikiria na kutoa maamuzi kuona kwamba ipo haja kuwa na chombo hiki cha vijana wa

Zanzibar, kuendeleza na kusimamia majukumu yao ya dhati yanayowakabili katika nchi yetu. Kwa hivyo, natoa pongezi zangu za dhati kabisa kuweza kufikiriwa hili na leo hii ikawa tumo katika kuijadili na kuichangia sheria hii ili kutia nyama tu baadhi ya maeneo ili kuifanya hii sheria isije ikaleta utata mbele ya safari tunakoelekea.

Mhe. Spika, na mimi kwa upande wangu natarajia kwenda kifungu baada ya kifungu ili nisitoke nje katika sheria hii.

Mhe. Spika, na mimi nianze katika ufafanuzi kifungu nambari 2 pale, suala zima maana ya Baraza. Nikubaliane na wale waliosema kuanza taifa, wilaya, Shehia, kwa kweli sio utaratibu.

Utaratibu wa kukwea ni kuanza kwenye shina. Kwa hivyo, tuanze Shehia, wilaya na taifa lakini tukianza kutoka kileleni, basi siku zote huko juu ndipo kwenye mengi, mara nyingi huku kati na chini kunasahaulika. Kwa hivyo, ni vyema tukawapa uzito watu wa Shehia na Mawilaya, halafu tukaangalia na huku juu. Kwa sababu huko juu hakutokuwa kama wanachama hawakutoka huko kwenye Mashehia, ndio tukafika kwenye Mawilaya na taifa. Kwa hivyo, ni vyema tukaipa hadhi sheria hii kuyajali zaidi Mashehia na Mawilaya.

Lakini tukija katika neno vijana, vijana tunaambiwa maana yake ni mtu mwenye umri baina ya miaka 15 na 35. Hapa Mhe. Spika, katika sheria nyengine tunaambiwa kijana ni yule aliyefikia umri wa 18, ana haki ya kuchagua. Lakini hapa kijana ameanza na miaka 15. Pia, na mimi katika wale waliomba ufafanuzi, na mimi ni mmoja wao ninahitaji kupata ufafanuzi wa kijana huyu aliyeanzia na miaka 15.

Kijana huyu tukimpeleka kwenye sheria ya Mzanzibar Mkaazi hana haki ya kupata kitambulisho cha Ukaazi, kwa sababu hajafika umri wa miaka 18. Na pengine katika sheria hii mambo haya ya vitambulisho yatakuwa yanazingatiwa sana. Je, kijana huyu ambaye amekaa kama nanga ya saa, hayupo huku wala huku. Sijui sheria hii imempa nafasi mahali gani pa kuweza kupata haki zake.

Kwa hivyo, hapa na mimi nahitaji kupata maelezo. Lakini pia na haya maelezo yaliyoandikwa umri baina sio neno la Kiswahili, hili ni neno la Kiarabu. Kwa hivyo, tungetafutiwa neno la Kiswahili hapa mukatuwekea, tukajua kwamba baina ya miaka 15 na 35, kidogo hapa sheria itakuwa inatukwaza huko mbele, kwa sababu kila kukicha Kiswahili kinakuwa. Kwa hivyo, tungeliambiwa kati ya miaka 15 hadi 35, kidogo sheria hii ingelitupa ufasaha kabisa. Kwa hivyo, naomba sana hapa Mhe. Spika, Mhe. Waziri, atakapokuja aje atupe ufafanuzi wa maana hii ya kijana.

Lakini pia, Mhe. Spika, nikubaliane na wale ambao waliosema kwamba mualikwa kiofisi, maana yake ni wageni waalikwa ambao watatokea katika taasisi za serikali kuhudhuria katika mkutano wa Baraza. Mhe. Spika, hapa hatujawa huru, hatujawapa uhuru vijana. Vijana wataingiliwa kati mno na waalikwa hawa na tumetoa taasisi moja tu ya serikali. Kuna taasisi za watu binafsi hazikupewa haki hii. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na wale waliosema kwamba hawa hii taasisi ikuzwe hapa, kuna watu mashuhuri hawakupewa nafasi ya kualikwa. Kwa hivyo, itakuwa bado vijana tumewabana. Kwa hivyo, kama tunataka sheria hii ya kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar tuwe huru na tuwape uwazi kabisa, wafanye mambo yao wazi kabisa kuliko kuanza kubanabana. Na ndio utakuta Mhe. Spika, kuna sheria zinazobanwa zimefika miaka kumi na kumi na tano, sheria hiyo haijafanya kazi kwa sababu imebanwa sana haipo wazi.

Kwa hivyo, kila tukienda tusirudi nyuma, kila tukienda twende hali ya kuwa wawazi katika mambo yetu ya kiserikali. Mimi hili sikubaliani nalo Mhe. Spika, kwamba waalikwe watu hao tu. Ni vyema tafsiri hii ikakuzwa ili kila vijana wanaowaona wana haki ya kuwaalika wakaweza kuwaalika katika mikutano au katika vikao vyao.

Lakini Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 4 (2), kuna maneno yanayosema kwamba, "kijana yeyote" kwa bahati nzuri kamati iliona wakaingiza neno "Mzanzibari" kijana yeyote Mzanzibari anayakubali malengo ya Baraza anaweza kuomba uanachama kwa kujaza fomu ya maombi ambayo itatolewa na Baraza la Vijana Shehia.

Mhe. Spika, nimejaribu kutafuta ufafanuzi wa neno Mzanzibari hakuna. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri, atupe tafsiri ya neno "Mzanzibari". Kwa sababu Wazanzibari wapo wa aina nyingi. Kuna Wazanzibari, kuna Wazanzibari Wakaazi, sijui kuna Wazanzibari gani. Naomba tupate ufafanuzi wa neno "Mzanzibari" ili huyu kijana yeyote ule Uzanzibari uweze kutambuliwa tujue nani Mzanzibari aliyekusudiwa hapa.

Mhe. Spika, kifungu cha 10(3) pale kimeelezea mkutano mkuu wa taifa utakuwa na wanachama wafuatao waalikwa ambao hawatokuwa na haki ya kupiga kura. Mimi nakubaliana na wale waliosema kwamba kifungu hiki kifutwe. Hawa watakuja kuwakwaza vijana wetu. Mtu anaweza kuja pahali akakosa kusema neno hata moja, lakini akapiga kura na kura yake ikaleta ufanisi. Lakini mtu anaweza kukiingia kikao akachangia kikao kile watu wote wakavutika na maneno yale, hatma yake ufanisi wake wa kazi ukaja ukakorofisha huko mbele.

Kwa hivyo, kwa hawa watu waliotajwa, Katibu Mkuu wa wizara, huyu pengine ni mtu mkubwa na msomi mkubwa, pengine mkutano ule anaweza akauhodhi yeye peke yake, Mkurugenzi wa idara anaweza kikao kile akakihodhi peke yake na watendaji wawili wa serikali ambao wataalikwa kutokana na utaalamu wao, jamani bado vijana tuwapeni haki yao bwana, wao wenyewe waangalie nani tumualike katika vikao hivi, kuliko kuanza kuwapangia, tutakuja kuwakwaza vijana.

Halafu tuone kwamba vijana wamepewa kazi lakini kazi ile imewashinda. Hebu tujaribuni kuwapa uhuru waweze kutoa mawazo yao na waweze kuangalia nani anaweza kulisukuma Baraza lao la Vijana. Kwa hivyo na mimi nakubaliana na wale waliosema kwamba kifungu hiki tukitoe basi ipo haja hiyo ya kuweza kukitoa.

Lakini pia, katika kifungu cha 10 (e) pale, wale vijana wawili wanaowawakilisha vijana wenye ulemavu. Hiki kifungu kinaambiwa kwamba wateuliwe na Waziri. Kwa nini ateue Waziri na tumeunda Umoja wa Walemavu na huu umoja upo na unasimamia shughuli hizi za walemavu.

Kwa nini Waziri asipelekewe majina yanayotokana na huu Umoja wa Walemavu akateua katika majina pengine yanayotakiwa wawili angalau Umoja wa Walemavu wakapeleka majina manne yanayoangalia jinsia pengine mmoja awe mwanamke na mmoja mwanamme; majina manne yale Waziri akaweza kuyateua majina mawili, akiwemo mmoja mwanamke na mmoja mwanamme. Kulikoni kukawa hakuna mawazo ya vijana, mawazo ya uteuzi yote akayachukua Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, na hili naliomba tulifanyie liwe lina utaratibu wake ili vijana waone ule uhuru wa chombo chao. Kwa hivyo, hilo naliomba sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikija kwenye kifungu hicho hicho cha 10 (5). Nahisi kifungu hichi kidogo cha (5) vingelisemea vifungu vyote vinavyohusu mikutano mikuu. Mkutano Mkuu wa Taifa utafanywa mkutano wake mara moja katika kila mwaka, na mkutano huo utahudhuriwa na wanachama wote wa mkutano mkuu. Mimi mawazo yangu hapa nimeona kwamba kuna baadhi ya mikutano haitoweza kufanyika.

Kwa sababu ukisema mkutano mkuu ufanywe na wanachama wote, siku nyengine wengine hawatokuja, pengine watadharurika wawili au watatu. Lakini sheria imeelekeza kwamba wote, kwa hivyo watu watarudi kwamba *quorum* haijatimia, hatuna akidi yoyote iliyosema kama ni theluthi mbili au tatu au zaidi, pamezungumwa wanachama wote wa mkutano ule. Kwa hivyo,

tukisema watu wote ni kuanzia mmoja mpaka mwisho wa wale wahusika, akikosa mmoja ni kwamba hao sio wote.

Kwa hivyo, suala hili naomba Mhe. Waziri nipate ufafanuzi, hiyo wote ni wote au vipi, ili hiyo mikutano ije iweze kwenda vizuri na ili vijana wasije wakakwazwa huko mbele. Kwa hivyo, ili mikutano ije kuwa huru na iweze kufanyika basi tunaomba kupata maelezo katika suala hili, kwa sababu wachangiaji wote waliopita akidi ya mkutano hapa bado haijazungumzwa.

Mhe. Spika, kuna kifungu cha 14(c) kinaeleza kwamba;

Kifungu cha 14(c)

> "Afisa wa vijana wa wilaya kwa nafasi yake kiofisi ambae atakuwa ni sekretari wa Baraza la Vijana Wilaya"; na wengine

Mhe. Spika, mimi hili siliungi mkono kwa sababu hivi sasa maafisa wengi wa wilaya ni watu wanaozidi miaka 35 lakini pia bado haya mabaraza tutakuwa tunayadhibiti ndani ya serikali, hawako huru. Huyu afisa akitoka pale atapeleka ripoti hizi wapi, atapeleka ripoti zake katika wilaya na hiki chombo kinaambiwa kiwe siri kweli kweli na huru. Kwa hivyo, mkutano haujamaliza afisa wa wilaya keshamuambia afisa wa mkoa, afisa wa mkoa keshamuambia afisa wa wizara.

Sasa ni vyema nafasi hii wakati katika kifungu cha 7 huku kinasema kwamba katika kuhakikisha kuwa linafanya kazi zake kiufanisi kwa mujibu wa sheria hii, Baraza litakuwa na uwezo wa kuajiri na mambo mengine. Sasa kwa nini hizi nafasi wasiachiwe wenyewe wakaajiri maafisa wao, kwa nini wizara waingilie kati, itakuwa hatujawatendea haki vijana. Ni vyema hiki chombo kiwe huru, kiweze kusimamia majukumu yake, kuliko kiwe kinaingiliwa katika majukumu yake na wizara.

Mhe. Spika, kifungu cha 17(1) kinasema;

> "Mkutano Mkuu wa Shehia utajumuisha wanachama wote wa Baraza wanaoishi katika Shehia"

Mhe. Spika, hapa kidogo napata kikwazo kidogo, hii sheria imeshatangulia. Lakini hivi sasa tukiangalia haya mabaraza ya shehia bado hayajakuwepo. Ama baada ya kushatiwa saini huu mswada na haya mabaraza kuanza kutafutwa pengine mwakani hii sheria itafanya kazi yake vizuri.

Lakini huu muda tulionao, hii mikutano watakaoiratibu na kuisimamia ni nani, kwa sababu katika hii sheria hatujaona nani kapewa majukumu ya kuwakusanya hawa vijana wakaweza kufanya mikutano yao katika mashehia. Kama ni sheha wa shehia ile basi ni vyema tukapata utaratibu tukajua kwamba sheha ndiye atakayekuwa mratibu wa mambo haya. Kwa hivyo, pia naomba kupata ufafanuzi katika suala hili la kuratibu mikutano ya shehia.

Mhe. Spika, naona unaniangalia sana. Mimi ningeomba sana Mhe. Spika, kwamba sheria ni msumeno, unakata sawa sawa, na sheria haijiendeshi inaendeshwa na kama sheria tulizonazo hapa Zanzibar zinajiendesha basi ingekuwa saa hizi nchi imetulia kweli. Kuwa na sheria nyingi sio ufanisi kabisa. Ufanisi wa sheria ni usimamizi na utekelezaji.

Mhe. Spika, mimi huu ni mwaka wangu wa tatu wa Baraza hili, kila vikao vya robo basi tunafanya vikao tunajadili sheria, ama tatu, tano au nne. Lakini ufanisi bado sijauona. Mimi nilipoingia hapa kulikuwa kuna sheria ile ya wapandaji vespa wavae *helmet*. Ama siku chache hii sheria ilisimamiwa kweli kweli. Lakini hivi sasa imekuwa ni jambo la kawaida watu wanapita njiani na askari wapo wala habari watu hawana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kuwa na sheria nyingi tutajaza mafaili kibao, lakini haitotoka sheria ikenda kusimamia jambo, sheria inasimamiwa.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote nichukuwe fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia leo kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuendelea na shughuli zetu ambazo zimetuleta pamoja na kuwa tumetumwa na wananchi kuja kuwawakilisha.

Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika mswada wa Baraza la Vijana ambao uko mbele yetu. Lakini Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuchangia, naomba uniruhusu na mimi niungane na wenzangu kwa ajili ya kuomboleza kifo cha mkombozi, shujaa na muasisi wa Kiafrika ndugu yetu Nelson Mandela, amewacha urithi mkubwa katika taifa la Afrika pamoja na dunia nzima. Ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema anapostahiki.

Mhe. Spika, vile vile napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na watendaji wake wote wa wizara, ambao kwa kweli wao ndio waliofanikisha katika kuuleta mswada huu mbele yetu.

Mhe. Spika, mimi kama mwenyekiti wa kamati inayohusika na wizara hii ninatoa pongezi maalum kwa Mhe. Waziri, kwa sababu Mhe. Waziri, alituahidi na ametimiza ahadi yake. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri, mbali na mswada huu, tumeweza pia kuona maendeleo na mambo mbali mbali ambayo Mhe. Waziri, amekuwa akiyafanya katika wizara hii.

Mhe. Spika, mswada huu uliokuja mbele yetu ni mswada ambao una nia na madhumuni mema kwa vijana wetu wa Zanzibar, na hilo tumeliona kwenye madhumuni ambayo yamejieleza katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha muda mrefu vijana wetu walikuwa, naweza kusema walikuwa hawana pahala pa kwenda kukutana, kukaa na kuzungumzia mustakabali wao. Kwa hivyo, mswada huu Mhe. Spika, ni mswada ambao umekuja kwa ajili ya kumkomboa na kumsaidia kijana wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, sisi kamati tulijaribu kuona mengi, nawashukuru na kuwapongeza sana wajumbe, kwa kweli mengi ambayo kamati waliyoyaona katika mswada huu ndio yale ambayo yamejitokeza kwa wajumbe mbali mbali. Mimi niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa makini katika kuutizama mswada huu.

Mhe. Spika, mimi nataka kuzungumzia mambo machache, kwa kuwa tayari nimeshatoa maoni yangu katika mswada huu.Kwa hivyo, mimi sioni umuhimu wa kuanza kuuchambua mswada katika vipengele vyake vilivyokuwemo. Lakini Mhe. Spika, nataka nitilie mkazo kwa kusema machache ambayo yamezungumzwa na wajumbe wengi.

Mhe. Spika, suala la kuwemo siasa ndani ya Baraza. Kwa kweli mimi naipongeza sana wizara kwa kuona umuhimu wa kutoa masuala yoyote yanayohusu siasa katika Baraza hili. Ikiwa itaingia siasa ndani ya mabaraza hayo, basi Mhe. Spika, nina hakika mabaraza hayo hayatoweza kufanyakazi zake kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, kuna wajumbe wengine hapa wamesema siasa ni kila kitu. Mhe. Spika, siasa sio kila kitu, siasa ni mfumo ambao unaweza kutumika katika kuwafikisha jamii fulani katika malengo fulani. Lakini inaweza ikawa siasa mbaya, Mhe. Spika.

Ndio maana dunia ya sasa hivi kutokana na siasa mbaya tunaona kwamba watu wanapigana na kuzozana. Baraza hili la vijana litaweza kuwasaidia vijana katika masuala yao muhimu, hili sio Baraza la kutengeneza siasa.

Vijana hawa kwa bahati nzuri sana Mhe. Spika, tumekaa nao na baadhi yao walisema kwamba kwa nini siasa imetolewa, wakajenga hoja.

Lakini kwa bahati nzuri sana kwa sababu vijana hawa ambao ndio walikuwa wadau wa mswada huu ndio waliouchangia vizuri sana, mimi nawapongeza sana vijana hawa. Wamesema wenyewe kwamba imeshafika wakati siasa tuziweke pembeni tutizame mustakabali na ustawi wa vijana wa Kizanzibari, hilo ndio muhimu, wenyewe wamesema mkianza kutia siasa ndani ya Baraza hili basi mtawatenga baadhi yao na yale ambayo yanawahusu makundi hayo Mhe. Spika, wanasema hawajui watakwenda wapi. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana wizara kwa kufikiria kupinga siasa ndani ya Baraza la Vijana.

Mhe. Spika, mimi nilipata bahati kidogo ya kutizama kwenye mtandao ili kujifunza mabaraza ya wenzetu. Kwa bahati nzuri sana nimegundua hamna siasa, mabaraza mengi yao miundo yake ni kwamba siasa wameweka pembeni, yamewahusisha vijana kuweza kuzungumza mambo ambayo yanawahusu vijana, yanazungumzia kuwatayarisha vijana kuwa raia wema, kujua maendeleo ya nchi yao na anapofikia umri wa kufanyakazi kuweza kupata ajira, na masuala ya kujitolea.

Tulichokiona Mhe. Spika, na ambacho nafikiri Mhe. Waziri, atakitilia maanani ni suala zima la vijana kutumia mabaraza haya kuwa kama ni *platform* ya kufundishwa uongozi. Uongozi ambao ndani yake hauna siasa. Hilo tumeliona kwamba ni muhimu na ningemuomba sana Mhe. Waziri, waliangalie kwa kina, kwa sababu mabaraza haya hasa ndio lengo lake, tunawatayarisha vijana kwa ajili ya kuwa raia wazuri.

Lakini suala jengine Mhe. Spika, ni suala zima la umri. Wajumbe wengi walikuwa wana wasi wasi kwamba umri wa miaka 15 hadi 35 na hasa umri wa miaka 15, walikuwa na wasi wasi nao sana. Mimi nilikuwa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wamfikirie huyu kijana mwenye umri wa miaka 15 ambaye bado tunamwita mtoto mpaka kufikia umri wa miaka 17.

Lakini huyu tukimuacha tusimlee tukamuweka kwenye Baraza ambalo na yeye anajitayarisha kuingia katika kundi lile tukamuachia atakwenda wapi. Kwa bahati nzuri sana vijana wetu sasa hivi wenye umri wa miaka 15 wanakua haraka, wana mambo yao na wao wanataka yajulikane, na yazungumzwe.

Vijana hawa watakuwa na *platform* ipi ya kuzungumzia masuala yao ikiwa leo tunasema hawa sio. Hawa ndio, wawemo na wao ili waweze kujifunza

kutoka kwa wakubwa wao, lakini wawemo kwa hoja kwamba watoto wa umri huu wengi wao wengine wanamaliza kidato cha pili wanakuwa hawana cha kufanya. Mzigo tunaowaachia wazee ni mkubwa, lakini leo wakiwa na jukwaa lao, na wao watajiona kwamba wanatambulika katika kundi hili. Mhe. Spika, mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe watafakari hilo.

Mhe. Spika, najua mswada huu kwenye suala la umri umeangalia mambo mbali mbali ikiwemo na mikataba ambayo kwa Tanzania tumefunga. Kwa hivyo, umri ule sio jambo geni kwamba umeingia katika mswada huu. Umri ule ni umri ambao umekubalika kimataifa. Suala la kuwa kijana yule bado hajatimia kupata kitambulisho au kupiga kura, hiyo ni sheria nyengine. Lakini hii ni *platform* ambayo itamuezesha kijana yule kuweza kuanza kujitambua. Kwa hivyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe walitafakari hilo na kujua umri ule una umuhimu wa kuwemo katika kundi lile la vijana.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulisisitiza ndani ya mswada wetu ni suala zima la mila na desturi zetu. Mhe. Spika, nimeona humu kuna baadhi ya vipengele na tumetaka kwamba ziwekwe tafsiri za kujua hasa tabia mbaya ni zipi ambazo mtu zinaweza kumuengua kuwa mwanachama. Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, na hili alitafakari vizuri na kuweza kupata uchambuzi wa neno tabia mbaya, ili tuhakikishe kwamba katika utendaji wa Baraza hili basi kweli lisiwepo na tabia mbaya.

Mhe. Spika, jengine ambalo mimi na wenzangu wengi wameligusia ni suala zima la Baraza kuwa karibu na wizara. Mhe. Spika, hili lina umuhimu wake, huwezi kusema wewe mtoto leo uko ndani ya nyumba ukataka kuchukua madaraka yote peke yako mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi najua umuhimu wa vijana kuwa na mamlaka yao wenyewe katika Baraza, najua umuhimu wake mkubwa, lakini haina maana kwamba vijana hawa kwa asilimia 100 wajiendeshe wenyewe. Ni lazima kuwe na mkono wa wizara au mkono wa serikali. Hawa vijana sisi tunawalea Mhe. Spika, hawa ni wakusaidiwa, hawa ni wa kushikwa mkono. Hatuwezi kuwaacha mkono tukasema kwamba watajifanyia kila kitu wenyewe, mimi napingana kabisa na mawazo hayo ambayo yamejitokeza kwa Waheshimiwa Wajumbe wengine. Hakuna mtoto ambaye anakua bila ya kushikwa mkono na mzee wake.

Mhe. Spika, nakubaliana na wengi kwamba kuna mambo ambayo itabidi yapunguzwe. Lakini iko haja kubwa Mhe. Spika, hasa mwanzo wa utekelezwaji wa mswada huu, wizara iwe makini katika kuwaongoza vijana. Mswada huu kwa bahati nzuri sana umeweka sheria ya kuzuia kuingizwa siasa, hiyo itatoa fursa kwa wizara kufikia lengo hilo.

Kwanza Mhe. Spika, mswada huu umeletwa na serikali, ni lazima tutambue hivyo kwa lengo na nia njema. Sasa kama serikali imeleta mswada huu halafu serikali ikasema kwamba waziri hana nafasi yoyote ndani ya mswada huu, haiwezekani. Mhe. Spika, mimi nafikiri hapo tutakuwa tunafanya makosa.

Mhe. Spika, mimi nafikiria sitokuwa na mengi sana, kwa sababu kama nilivyosema mwanzo sioni umuhimu wa mimi kuanza kuchambua kipengele kwa kipengele, hasa kwa sababu tayari tumeshaupitia na maoni yetu kutoka katika kamati. Nafikiria kwamba Waheshimiwa Wajumbe wengi wameyaona kwani itakuwa wamepewa.

Kwa hivyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kuukubali mswada huu na kuupitisha. Hii haina maana kwamba labda yale ambayo yana umuhimu wa kufanyiwa marekebisho yasirekebishwe, la hasha! Ningemuomba sana Mhe. Waziri pamoja na yote, yale ambayo yana umuhimu mkubwa wa kufanyiwa marekebisho katika mswada huu basi yafanyiwe marekebisho. Lakini hapo hapo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuupitishe mswada huu kwa ajili ya manufaa ya vijana wetu wa Zanzibar.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, inaelekea kama vile tumemaliza michango kutokana na marejeo mengi ambayo tunayaona. Kwa hivyo, tumalizie kwa wajumbe wawili wafuatao ambao wameomba dakika chache kila mmoja ili kumaliza mjadala huu.

Kwanza ni Mhe. Abdi Mossi Kombo, na baadae Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye atatumia dakika tano tu. Mhe. Abdi Mosi Kombo, karibu.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ndogo ya mwisho. Kabla ya kutoa mchango wangu na mimi naungana na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya, muasisi Mhe. Saleh Nassor Juma, pamoja na wananchi wa Afrika ya Kusini kwa kuondokewa na wazee muhimu.

Mhe. Spika, kwa kuanza mchango wangu sitozungumza mengi kwa sababu na mimi ni mjumbe wa kamati hii, tumeshatoa maoni yetu hapo juu. Kwa hivyo, nawapongeza wajumbe, wengi wao wameuunga mkono mswada wetu huu ambao umetolewa na Mhe. Waziri kwa kuunda mabaraza ya vijana.

Mhe. Spika, mimi nitachangia kifungu hiki cha 3(1) katika ukurasa wa 343, naanza kunukuu;

> "Kunaanzishwa Baraza la Vijana kwa kifupi *"ZYC"* ambalo litakuwa ni chombo kinachojitegemea na litakuwa;
>
> (a) Lina hadhi ya kisheria na uwezo wa kurithiwa na muhuri wake rasmi;"

Mimi hapa naongeza baada ya kuwa na muhuri pawe na nembo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, ametuletea mswada huu wa vijana. Vijana wetu wa Zanzibar watakuwa na Baraza lao rasmi la kuweza kujiamulia wenyewe, na kupanga kila kitu. Mimi ningeiomba serikali, baada ya kukubalika Baraza hili, serikali iwape uwezo vijana, nyanja za kufanyia kazi, fedha za kujiendesha, na uhuru wa kujiamulia wenyewe vijana kwa yale ambayo watayajadili.

Mhe. Spika, Zanzibar mara nyingi huwa tunaunda taasisi nyingi sana, lakini taasisi hizi huwa zinamezwa, zinaingiliwa na wanasiasa mpaka zile taasisi ambazo zinakuwa hazina maana na zinajitosa katika mambo ambayo hayana msingi wowote.

Mhe. Spika, mimi kwa Mswada huu , waheshimiwa wanasiasa baada ya kuundwa mabaraza haya ya vijana wasijewakageuka mapaka shume. Maana mapaka shume hutafuta watoto baada ya kupata wale watoto wakawatafuna wenyewe. Kwa hivyo, naomba wanasiasa wasijewakaingilia mabaraza yetu ya vijana, wakaja wakawapoteza.

Kwa sababu yatakapoundwa mabaraza ya vijana wanasiasa watakuwa na tamaa, sasa hivi tumeshapata wapiga kura. Nasisitiza na naiyomba serikali kwamba vijana wapewe uhuru kama unavyokusudiwa Mswada huu. Leo vijana wengi wanahangaika hawana pakwenda hata wakiwa na mahitaji, hawawezi kuamua.

Mhe. Spika, nakwenda kifungu cha 4 (1) kinasema hivi:-

> "Uwanachama kwa Baraza utakuwa wazi kwa vijana wote kupitia Mabaraza yao ya Vijana Shehia"

Mhe. Spika, uwanachama tunakusudia kuunda mabaraza ya vijana wa Zanzibar. Pamezungumzwa katika kifungu hiki kwamba vijana watakuwa huru kujiunga bila ya pingamizi. Lakini mimi hofu yangu kwamba serikali hutangaza fursa kwa wananchi, kwa mfano nitatoa katika vitambulisho vya

Mzanzibari. Serikali ilitangaza kila mwananchi anaetimia miaka 18 awe na haki ya kitambulisho.

Lakini hivi sasa kuna wananchi wametimia miaka 18 na vitambulisho hawapati, pamoja nakuwa na vyeti vya kuzaliwa. Na huu uwanachama wa vijana isijekuwa panatangazwa hapa kwamba nafasi zitakuwa wazi kujiunga lakini baadaye wakaekewa pingamizi. Naomba Mswada huu ukipita vijana wapewe fursa bila ya matatizo.

Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naunga mkono Mswada huu na kwa vile mimi ni Mjumbe wa Kamati hii iliyopitia Mswada huu naunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniruhusu kuchangia mambo mawili matatu na kwa vile wizara hii ilikuwa ni miongoni mwa Kamati yangu kipindi kilichopita. Naomba niende moja kwa moja kifungu cha 9 Sehemu ya Nne kuhusu muundo wa vyombo vinavyounda Baraza. Kwanza naupongeza muundo huu ulioundwa kwani umezingatia makundi yote, ikiwamo vijana, wanafunzi, na walemavu. Ni jambo la kupigiwa mfano na kero zao zitasikika kupitia Baraza la Vijana.

Mhe. Spika, ningeomba mswada huu utamke wazi kabisa kiongozi wa Baraza la Vijana asiwe ni mtumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, bangi n.k. Tukizingatia vijana wetu wengi wameathirika.

Mchango wangu wa mwisho ni kuwa Zanzibar ni pande mbili nazo ni Unguja na Pemba. Ni vyema Makao Makuu yakajulikana yatakuwa Unguja au Pemba. Pia ni vyema vikao vifanyike kwa zamu. Nafikiri Mhe. Spika, hata dakika tano haikufika, ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, uliahidi kwamba hutozidi dakika 5 na kweli umefanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri kwa mujibu wa mjadala ulivyokwenda inaelekea kwamba sasa michango iliyotolewa inatosheleza kwa mujibu wa waheshimiwa wajumbe. Kwa maana hiyo, kama tulivyotangulia kusema wakati wa mchana, nimpe Mhe. Waziri, nafasi ili kesho aje afanye majumuisho baada ya kipindi cha maswali. Na kwa kuwa hakuna shughuli nyengine basi tusitishe shughuli zetu kuanzia hapa na niahirishe Kikao hichi hadi kesho tarehe 12/12/2013, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:36 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 12/12/2013 saa 3:00 za asubuhi)